

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TISA

Kikao cha Sita – Tarehe 14 Novemba, 2017

(Bunge lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Tukae, Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

- (i) Toleo Na. 35 la tarehe 01/09/2017
- (ii) Toleo Na. 36 la tarehe 08/09/2017
- (iii) Toleo Na. 37 la tarehe 15/09/2017
- (iv) Toleo Na. 38 la tarehe 22/09/2017
- (v) Toleo Na. 39 la tarehe 29/09/2017
- (vi) Toleo Na. 40 la tarehe 06/10/2017
- (vii) Toleo Na. 41 la tarehe 13/10/2017

- (viii) Toleo Na. 42 la tarehe 20/10/2017
- (ix) Toleo Na. 43 la tarehe 27/10/2017

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):

Maelezo ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa Mwaka 2017 (*The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017*)

MHE. HAWA M. CHAKOMA (K.n.y. MHE. NORMAN A.S. KING - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU):

Maoni ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa Mwaka 2017 (*The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017*)

MHE. QAMBALO W. QULWI (K.n.y. MHE. JAMES F. MBATIA - MSEMaji MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI WA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO):

Maoni ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa mwaka 2017 (*The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017*)

NAIBU SPIKA: Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali. Tutaanza na ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimwa Sonia Jumaa Magogo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 68

**Watumishi ambao Hawajaandikishwa Kwenye
Mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

MHE. SONIA J. MAGOGO aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani dhidi ya waajiri ambao hawawaandikishi Watumishi wao katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na kuwasababishia kukosa stahiki zao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa Serikali katika kuhakikisha waajiri wote wanaandikisha wafanyakazi wao kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ni kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii Na. 8 ya Mwaka 2008, Kifungu cha 30 ambacho kimeweka utaratibu unaomtaka mwajiri kuwaandikisha watumishi wake katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Aidha, mwajiri anayekiuka matakwa ya kifungu hiki anastahili adhabu ya kulipa faini ya kiasi kisicho zidi shilingi milioni ishirini kwa mujibu wa kifungu cha 55 cha Sheria ya Usimamizi na Udhhibiti wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha usimamizi wa Sheria za Kazi, Serikali kupitia Bunge ilifanyia marekebisho ya Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya mwaka 2004 ili kuimarisha mfumo wa kaguzi za kazi mahali pa kazi kwa kuruhusu kutoa adhabu za papo kwa papo kwa waajiri wanaokiuka matakwa ya sheria ikiwa ni pamoja na kutosajili au kuandikisha wafanyakazi katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sonia Magogo, swali la nyongeza.

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, Serikali ina mkakati gani juu ya vijana ambao wamekuwa wakipata ajira za muda mfupi na kushindwa kuendelea na ajira zile, lakini kwa kigezo cha umri wamekuwa wakishindwa kupata mafao yao ambayo yangeweza kuwasaidia katika kuendeleza maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kumekuwa na tofauti ya pensheni za kila mwezi kutoka mfuko mmoja na mwingine. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha wazee hawa wanaostaafu wanapata pensheni iliyo sawa ya kila mwezi na ambayo inaweza kuwasaidia kuendesha maisha yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri, tukifuata mtindo huu wa kuuliza maswali, Waheshimiwa Wabunge tutapata muda wa kuuliza maswali mengi sana. Kwa hiyo Mheshimiwa, japokuwa ni Mbunge mgeni ameuliza vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza alikuwa anazungumzia kiujumla kuhusu fao la kujittoa na amewazungumzia vijana ambao bado hawajafikia umri wa kupokea pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo tumesema awali katika Bunge lako kwamba Serikali inaendelea kulifanyia kazi suala hili la fao la kujittoa. Hivi sasa tupo katika utaratibu wa kushirikiana na wadau ili kutengeneza kwa pamoja mfumo mzuri ambao utawa-*cover*watu wote katika makundi tofauti tofauti. Hivyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge, kwa sababu jambo hili bado linafanyiwa kazi na Serikali tutakuja na mpango mzuri wa kuweza kusaidia kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu pensheni, tayari *SSRA* wameshatoa miongozo kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kulipa kima cha chini cha pensheni sawa kwa mifuko yote na ambayo hivi sasa imeanza kutekelezwa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara, swali la nyongeza.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swali dogo la nyongeza. Hivi karibuni kumekuwa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba Watumishi wa Umma wakiwemo na Walimu, wasihamishwe kutoka kituo kimoja kwenda kingine bila kuwa na malipo ama stahiki zao. Vilevile kumekuwa na uhamishaji huo unaendelea katika Halmashauri mbalimbali na sasa hivi ninavyozungumza kuna mgogoro mkubwa kati ya Walimu na katika Wilaya ya...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara, nimetoka kutoa ushauri sasa hivi. Muda hautatoshwa Wabunge wote wakianza kutoa maelezo. Uliza swali ili uweze kujibiwa.

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu ni kwamba naomba nipate majibu ya Serikali, Rais ametoa maelekezo watumishi wa umma wasihamishwe kutoka kituo kimoja kwenda kingine bila malipo yao, lakini Wakurugenzi wameendelea kuhamisha walimu na watumishi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara, nadhani sasa huna swali ndugu yangu kwa sababu unarudia maelezo uliyotoa mwanzo. Sasa hivi nimekwambia uliza swali, unaenda maelezo marefu. Naomba ukae. Mheshimiwa Mtolea.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sekta hizi zisizo rasmi na hapa nawalenga hasa wale wanaofanya kazi za

daladala kwa maana ya madereva wa madaladala na makondakta wao na hii ni sekta ambayo imeajiri vijana wengi na watu wengi. Kimsingi wana malalamiko mengi ya haki za wafanyakazi, kwamba hawapewi stahiki zao. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakuwa tayari kukutana na Madereva na Makondakta wa daladala ili asikilize kero zao na uweze kuzipeleka Serikali kwa ajili ya kuzishughulikia, ukianzia Temeke? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii kama Wizara tumekuwa tukiifanya, tutaendelea kuifanya na nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba nipo tayari kukutana nao na kujadiliana nao kuhusu haki ambazo zinawahusu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje, swali la nyongeza.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Swali langu ni kwamba, kwa kuwa kuna waajiri ambao wanakata mshahara lakini hawapeleki fedha hizi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Je, Serikali inawachukulia hatua gani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa sheria kila mfanyakazi aliyeandikishwa na anayekatwa makato yake kwa ajili ya hifadhi ya jamii yanapaswa kuwasilishwa katika mfuko husika. Kinyume na kufanya hivyo ni kukiuka taratibu za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana baada ya kuziangalia sheria zetu tukafanya marekebisho ya mwaka 2016 katika Sheria Na. 7 ya Mwaka 2004 ambayo

inashughulikia masuala ya Taasisi za Kazi ambapo lengo lake ni ku-*compound* hizo *fences* na inapotokea mwajiri amekiuka taratibu hizi tutakachokifanya ni kwenda kumpiga faini ya papo kwa papo ili kufanya *deterrence* na kumpunguzia mzigo mfanyakazi lakini kumfanya mwajiri awe ana-*comply* na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyika kwa mwajiri kuwasilisha mchango wa mwajiriwa wake ikiwa ni haki yake ya mchango ambao ni sehemu ya mshahara wake.

NABU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 69

Hitaji la Vifaa Tiba – Hospitali ya Wilaya ya Singida

MHE. MUSSA R. SIMA aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa vifaa tiba kwenye Hospitali ya Wilaya ya Singida Mjini au kituo cha afya Sokoine?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sima, Mbunge kutoka Singida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanikiwa kununua vifaa tiba vyenye thamani ya Sh.102,939,700.00 kwa kutumia fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Vifaa vilivyonunuliwa ni vitanda vitatu (3) vya kujifungulia, mitungi mitano (5) ya kuhifadha gesi, vitanda ishirini (20) vya hospitali na mashine tatu (3) za

kutakasia vyombo vya hospitali. Vifaa vingine vilivyonunuliwa ni pamoja na mashine moja (1) ya kutolea dawa ya usingizi (*anaesthetic machine*), kitanda kimoja (1) cha upasuaji (*operation table*) na mashine ya kutakasia vifaa tiba vyenye ujazo wa lita 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Serikali imetenga jumla ya Sh.160,866.466.01 kwa ajili ya kununua vifaa tiba kwenye kituo cha afya cha Sokoine. Kati ya fedha hizo, Sh.41,451,400 zimeshalipwa Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*)kwa ajili ya vifaa tiba. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima swali la nyongeza.

MHE. MUSSA R. SIMA: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali lakini bado kuna changamoto kubwa kwa akina mama wajawazito wanapokwenda hospitali za umma kwa ajili ya kupata vipimo na matibabu mengine, vifaa havipatikani. Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali inafanya kazi nzuri sana ya zoezi la ukusanyaji damu salama na imetoa mwongozo mzuri kwa Halmashauri zetu kutenga bajeti kwa ajili ya kukusanya damu salama, lakini bado ziko Halmashauri zimeshindwa kutenga bajeti hiyo. Je, Serikali pia inatoa tamko gani kwenye Halmashauri hizi zilizoshindwa kufanya kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali langu

la nyongeza na mwenyewe amekiri jitihada kubwa ambazo zinafanywa na Serikali ili kuhakikisha kwamba vifaa tiba vinapatikana na kuondoa adha na hasa kwa akinamama kama ambavyo na yeye mwenyewe amekuwa mdau mkubwa kuhakikisha kwamba akinamama hawapati adha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee naomba niendeleo kupongeza Halmashauri yake ambayo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akihakikisha kwamba vifaa tiba vinanunuliwa. Nizitake Halmashauri zingine wahakikishe kwamba vifaa tiba vinatengewa pesa na vinanunuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimpongeze Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri yake kwa sababu katika hizi pesa ambazo zimelipwa milioni 41 niliyotaja ni pamoja na kitanda cha upasuaji kimeshalipiwa, mashine ya kutolea dawa ya usingizi, jokofu la kuhifadhiya damu kama ambavyo amesema Halmashauri zingine hazifanyi, wao wanafanya vizuri sana; mashine ya kufulia moja, vitanda vya kujifungulia vinne, mfumo wa hewa ya *oxygen*, vitanda vya kubebea wagonjwa. Kwa hiyo, kwa ujumla nizitake Halmashauri zingine zote nchini waige mfano mzuri ambao wenzetu wanafanya ambako Mheshimiwa Mbunge amesemea.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa John Kadutu, swali la nyongeza.

MHE. JOHN P. KADUTU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Serikali iliahidi kupeleka fedha za kutosha kwa ajili ya ukarabati na kuviwezesha vituo vya afya karibu sehemu yote ya nchi. Mojawapo ni kituo cha afya cha Ulyankulu. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutupa *status* ya utumaji wa fedha hizo kwenye vituo vya afya kote nchini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri wangu kwa ufafanuzi mzuri wa swali la awali. Hata hivyo, napenda kutoa *status* ya suala la ujenzi wa vituo vya afya ambavyo tumesema ni ukarabati mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulifanikiwa kupata fedha kutoka mifuko miwili. Fedha kutoka *World Bank* ambapo lengo letu ni ukarabati vituo vya afya 100, lakini nyingine tulipata fedha kutoka Ubalozi wa Canada tumeshazipeleka katika kila kituo takriban shilingi milioni 500. Hali ya ujenzi mpaka sasa, wengine wako katika *stage* ya lenta na wengine wanapauwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotoka Mfuko wa *World Bank*, fedha zile zilichelewa kidogo ambapo ndani ya wiki hii fedha hizo ndio zitafika vituoni, japokuwa tulitoa *deadline* kwamba, tarehe 30 mwezi wa 12 vituo vyote viwe vimeweza kukamilika, kwa sababu hizi fedha kutoka Mfuko wa *World Bank* zilichelewa kufika vituoni tuta-*extend* huo muda angalau tufike mwishoni mwa mwezi Januari. Hali halisi hivi sasa fedha za Canada zimeshafika, lakini za *World Bank* ndiyo wiki hii zinafika vituoni. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joyce Sokombi, swali la nyongeza.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi hii. Napenda tu kumuuliza Mheshimiwa Waziri ni lini Kituo cha Bunda Mjini kitapewa hadhi ya hospitali ya Wilaya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, suala la

mchakato wa kupandisha kituo cha afya kuwa hospitali ni utaratibu. Mchakato huo unaanzia katika Halmashauri kwenye Baraza la Madiwani linafanya hivyo *and then* inaenda DCC, RCC, baadaye inafika kwa Waziri mwenye dhamana wa sekta ya afya; atakapooona kwamba kituo hiki kimekidhi na inafaa kufanya hivyo, basi atafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kama mchakato huo umeshaanza basi, jukumu hilo litakuwa chini ya Ofisi ya Waziri wa Afya, atakapooona kwamba vigezo vimekamilika na inabidi kufanya hivyo basi atafanya hivyo bila tatizo. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Josephine Tabita Chagula, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 70

Matatizo Yanayoikabili Hospitali ya Mkoa – Geita

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA aliuliza:-

Hospitali ya Mkoa wa Geita inakabiliwa na kero mbalimbali kama vile ukosefu wa Madaktari Bingwa wa akinamama na watoto, dawa, vifaa tiba pamoja na uhaba wa majengo ya wodi za wazazi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kutatua kero hizo katika Hospitali ya Mkoa wa Geita?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tabitha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mkoa wa Geita ina Daktari Bingwa mmoja wa upasuaji. Madaktari wengine

watatu wako masomoni akiwemo Daktari Bingwa wa Magonjwa ya akina Mama na Watoto. Ukosefu wa Madaktari Bingwa unasababishwa na uchache wa Madaktari ukilinganisha na uhitaji wetu. Katika kibali cha mwaka wa fedha 2017/2018 cha kuajiri watumishi 2,058 kilichokuwa na Madaktari 46, Hospitali ya Mkoa wa Geita imepangiwa jumla ya Madaktari wanne ambao wamesharipoti na wameanza kazi, naamini Madaktari hao watapunguza uhaba uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliwa na changamoto ya upungufu wa dawa, Mkoa wa Geita umepanga kuanzisha duka la dawa kwa kutumia mkopo wa shilingi milioni 160 kutoka *NHIF*. Wagonjwa watapatiwa dawa na vifaa tiba kwa gharama nafuu zaidi ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kutatua tatizo la uhaba wa miundombinu mkoa unaendelea na ujenzi wa Hospitali Mpya ya Rufaa ya Mkoa wa Geita. Ujenzi upo katika hatua za msingi kwa majengo manne ambayo ni jengo la upasuaji, wagonjwa wa nje, jengo la mionzi na jengo la kufulia nguo. Kazi hii inatekelezwa na Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Chagula, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE T. CHAGULA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza niishukuru sana Serikali kwa mkakati huo, pia nimshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kutia moyo. Nina swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mkoa wa Geita imekuwa ikihudumia wagonjwa wengi sana kiasi kwamba inaelemewa kabisa. Hii ni kutokana na mapungufu makubwa yaliyopo katika Hospitali zetu za Wilaya. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuweza kuboresha hospitali zetu hizi za Wilaya ili kupunguza msongamano wa wagonjwa

uliopo katika Hospitali yetu ya Mkoa wa Geita? Ahsante.
(Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE): Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Serikali ina nia njema ya kuhakikisha kwamba, kwanza si kuimarisha Hospitali za Wilaya, tunaanzia kwanza kuimarisha vituo vya afya ndiyo maana pesa nyingi sana imepelekwa ili kupunguza ule msongamano ambao wananchi watalazimika kwenda hospitali za Wilaya. Kama hilo halitoshi tunajua kabisa, ili kuweza kupunguza mlundikano kwa wananchi ambao wangependa kwenda hospitali za mikoa ni kuwa na uhakika wa kutibiwa katika hospitali za wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwatake wananchi na Halmashauri zetu zote nchini, wahakikishe kwamba, maeneo kwa ajili ya kujenga hospitali za Wilaya yanatengwa kwa kufuata viwango ambavyo vinatakiwa na Halmashauri kwa kutumia *own source* waanzishe na Serikali itaweka mkono wake. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge mmesimama wengi mpaka inakuwa balaa. Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la yongeza.

MHE. JOSEPH M. MKUNDI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Matatizo ya upungufu wa Madaktari, watumishi wengine wa afya na vifaa tiba yaliyoko hospitali ya Mkoa wa Geita ni sawa kabisa na yale yaliyoko kwenye Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe, Hospitali ya Nansio. Serikali iko tayari sasa kuangalia visiwa vya Ukerewe kwa upendeleo maalum na kutusaidia kuondoa tatizo hili ili kupunguza vifo vya akinamama na watoto visiwa vya Ukerewe?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli. Mheshimiwa Mbunge anakiri kwamba, nilipata fursa ya kwenda na tuliweza kufika mpaka kule Ukerewe na ni kweli changamoto ya afya katika visiwa vile imekuwa ni kubwa zaidi. Ndiyo maana katika vipaumbele vyetu sasa hivi hata ukiangalia idadi ya Madaktari ambao juzi tu tumewaajiri, tumeajiri Madaktari takribani 2,058, tumepeleka vijana kule kwa ajili ya kusaidia suala la changamoto inazozipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kuna fedha vilevile tunaenda kuboresha kile kituo cha afya kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge na hatutasita kuendelea. Tunafanya juhudi ya kutosha hasa kwa sababu tunajua kwamba eneo la Ukerewe lazima tuboreshe miundombinu ili hata watumishi tunaowapeleka kule wawe na hamasa ya kufanya kazi baada ya kuboresha mazingira yao. Kwa hiyo, jukumu hili tumelichukua sisi Serikali kwa ajili ya maslahi mapana ya wananchi wa Ukerewe.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hili swali kwa sababu linahusu akinamama na watoto, naona ni zamu ya akinababa sasa waseme habari za akinamama.

Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, swali la nyongeza.

MHE. CONSTANTINE J. KANYASU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Hospitali ya Geita ambayo sasa hivi ni Hospitali Teule ya Mkoa ilikuwa Hospitali ya Wilaya. Hata baada ya kuipandisha hadhi na kuwa hospitali ya mkoa imeendelea kupata huduma kutoka Serikali Kuu kama hospitali ya wilaya. Je, ni lini Serikali itaipatia huduma kama hospitali ya mkoa?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, swali linauliza ni lini?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba, kwa sababu imepandishwa, tunalifanyia

kazi. Hata hivyo juhudi tuliyofanya kubwa kama Serikali ni kuhakikisha tunaanza hospitali ile kubwa ya Rufaa ya Mkoa, juzi Naibu Waziri wangu nimemtuma kuna kazi kubwa imeshaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie wananchi wa Geita kwamba Serikali tumejipanga kuboresha sekta ya afya katika Mkoa wa Geita kwa ujumla wake ili kuimarisha hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa na hospitali ya Mkoa na hali kadhalika vituo vya afya, tukijua kutokana na uchimbaji wa madini *population* imekuwa kubwa katika maeneo hayo. Kwa hiyo, kama Serikali tumelichukua, tutalifanyia kazi kuhakikisha tunapata idadi ya dawa zinazohitajika katika hospitali. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa James Francis Mbatia.

Na. 71

**Sheria ya Maslahi na Mafao ya Majaji Namba
Tatu ya Mwaka 2007**

MHE. JAMES F. MBATIA aliuliza:-

Sheria ya Maslahi na Mafao ya Majaji Namba tatu (3) ya Mwaka 2007 Kifungu cha 8; inafafanua kuwa Jaji Mkuu, Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji Kiongozi au Jaji wa Mahakama Kuu akifariki dunia akiwa madarakani au baada ya kustaafu, Serikali itagharamia gharama za mazishi na Kifungu cha 10 cha Sheria hiyo kinafafanua malipo ya pensheni na huduma nyingine atakazostahili Jaji wakati wa kustaafu kama ilivyo kwenye Kifungu cha 20 na 21 cha Sheria ya Utumishi wa Umma:-

Je, Serikali haioni busara kuifanyia marekebisho sheria hiyo au vinginevyo ili Majaji waweze kupatiwa huduma muhimu na hasa matibabu wakati wanapostaafu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Francis Mbatia, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Malipo ya Mshahara na Mafao ya Hitimisho la Kazi kwa Majaji (*The Judges Remuneration and Terminal Benefits Act*) na Namba tatu (3) ya Mwaka 2007 katika Kifungu cha 10 na Vifungu vya 20 na 21 vya Sheria ya Mafao Katika Utumishi wa Umma (*The Public Service Retirement Benefits Act*) Sura ya 371 zinaweka utaratibu wa mafao na stahili za Majaji baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, masharti ya kazi na stahili za Majaji, kwa maana ya Jaji Mkuu, Majaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji Kiongozi na Majaji wa Mahakama Kuu yamefafanua kuwa, Majaji hao wamejumuishwa katika utaratibu wa matibabu kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya afya wawapo kazini na gharama hizo hulipwa na Serikali na hata wanapostaafu wanaendelea kupata huduma hizo kupitia Mfuko huo. Kwa wale waliostaafu kabla ya masharti hayo kuanza kutumika hawanufaiki na Mfuko huo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa James Mbatia, swali la nyongeza.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Swali la kwanza, Majaji waliostaafu kabla ya mwaka 2013 ambao siyo wengi, hawako kwenye hali nzuri sana wakati wa kupata matibabu. Serikali haiwezi ikatumia busara hili suala likawa ni la kiutawala (*administrative*) ili bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria ikawahudumia Majaji hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, *Political Leaders Pension Act* ya Mwaka 1981 inaelezea pamoja na watu wengine ambao wanatakiwa kupata *pension*, angalau

wapo kazini kwa miaka 10 ni Wabunge. Je, Serikali haioni busara kuleta Muswada hapa Bungeni ili kufufua Sheria hii ya mwaka 1981 ili Wabunge waweze kupata *pension*? (Makofi)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la kwanza amezungumza kuhusu Majaji waliostaafu kuanzia mwaka 2013. Kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge ni kweli kwamba, kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Bima ya Taifa ya Afya, Kifungu Namba 11(3) kinaeleza kuhusu wale watumishi wa Serikali waliokuwa wana-*hold Constitutional Office* ambao wanaweza kunufaika katika matibabu ya afya. Hata hivyo, katika Kifungu hicho pia, kupitia Sheria hii ya Mwaka 2007 imetamka pia, aina ya watu wanaostahili kupata huduma na stahiki kutokana na sheria ambayo imesomwa ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, katika hili ombi la Mheshimiwa Mbunge la kwamba Serikali ione busara, kwa sababu ni suala ambalo linahusisha pia Sera na Sheria niseme tu kwamba, kama Serikali tunalichukua, lakini siwezi kuweka *commitment* ya kwamba litafanyika, ni pendekezo limetolewa, linahitaji kwenda kuangalia sera na sheria ambazo zinatungoza, hasa kuanzia yale mafao ya Majaji, na sheria ambazo pia zinahusika kwa maana ya watoa huduma katika baadhi ya masuala ambayo yanawahusu Majaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali lake la pili ameuliza kuhusu *pension* kwa Wabunge. Ombi la Mheshimiwa Mbunge hapa ni kufufua tu sheria, sasa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu, masuala haya yanaweza kupitia Tume ya Utumishi wa Bunge na ninyi ndiyo Wabunge, lianzie kwenu kwanza ndiyo lifike Serikalini. Kwa hiyo, hii ni kazi ya Kibunge lianzie katika upande wa Bunge. (Makofi)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 72

Kurejesha *Community Centres*

MHE. FATMA H. TOUFIQ aliuliza:-

Katika miaka ya 70 kulikuwa na *Community Centres* ambapo wananchi wa rika tofauti walikuwa wakikutana na kubadilishana mawazo na maeneo hayo yalikuwa ya muhimu kupata huduma za jamii kama afya ya akili, wananchi wenye msongo wa mawazo, ugonjwa wa kisukari, kifafa, pumu na shinikizo la damu:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurejesha *Community Centres*?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Majibu.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge walimpigia makofi mengi Mheshimiwa Naibu Waziri)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya naona unapigiwa sana makofi, wanayajua tayari majibu nini. *(Makofi)*

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa siku hii ya leo, lakini namshukuru vilevile Mheshimiwa Rais kwa imani yake kwangu. Niwashukuru pia wananchi wa Kigamboni kwa kuendelea kuwa na imani nami kama mtumishi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali Namba 72 la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na pia namuunga mkono Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri kuhusiana na suala zima la kurejesha majumba ya maendeleo na umuhimu wake ulionekana hapo awali katika Halmashauri mbalimbali nchini kwa dhumuni la kuwapatia wananchi taarifa mbalimbali, maarifa, burudani, lakini pia stadi za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapendekezo yaliyotolewa na Wizara yangu ya kuimarisha sekta ya maendeleo ya jamii ya mwaka 2007, pamoja na mambo mengine yaliyopendekezwa suala la kuyafufua majengo ya maendeleo na kuyarejesha katika matumizi yake ya awali lilitiliwa mkazo. Hata hivyo, Halmashauri 135 ndizo zilizokuwa na majumba ya maendeleo yaliyojengwa mwaka 1961 na mwaka 1962. Zipo Halmashauri zimerejesha matumizi ya awali ya majumba hayo, ikiwa ni pamoja na Iringa Manispaa, Dodoma Manispaa na Mpwapwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo Halmashauri ambazo zimebadilisha matumizi ya majengo haya na hayawezi yakarudishwa katika matumizi ya awali. Kwa mfano, Manispaa ya Temeke imekuwa Hospitali ya Rufaa, Manispaa ya Mtwara imeendelezwa na kuwa Ofisi ya Ardhi na Maendeleo ya Jamii na Manispaa ya Ilala imeendelezwa na kuwa Ofisi za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara yangu imekuwa ikifanya mawasiliano na Ofisi ya Rais, TAMISEMI mara kwa mara, juu ya kukumbusha Mamlaka ya Serikali za Mitaa kurejesha matumizi ya majengo ya maendeleo kwa lengo la kutumika kama sehemu ya kujadili masuala ya maendeleo, kupata taarifa mbalimbali, burudani na stadi za maisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa rai kwa

Waheshimiwa Wabunge kuwa, hili ni jukumu la kila Halmashauri, hivyo niwaombe tunapokutana katika vikao vyetu kujadili mipango mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri zetu, basi tulisitize suala hili muhimu na lipewe uzito unaostahili ili kulitekeleza kwa vitendo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fatma Taufiq swali la nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa, Serikali imeona umuhimu wa kufufua na kurejesha majengo ya maendeleo ya jamii. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupata wataalam wa kutosha ili kuhudumu katika majengo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa, hali ya maisha imebadilika sana na wananchi wengi wana msongo wa mawazo na matatizo mbalimbali, mfano, masuala ya ukatili, hivyo wanahitaji wataalam wa unasihi na nasaha. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka muda maalum ili kuharakisha Halmashauri zote nchini zifufue majengo hayo? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Ni kweli tumekuwa na changamoto kubwa sana ya watumishi katika Sekta nzima ya Maendeleo ya Jamii na hivi sasa tuna upungufu wa asilimia takribani 61. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuchukua jitihada mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza udahili katika mafunzo ya watumishi katika sekta hii, mpaka sasa hivi tumeongeza udahili kwa kiasi kikubwa sana. Lengo ni kuhakikisha kwamba sasa huu upungufu tulionao tunaweza tukapata watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili kwamba, kutokana na kuonekana kuna wananchi wengi sasa hivi wamekuwa na msongo wa mawazo, tunapokea ushauri huu nasi katika sekta ya afya tutaangalia njia nzuri zaidi ya kuweza kulifanyia kazi jambo hilo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka, swali la nyongeza.

MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba niulize swali dogo tu kuhusiana na idara hii ya maendeleo ya jamii.

Kwa kuwa, idara hii ya maendeleo ya jamii ni muhimu sana katika Vijiji, Kata na Halmashauri zetu kwa ujumla, lakini unakuta idara hii haijaimarishwa na kwa muda mrefu Maafisa Maendeleo wamekaa katika sehemu moja kwa miaka mingi na bila nyenzo za kufanyia kazi. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuimarisha kitengo hiki na kuwasaidia Maafisa Maendeleo ya Jamii ili wafanye kazi yao ambayo sasa hivi tunavyoingia katika viwanda ndio watasaidia sana kuhamasisha wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua mchango mkubwa wa Maafisa Maendeleo ya Jamii hususan katika kuhamasisha na kufua hali ya wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika majibu yangu ya hapo awali ni kwamba Serikali inatambua suala hili na kupitia Sera ya Maendeleo ya Jamii ya mwaka 1997, tumesisitiza kwanza kuweka msisitizo katika masuala mazima ya udahili; pili. kuweka msukumo sasa katika kupitia Serikali kuu na katika Halmashauri zetu kuweka msisitizo katika

kuhakikisha kwamba Maafisa Maendeleo ya Jamii wanapata kipaumbele na wanaajiriwa ili waweze kwenda kuhudumu katika Halmashauri zetu. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

MHE. FLATEI G. MASSAY: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri ametoa majibu mazuri ya kueleweka katika maswali haya na katika majibu yake ya msingi. Je, yupo tayari sasa kuandika maelekezo haya yaende kwenye Halmashauri yetu ili hizi *Community Centers* zifanye kazi yake iliyokusudiwa? *(Makofi)*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile kwa umahiri wake wa kwenda vizuri katika eneo hilo la afya na maendeleo ya jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwa muda mrefu sana Maafisa Maendeleo ya Jamii walikuwa wanatumika kama *spare tyre*. Matumizi yao mara nyingi sana katika Halmashauri zetu walikuwa hawatumiki vizuri, lakini kuanzia sasa ndiyo maana *last week* tulikuwa na *training* kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii yaliyodumu kwa siku tano mfululizo. Licha kutoa mafunzo hayo tuliwapa *terms of reference* nini wanatakiwa kufanya katika kazi zao. Namshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama, Waziri wa Afya na Waziri wa Viwanda, tuliwapa mwongozo maalum kwa ajili ya kwenda kusimamia katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa nimewaagiza Wakurugenzi wote kwa sababu Maafisa Maendeleo ya Jamii ndio *agent of change* katika maendeleo ya Halmashauri zetu. Sasa wawatumie na wawawezeshe kwa rasilimali fedha hali kadhalika kuwafanya kwamba kazi zao zifanyike vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge naomba niwahakikishie kuanzia sasa mtaona mwenendo tofauti wa Maafisa Maendeleo ya Jamii chini ya Wizara ya Afya na chini ya TAMISEMI ambao ndio tunawasimamia kwa karibu zaidi kama waajiri wao. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbene, swali la nyongeza.

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Naomba nami niulize swali la nyongeza kuhusiana na masuala ya matumizi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii na nipendekeze kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna upungufu mkubwa wa Maafisa Maendeleo ya Jamii, vilevile kuna kundi zima la vijana wengi wanaomaliza shule kuanzia Darasa la Saba, Kidato cha Pili, Kidato cha Nne mpaka Kidato cha Sita. Je, kuna uwezekano wa kuwatumia hawa kuwapa mafunzo ili watumike katika Vijiji vyao kama Maafisa Maendeleo ya Jamii hata kama ni *Para Community Development Officers* wa kufanya uraghibishi wa aina mbalimbali ili waweze kusaidia katika nguvu ya maendeleo ya jamii yaliyopo? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Janeth Mbene ametoa ushauri kwa Serikali kwamba kwa sababu sasa hivi tunaelekea Tanzania ya viwanda na tuna changamoto kubwa sana ya vijana ambao hawana ajira; mawazo yake tunayapokea, tutaenda kuyafanyia kazi na kuangalia jinsi gani ya kuweza kuwashirikisha vijana katika kuleta maendeleo. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 73

Kodi ya Umiliki wa Nyumba Kutozwa na TRA

MHE. WILFRED M. LWAKATARE aliuliza:-

Serikali imeamua kuhamisha tozo la kodi ya umiliki wa nyumba kutoka Serikali za Mitaa kwenda *TRA* na hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa mapato na bajeti za Halmashauri nyingi nchini zilizokwishapendekezwa na kupitishwa na vikao vya Halmashauri:-

(a) Je, Serikali inazipa Halmashauri ushauri gani wa kitaalam wa hatua za kuchukua ili kuziba pengo hilo la kibajeti?

(b) Kwa kuzingatia uwezo mdogo uliooneshwa na *TRA* katika kukusanya kodi mbalimbali ambazo wamekuwa wakikusanya kwa mujibu wa sheria. Je, Serikali haioni kwamba uamuzi huu ni kuzidi kuipa *TRA* mzigo mkubwa ambao hawatauweza?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango napenda kujibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge wa Bukoba Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwa kodi ya majengo imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji katika kutekeleza mipango ya utoaji wa huduma na maendeleo kwa wananchi. Hata hivyo, hatua ya Serikali kukasimu jukumu la ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa *TRA* haikulenga kuzinyang'anya Halmashauri vyanzo vya mapato bali ni kuimarisha ukusanyaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na changamoto kubwa kwenye ukusanyaji wa kodi ya majengo

kwenye Halmashauri zetu. Changamoto hizi zipo pia kwa upande wa matumizi ya mapato hayo yanatokana na kodi ya majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba, kunakuwepo na ufanisi katika ukusanyaji na matumizi ya kodi zote zinazokusanywa ndani ya Taifa letu. Aidha, Halmashauri zote zinapata mgawo wa fedha kwa kuzingatia makisio ya bajeti zao na makusanyo ya mapato yote ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo yatokanayo na kodi za majengo kutoka Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji 30 yaliyokuwa yakisimamiwa na *TRA* yameongezeka kutoka shilingi bilioni 28.28 mwaka 2015/2016, hadi bilioni 34.09 kwa mwaka 2016/2017, kipindi ambacho *TRA* ilianza kukusanya kodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 20.6 ya makusanyo halisi yaliyopatikana kutoka Halmashauri husika kabla ya kodi hiyo kuhamishiwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Ongezeko hili la makusanyo linadhihirisha kuwa *TRA* imefanya vizuri zaidi katika kukusanya mapato hayo ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa na Halmashauri hizo 30 katika mwaka wa 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2017/2018, *TRA* ilipangiwa kukusanya kodi ya majengo ya kiasi cha shilingi bilioni 11.9. Hadi kufikia 30 Septemba, 2017, *TRA* ilifanikiwa kukusanya shilingi bilioni 13.2 ikiwa ni ufanisi wa asilimia 111. Kwa mwenendo huu wa makusanyo ni wazi kwamba *TRA* imefanya vizuri kwa sababu ya uzoefu walionao katika kukusanya mapato pamoja na kuwa na mifumo ya kisasa ya kukusanya mapato ikilinganishwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, swali la nyongeza.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali iliyoyatoa hapa, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na takwimu kubwa alizozitoa ambazo zinaonyesha kupanda kwa mapato ni ukweli usiopingika kwamba yapo maeneo mengi kwelikweli ambayo hayajafikiwa na *TRA* kwa sababu ya mtandao wake mdogo, kiasi kwamba *TRA* hata kufanikisha hiki kilichofanikisha imelazimika kuwatumia Maafisa Watendaji wa Kata ambao ni waajiriwa wa Halmashauri hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Serikali isichukue wazo langu la kujaribu kuweka *category* mbili kwamba baadhi ya tozo hii ya *property tax* na hasa za majumba makubwa zitozwe na *TRA* lakini kwa majengo ya chini yatozwe na Halmashauri zetu na hiyo itaongeza ufanisi badala ya kuzi-*tight* kwenye Majiji 30? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; suala la mapato na makusanyo kupanda limekuwa ni wimbo wa kila siku, kutoka kwenye taarifa za Serikali pamoja na *TRA*, lakini Bunge kupitia Kamati zake na kupitia kwenye Halmashauri zetu...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Lwakatare, naomba uulize swali la pili tafadhali. Naomba uulize swali la pili maelezo yamekuwa marefu sana, tafadhali.

MHE. WILFRED M. LWAKATARE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini taarifa zinaonesha Taasisi nyingi za Serikali na Serikali yenyewe na Mashirika pamoja na Halmashauri zetu hata Bunge lenyewe limeshindwa kwenda sambamba na bajeti kiasi kwamba maeneo mengine ina-*read zero, zero* wakati wanasema wanakusanya sana? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpomgeze kwa kukiri kwamba anaelewa sasa mapato ya Serikali yamepanda katika nyanja zote kwa kodi zote zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania ikiwemo kodi ya majengo, nakupongeza sana shemeji yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili alilolisema sasa tugawanye kwamba majengo makubwa yakusanywe na Mamlaka ya Mapato na madogo yakusanywe na Serikali za Mitaa, tutajikuta tunatumia nguvu za aina mbili katika eneo moja bila sababu yoyote ya msingi. Serikali yetu na Bunge lako Tukufu tulipitisha Sheria ya Fedha, kwamba kodi ya majengo ikusanywe na Mamlaka ya Mapato kwa lengo la kuimarisha ufanisi wake katika ukusanyaji na ufanisi wake katika matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali tutaendelea kusimamia sheria hii kuhakikisha kwamba lengo la kuchukua kodi hii linafikiwa na wananchi wetu wanapata huduma stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kwamba sasa bajeti hai-*reflect* mapato. Ni siku mbili zilizopita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI amesema tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani kwa mwaka huu wa fedha kwa robo tu ya kwanza Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepata zaidi ya shilingi trilioni moja katika bajeti zao. Serikali inafanya vizuri kwenye ukusanyaji lakini pia tunafanya vizuri kupeleka fedha hizi katika kila taasisi ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi nimuulize mtani wangu swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha amesema kwamba Serikali inapeleka fedha katika Halmashauri zetu na fedha wanazopeleka kwa upande wa *OC* ni fedha za mitihani tu. Mfano, Halmashauri yangu ya Mji wa Babati wamepeleka 265,605,000 za mitihani tu, hakuna fedha za *OC*. Je, nini kauli za Serikali kuendelea kudumaza Halmashauri zetu, Wakurugenzi wanashindwa kuendesha ofisi na ni lini wanapeleka pesa? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Pauline tena hapa kulikuwa na majibu yako mazito jana hukuwepo saa ya kupokea majibu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nianze pia kwa kumpongeza kwa kukiri kuwa tunapeleka fedha kwenye Halmashauri. Kwa sababu swali hili linahitaji takwimu nitamletea takwimu sahihi katika Halmashauri yake tumepeleka kiasi gani kama *OC* katika utekelezaji wa bajeti. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu.

Na. 74

Watoto Wenye Matatizo ya Afya na Ubongo

MHE. ZAYNAB M. VULLU (K.n.y MHE. MARIAM N. KISANGI) aliuliza:-

Ongezeko la watoto wenye matatizo ya afya ya akili na ubongo limekuwa kubwa kwa sasa katika nchi yetu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha vitengo vya elimu kwa watoto wenye mahitaji maalum (walemavu) wa viungo na ubongo?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa watoto wenye ulemavu wa akili na wenye usonji na jitihada mbalimbali zinafanyika ili kuhakikisha kuwa watoto hao wanapata fursa ya elimu kama watoto wengine. Takwimu za mwaka 2016 zinaonesha kuwa kuna jumla ya wanafunzi wenye ulemavu wa akili na wenye usonji 11,386 katika ngazi ya elimu ya awali na msingi na wanafunzi wenye ulemavu wa viungo 8,115 wanaosoma ngazi ya elimu ya awali, msingi na sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kupanua fursa za upatikanaji wa elimu na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wenye ulemavu nchini. Hatua hizo ni pamoja na:-

Wizara ilitoa mafunzo kazini kwa Walimu wapatao 699 wanaofundisha wanafunzi wenye ulemavu wa akili na wenye usonji kwa lengo la kuwajengea uwezo ili kuinua ubora wa elimu itolewayo; kuboresha miundombinu ya shule ili kukidhi mahitaji ya ujifunzaji kwa wanafunzi wenye ulemavu wa viungo; kuanzisha na kuimarisha vitengo 349 vinavyopokea wanafunzi wenye ulemavu wa akili na wenye usonji nchini; na kufanya mapitio ya mwongozo wa ujenzi wa majengo ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Mwongozo huu utazingatia mahitaji maalum ya wanafunzi wenye ulemavu wa viungo ili kuwawezesha kusoma bila vikwazo wawapo shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inakamilisha uandaaji wa mwongozo wa kufundishia wanafunzi wenye ulemavu wa akili na wenye usonji ambao utasambazwa

katika vitengo vyote 349 vinavyopokea wanafunzi hao. Mwongozo huo una lengo la kupanua uelewa wa Walimu juu ya mbinu za kufundishia, matumizi ya vifaa pamoja na saikolojia ya kufundishia wanafunzi hao kwa ubora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara imetenga jumla shilingi bilioni 3.5 katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na visaidizi kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum wakiwemo wanafunzi wenye ulemavu wa viungo, akili na wenye usonji.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Zainab Matitu Vullu, swali la nyongeza.

MHE. ZAYNAB M. VULLU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Swali la kwanza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, bado inaonekana kuna tatizo la uhaba wa Walimu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inatoa Walimu wa kutosha ili waweze kufika kwenye Halmashauri zetu. Pia kuwa uwezo wa kupata Walimu wengi kwa sasa hivi haupo, je, hakuna haja ya kwamba wachukue Maafisa Afya kwenye Kata zetu waweze kusaidia watu ambao wana watoto wenye matatizo ya akili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa, tatizo la ugonjwa wa akili au usonji linaongezeka nchini. Je, chanzo cha tatizo hilo ni nini, ni lische duni, uhaba wa madini wakati mama anapokuwa mjamzito au ni nini kinachopelekea mpaka kuwa na idadi kubwa ya watu wenye ugonjwa wa akili? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba kwa kiasi fulani kuna changamoto ya kuwa na Walimu wa

kutosha kwa ajili ya kuwafundisha watoto wenye matatizo ya akili na usonji. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba pamoja na changamoto hiyo Wizara imejipanga kuhakikisha kwamba katika siku za huko mbele tatizo hilo linaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati hiyo imeanza kwa kujenga chuo cha kisasa cha kufundishia Walimu cha Patandi. Tunajenga *The State of Art College* kwa ajili ya kufundisha Walimu watakaotoa huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji hayo. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba siyo kwamba Serikali haijajipanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wazo lake alilopendekeza kwamba tuwatumie Maafisa Maendeleo ya Jamii tutalifikiria kuangalia namna tutakavyoweza kufanya kazi pamoja na kwamba tunafahamu kwamba unahitaji watu maalum ambao wanajua saikolojia na namna nzuri ya kuwafundisha watoto hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na chanzo, kuna vyanzo mbalimbali vinavyosababisha watoto wazaliwe wakiwa na hayo matatizo. Mojawapo ni suala la *alcoholic disorders* hasa kwa akinamama wajawazito. Ni muhimu sana kujua kwamba tayari kuna tafiti zinaonesha kwamba kama mzazi akiwa mjamzito atakuwa mlevi sana inasababisha mara nyingi mtoto kuzaliwa akiwa na haya matatizo. Sababu ya pili ni kwamba magonjwa mengine ni ya kurithi, kwamba watoto wanazaliwa kwa sababu wamerithi kutoka kwa wazazi na kuna sababu nyingine, kwa vyovyote vile nina uhakika wenzetu wa afya wanaweza wakawa na taarifa sahihi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kama wameongezeka au hawajaongezeka, kama Wizara ya Elimu tunachofahamu na tunachofanya ni kwamba, tunajua tumeendelea kuongeza uwezo wetu wa kuwapokea wengi zaidi. Ndiyo maana kama ninavyosema, tumeendelea kutenga fedha kila mwaka; mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 3.5 kuhakikisha kwamba wanafunzi wale katika shule

za msingi na sekondari wanapata vifaa vya kuwafundishia. Vilevile hata katika ujenzi wa majengo wa sasa ukienda kwenye shule za msingi yanajengwa ili yaweze kukidhi mazingira maalum ya wanafunzi wa aina hii. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, nataka kuongeza maelezo mafupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa hivi ina mkakati, imeonekana kwamba siku 1,000 za mwanzo za mtoto baada ya kuzaliwa iwapo atapata tatizo la utapiamlo zinamuathiri sana katika kukua vilevile kiakili. Kwa hiyo, sasa hivi Serikali kupitia Taasisi yake ya Lishe, imeweka mkakati wa kuhakikisha kwamba siku 1,000 za mwanzo mtoto anapata lishe nzuri ili kuhakikisha kuwa anakua vizuri na anapata uwezo mzuri wa kuweza kuwa na akili sawasawa.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Zainab Amir, swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuweza kuwapatia wanafunzi hususan wa shule za msingi angalau mlo mmoja kwa siku?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni lini Serikali itahakikisha kwamba wanafunzi watapata angalau mlo mmoja kwa siku, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kuna utaratibu unaoendelea kwenye shule nyingi nchini

kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapata uji wakiwa shuleni. Hata hivyo, katika Mpango wetu wa elimu bila malipo, tayari tunafikiria kufanya maboresho ili masuala kama haya ya mlo vilevile yaweze kuchukuliwa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Hongoli, swali fupi.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Jimbo la Lupembe katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, tuna shule moja ya Matembwe ambapo watoto wenye ulemavu tofauti tofauti wanasoma pale na tuliomba vifaa vya kufundishia na kujifunzia wanafunzi kutoka Wizarani au Serikali lakini mpaka sasa bado hatujapata. Nataka kujua ni lini Serikali italeti vifaa kwa ajili ya kuwawezesha watoto wale waweze kupata elimu vizuri, kwa kuwa vifaa sasa hivi hawana? Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, katika bajeti ya mwaka uliopita 2016/2017, tulitoa vifaa kwa shule 213 za msingi na shule 22 za sekondari. Mwaka huu tumetenga shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kununua vifaa. Naomba Mheshimiwa Mbunge aongozane nami nikitoka leo Bungeni ili anieleze mazingira ya shule yake tuweze kuweka kwenye utaratibu wa kugawa vifaa katika bajeti ya mwaka huu.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, wakati mkifanya hivyo, shule zenye watoto wenye ulemavu ziko nyingi katika maeneo mengi, naamini mtafanyia kazi kwenye maeneo yote ambayo yana changamoto zinazofanana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 75

Hitaji la Chuo cha VETA Mkoa wa Simiyu

MHE. ESTHER L. MIDIMU aliuliza:-

Mkoa wa Simiyu hauna Chuo cha Ufundi (VETA):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Chuo cha VETA katika Mkoa wa Simiyu?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mpango wa kujenga vyuo 43 vya ufundi stadi ngazi ya Wilaya kwa awamu. Kipaumbele ni zile Wilaya zisizo na chuo chochote cha ufundi stadi na ambazo maeneo yake yana miradi mikubwa ya Kitaifa kwa manufaa ya Watanzania. Lengo ni kuongeza fursa za kuwapatia ujuzi vijana zaidi ya milioni moja ambao humaliza elimu ya msingi na sekondari na kuingia katika soko la ajira kila mwaka bila ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa Chuo cha Ufundi Stadi Makete kimekamilika na kuanza kutoa mafunzo na vyuo sita vya Wilaya za Namtumbo, Kilindi, Chunya, Chato, Nyasa na Ukerewe vipo katika hatua mbalimbali za maandalizi ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vipya ngazi ya Mkoa katika Mikoa ya Manyara, Pwani, Lindi, Kipawa ICT na Chuo cha Hoteli na Utalii Arusha vimejengwa. Aidha, hatua mbalimbali za maandalizi ya ujenzi wa vyuo ngazi ya Mkoa vya Njombe, Geita, Rukwa, Simiyu na Kagera zinaendelea.

Serikali itaendelea kutenga bajeti ya maendeleo kila mwaka pamoja na kutafuta wafadhili wa ndani na nje ili kuwezesha kujenga vyuo vingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Chuo cha VETA Mkoa wa Simiyu kwa mkopo wa fedha za Benki ya Maendeleo ya Afrika upo katika hatua za maandalizi. Mshauri Elekezi wa kusanifu majengo na kusimamia ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Mkoa wa Simiyu amekamilisha kazi ya kuandaa michoro, makadirio ya ujenzi na makabrasha ya zabuni mwezi Oktoba, 2017. Hatua zinazofuata ni kutangaza zabuni na kumpata mjenzi mwezi huu wa Novemba na kuanza ujenzi wa chuo mwezi Februari, 2018. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Midimu, swali la nyongeza.

MHE. ESTHER L. MIDIMU: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa mpango wake wa kujenga chuo kila Mkoa. Kwa kuwa vijana wengi Mkoa wa Simiyu hawana kazi na ukosefu wa ajira unasababisha vijana wengi kujiingiza kwenye vitendo vya uhalifu. Namwomba Naibu Waziri anihakikishie, ni lini sasa huo ujenzi utanza Mkoani Simiyu ili vijana wajifunze ujuzi waweze kujajiri wenyewe waondokane na umaskini? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sayansi, Elimu na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, kwamba kwa namna tulivyopangilia tutajitahidi tusitoke nje ya mipango yetu, ujenzi unatakiwa uanze Februari mwaka kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho wakati tunasubiri chuo kikamilike, tunaendelea kuwasihia vijana wa Simiyu na wengine wa Tanzania waendeleo kuachana na uhalifu kwa sababu inawezekana isiwe tiba ya changamoto iliyopo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Shaabani Shekilindi, swali la nyongeza.

MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Elimu ya ufundi ni muhimu ili kuwawezesha vijana wetu kuajiriwa au kujajiri. Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha *VETA* Wilayani Lushoto?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye swali la msingi, Serikali kwa sasa ina mpango wa kujenga vyuo 43 katika Wilaya mbalimbali hapa nchini, tayari tumeanza taratibu katika wilaya saba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu ni kwamba Wilaya zote nchini katika wakati mmoja au mwingine zinakuwa na Vyuo vya *VETA*. Kwa hiyo, hata kwake Mheshimiwa Mbunge, Lushoto, kwa vyovyote vile ni sehemu ya Tanzania na ipo katika mipango hii. Naomba tu avute subira kama Waheshimiwa Wabunge wengine vilevile nitakapowaeleza, kwa sababu Serikali imedhamiria kwamba itaendelea kujenga vyuo hivi kadri ya fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimwombe Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba inakuwa ni rahisi zaidi Serikali kuingiza mikono yake au jitihada kama wananchi wenyewe wamehamasika. Kwa hiyo, pale tunapooni wananchi wenyewe wameanza kujichangisha na kuhamasika inakuwa ni rahisi hata Wizara kutumia fedha ambazo zinapatikana kusaidia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Lyimo, swali la nyongeza.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi. Pamoja na Serikali kuendelea kujenga vyuo katika Mikoa na Wilaya, tuna tatizo kubwa sana la Walimu wa Vyuo vya VETA, kwa sababu tuna chuo kimoja tu cha Morogoro ambacho ndicho kinachotoa Walimu. Je, Serikali inatusaidiaje kuhakikisha kwamba Vyuo hivi vya VETA vinavyojengwa na vilivyopo ambavyo vina tatizo kubwa sana la Walimu vinakuwa na Chuo kingine cha Walimu ili kuweza kutatua tatizo la wanafunzi, watoke pale wakiwa wamekamilika? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sayansi, Elimu na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema kwamba kuna changamoto ya kuwapata Walimu wa Vyuo vya VETA. Nimhakikishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mkakati wa kuhakikisha kwamba elimu ya ufundi inapatikana nchini kwa wingi na ubora zaidi ni pamoja na kuhakikisha kwamba tunakuwa na Walimu wa kutosha. Kwa hiyo, katika mikakati ya Wizara kuna mkakati wa kuhakikisha kwamba Walimu pia wanapatikana.

NAIBU SPIKA: Tunaendelea na Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 76

Idadi ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi Nchini

MHE. EDWARD F. MWALONGO aliuliza:-

Elimu ya ufundi ni muhimu ili kuwawezesha vijana kuajiriwa na kujiajiri:-

(a) Je, nchi yetu ina vyuo vingapi vya Ufundi Stadi vya Umma?

(b) Je, kuna vyuo vingapi visivyo vya Umma?

(c) Je, hivi vyote vina uwezo wa kudahili vijana wangapi kwa mwaka?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu kwa mwaka wa 2016/2017 ilikuwa na jumla ya vyuo vya ufundi stadi 127 vya umma na vyuo 634 visivyo vya umma vilivyokuwa vinatambulika na kusajiliwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA). Vyuo 501 kati ya 761 vilipata ithibati ya VETA na viliweza kudahili jumla ya wanafunzi 56,420 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyuo vya ufundi stadi vina umuhimu mkubwa wa kuandaa nguvukazi ya kutosha, mahiri na yenye ujuzi unaotakiwa ili iweze kushiriki katika kujenga uchumi wa viwanda wakati tunaelekea kwenye nchi ya uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa 2016/2017 - 2020/2021 imelenga kuongeza idadi ya wahitimu katika vyuo vya ufundi stadi kutoka 150,000 kwa mwaka 2015 hadi kufikia 700,000 ifikapo mwaka 2021 ili kuongeza fursa za ajira kwa vijana wenye ujuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itakamilisha ujenzi wa vyuo vya ufundi stadi ngazi ya mkoa katika mikoa mitano na ngazi ya wilaya katika wilaya sita. Aidha, itakamilisha ukarabati wa vyuo vya ufundi stadi katika wilaya mbili. Mkakati uliopo ni Serikali kuendelea kutenga bajeti ya

maendeleo kila mwaka pamoja na kutafuta wafadhili mbalimbali wa ndani na nje ya nchi ili kuweza kujenga vyuo vingine.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwalongo, swali la nyongeza.

MHE. EDWARD F. MWALONGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Serikali iliahidi kwamba maeneo yenye vyuo vya wananchi (*FDCs*) itaviongezee uwezo ili viweze kutoa elimu ya ufundi kwa ufanisi zaidi. Je, ni lini Serikali sasa itatimiza hiyo azma katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi, Njombe Mjini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ujenzi wa Vyuo vya *VETA* nchini unasuasua sana na Jimbo la Njombe Mjini lina shule 11 za sekondari, kuanzisha fani ya ujenzi ama umeme gharama yake ni nusu ya gharama ya kujenga maabara ya kemia ama ya baiolojia. Je, Serikali ipo tayari kuzifanya Shule za Sekondari Mgola na Luhololo kuwa shule za Sekondari za Ufundi kwa fani mbili kwa majaribio (*pilot project*)?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu jitihada za Serikali katika kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (*FDCs*); naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara tayari imepata ufadhili wa kuweza kukarabati vyuo 30 kati ya 55 tulivyonavyo vya wananchi. Lengo ni kuhakikisha kwamba vyuo hivi vinarudi katika utendaji bora zaidi, vilevile ikiwezekana waendeleo kutoa elimu ya ufundi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Chuo chake cha Njombe Mjini nimweleze tu kwamba ni fursa imejitokeza kwamba tayari tumepata dola milioni 120 kwenye mradi unaoitwa *Education and Skills for Productive Jobs (ESPJ)*, fedha hizi zinapatikana lakini kwa ushindani. Kwa hiyo hata Chuo chake cha Njombe Mjini inabidi washindane kuomba fedha

hizi ili Wizara iweze kuja kufanya tathmini na kuangalia kama ni chuo ambacho kinahitaji kukarabatiwa, ni fursa ambayo ipo. Kwa hiyo nimweleze tu kwamba fedha zipo tutatangaza muda sio mrefu ili waweze kuziomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mpango wa kurejesha vyuo vyote 55 vya wananchi virudi katika hali yake ya zamani, viwe vyuo vizuri ili viendeleo kusaidia kutoa mafunzo katika maeneo mbalimbali ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili ni kuhusiana...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri, naomba ufupishe kidogo majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na Shule zake za Sekondari za Mgola na Luhololo kuruhusiwa kuwa shule za ufundi hili linajadilika. Nimwombe Mheshimiwa Mbunge kama wao kama Njombe Mjini wanakubali zibadilike kuwa shule za ufundi sisi tuko tayari kama Wizara tufanye majadiliano na kwa hakika itawezekana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Raphael Chegeni, swali la nyongeza.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Maswali Namba 75 na swali Na 76 yanafanana lakini Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu yake ambayo ni mazuri sana amesema kwamba palipo na wananchi na kama wamehamasika na wameshajitolea kuanza kazi za ujenzi wa vyuo kama hivi, Serikali iko tayari kuweza kuwapa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lililopita, Serikali iliwakubalia wananchi wa Wilaya ya Busega kutenga

eneo kwa ajili ya kuanzisha Chuo cha Ufundi Stadi (VETA). Je, wazo hili la Serikali bado liko palepale au limebadilika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu kwa kifupi.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema mwenyewe, kama tayari kuna ahadi thabiti ya Serikali kuhusiana na chuo chake cha VETA Busega, leo hii haiwezi ikabadilika. Kwa hiyo, tuendeleo na majadiliano tokea tulipoacha kutoka kwa wenzetu ili tuone namna bora ya kutekeleza ahadi hiyo. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Antony Komu, swali fupi

MHE. ANTONY C. KOMU: Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa, hivi karibuni Serikali kupitia Waziri Jafo ilitangaza kwamba au ilitoa agizo kila mkoa utengeneze viwanda 100 na kwa kuwa vyyo hivi vya ufundi ni muhimu sana. Je, ni lini Serikali itaanza kutoa ruzuku kama ilivyokuwa ikiahidi mara kwa mara kwenye vile vyyo ambavyo ni vya wananchi, kule kwangu kuna vyyo vya Mawelas, KVTC, Imani ili azma hiyo ya Serikali iweze kutimia haraka? *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika moja kati ya majibu yangu leo, kwa kuanzia tunaanza na ukarabati kabla hatujaanza kufikiria kutoa ruzuku tunaanza kwanza na ukarabati, kama nilivyosema tumepata Dola milioni 120 tunaanza kukarabati vyyo 30 kwanza kati ya 55.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Komu achukulie kama ni hatua

mojawapo kufikia hicho anachotaka ili vyuo vyake viweze kushindania fursa hii ya kukarabatiwa; baadaye sasa vikishakuwa katika hali nzuri ya kuchukua wanafunzi ndiyo tuanze kufikiria masuala mengine kama ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 77

**Kupanua Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga -
Mkoa wa Rukwa**

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA aliuliza:-

Serikali ilipanga kujenga na kupanua Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga Mjini:-

Je, ni lini ujenzi huo utakamilika pamoja na kuwalipa fidia wananchi wanaozunguka uwanja huo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa ukarabati wa uwanja wa ndege wa Sumbawanga upo kwenye hatua ya manunuzi. Mkataba wa usimamizi wa kazi ya ujenzi ulitiwa saini baina ya Serikali na kampuni ya *SMEC* kutoka Australia mwezi Oktoba, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mwezi Juni, 2017 Serikali ilitiliana saina mkataba wa ujenzi wa ukarabati wa uwanja huo na Kampuni ya *Sino-Shine Overseas Construction and Investment East Africa Limited* kutoka Nchini China. Utekelezaji wa mradi huo utakapoanza unategemewa kukamilika ndani ya miezi 18. Kazi ya ujenzi wa uwanja huo zitaanza mara baada ya Serikali kukamilisha taratibu za malipo ya fidia kwa wananchi wanaostahili kulipwa ili waondoke kupisha ujenzi wa uwanja.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya ulipaji wa fidia kwa wananchi watakoathirika na mradi huo yapo katika hatua ya uhakiki wa mwisho kabla ya ulipaji wa fidia kuanza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa wananchi hawa walifanyiwa tathmini ya muda mrefu mpaka sasa hawajalipwa, nataka kujua, je, ni lini Serikali sasa itawalipa wananchi hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa wananchi hawa walifanyiwa tathmini muda mrefu ya nyumba zao na wameshindwa kuziendeleza na kufanya maendeleo. Je, Serikali iko tayari kuwaongezea tathmini ya fidia ili walipwe kiasi kikubwa? (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia maendeleo mbalimbali kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kwamba hivi karibuni Mheshimiwa Waziri alitembelea eneo hili walizungumza na alipata pia taarifa kwamba muda siyo mrefu, wakati wowote wananchi watalipwa hizi fidia. Kwa hiyo, nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge avute subira wakati wa hatua za kukamilisha ili tuweze kuwalipa wananchi wale na ujenzi uweze kuanza basi avute tu subira na wananchi wa Sumbawanga nawashukuru kwa uvumilivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kulipa kwa ziada inategemea na sheria yenyewe na utaratibu wenyewe. Kwa hiyo, nimuahidi tu Mheshimiwa Mbunge labda kama kuna suala la ulazima basi tuzungumze tuone kwamba je, wanastahili kulipwa ziada kutokana na kuchelewa au iko katika hali gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 78

Kukipatia hadhi ya EPZ Kiwanda cha Nyuzi Tabora

MHE. MUNDE T. ABDALLAH aliuliza:-

Pamoja na jitihada za Serikali na mmiliki wa Kiwanda cha Nyuzi Tabora (*TABOTEX*) ambazo zimewezesha kiwanda hicho kuwa katika hali ya kufanya kazi bado kiwanda hicho kinakabiliwa na ukosefu wa soko la bidhaa zake:-

Je, ni kwa nini Serikali isikipatie kiwanda hiki hadhi ya *EPZ* ili kipate vivutio vitakavyoziwezesha kupata ushindani katika masoko ya nje?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha Nyuzi cha Tabora kilisajiliwa na Serikali tarehe 17 Agosti, 1977 kwa lengo la kusokota nyuzi za pamba ili kuuza kwenye viwanda vya nguo vya ndani ya nchi na ziada kuuzwa nje ya nchi. Kiwanda hiki kilianza kazi rasmi tarehe Mosi Januari, 1990 kikiwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni 6.22 kwa mwaka na kuajiri zaidi ya watu 1,000. Kiwanda hiki baadaye kilibinafsishwa kwa mtindo wa kuuza mali (*disposal of assets*) kupitia *Loans and Advances Realization Trust (LART)* hadi mwaka 2004 kilipopata mnunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnunuzi huyo *Ms Rajan Industries* alinunua kiwanda hicho kwa thamani ya dola milioni 1.5 ambapo baadaye pia alishindwa kuendesha kiwanda hicho. Mwezi Julai hadi Septemba, 2017 alijitokeza mwekezaji na kufunga mitambo midogo na kwa ajili ya kutengeneza kamba na vifungashio kwa mazao kama tumbaku na korosho. Aidha, ameanza mchakato wa kufufua kinu cha kuchambulia pamba cha Manonga ambacho Rajan ni mmiliki mbia na chama cha *Igembensabo Corporation Union* kwa asilimia 80 na mwenzake asilimia 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kiwanda kusajiliwa chini ya Mamlaka ya *EPZ* nawashauri wawekezaji wawasiliane na *EPZA*. Hata hivyo, ili kiwanda kiweze kusajiliwa chini ya mamlaka ya *EPZ* kinatakiwa kukidhi vigezo vifuatavyo:-

(i) Kuwa na uwekezaji mpya ikiwa ni pamoja na mashine;

- (ii) Kuwa na mtaji usiopungua dola za Kimarekani milioni 500;
- (iii) Kuwa na uhakika wa soko la nje;
- (iv) Kuuza asilimia 80 ya bidhaa zake nje ya nchi; na
- (v) Kuwa na uhakika wa kutoa ajira mpya zisizopungua 500 tofauti na ajira zilizopo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo nawashauri wawekezaji kupitia vigezo hivyo kutathmini na hatimaye kuwasilisha maombi ya kusajiliwa kwenye mamlaka ya EPZ.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, swali la nyongeza.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda napenda kuuliza maswali kama ifuatavyo.

Swali la kwanza; kiwanda cha Nyuzi cha Tabora kinazalisha vifa tiba ambavyo vinatangenezwa na pamba yetu inayolimwa hapa hapa nchini. Inazalisha vifaa kama pamba, *bandage* na nyuzi. Je, kwa nini Serikali kupitia MSD isimuunge mkono Mheshimiwa Rais maneno yake aliyotamka Mwanza na kununua vifaa tiba kwenye viwanda vyetu vya ndani hususan Tabora badala ya kuagiza nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kiwanda hicho kina uwezo wa kutengeneza sare za wanafunzi (*uniform*). Kwa nini sasa Serikali isitoe agizo, badala ya kununua sare za shule sehemu tofauti, sare za shule zinunuliwe kwenye viwanda vilivyopo nchini? Kwanza, ili kuchochea uchumi pia kupanua ajira hususan katika Mkoa wetu wa Tabora ambao kwa kweli hauna viwanda vya kutosha. Naamini vijana wetu wa Tabora

watapa ajira za kutosha kama sare zitanunuliwa katika kiwanda hicho cha nyuzi cha Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Bisahara na Uwekezaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni kweli kabisa iko haja ya kuunga mkono jitihada zinazofanywa na viwanda vyetu nchini ikiwemo vifaa tiba. Kimsingi viwanda hivi wakati vinaanzishwa vilikuwa na lengo la kusaidia kutoa malighafi katika viwanda vingine, lakini baada ya kuanza biashara huria na mikataba mbalimbali tuliyosaini Kimataifa, tumejikuta kwamba baadhi ya viwanda vyetu vinashindwa kuzalisha kutokana na wadau waliokuwa wanunue vifaa hivyo kutoka kwetu wanaamua kuagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni suala ambalo Wizara tayari tumeshaliona na tunalifanyia kazi. Vilevile kuimarisha masoko ya ndani na nje kwa hiyo kitengo chetu kitaendelea kufanyia kazi eneo hilo na hivyo niwaombe *MSD* waweze pia kufuatilia na kuweza kununua pamba na *bandage* zinazozalishwa katika kiwanda hiki nasi tutafutilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu *uniform*; naomba vilevile kuwashawishi wadau mbalimbali ambao wanatumia *uniform* zinazofanana na zile zinazozalishwa katika kiwanda hiki waweze kukipatia kipaumbele pamoja na viwanda vingine ambavyo viko humu nchini. Niwaombe pia Watanzania wote kupenda bidhaa zetu kwanza. Tufahamu kwamba viwanda hivi vinapokufa vinakosesha ajira kwa watu wetu na kwa kweli uzalendo ni kutumia mali zetu za ndani. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nichukue fursa hii kumshukuru na kumkaribisha Naibu wangu mpya. Napenda nitoe jibu la nyongeza kuhusu bidhaa tiba za Tabora *Textile*.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Mbunge Munde Tambwe kwa jinsi alivyopigana kufufua kiwanda hiki, watu wa Tabora watamkumbuka. Nataka nisisitize tamko la Mheshimiwa Rais, Wawekezaji wa Tabora *Textile* na wote mnaozalisha vifaa tiba nendeni sasa hivi *MSD*, msisubiri *MSD* iwafuate. Ni agizo la Rais kwamba *MSD* kwanza inunue vifaa vinavyotengenezwa hapa ndiyo maana ya kutenga bilioni 269 kwa ajili ya tiba. Kwa hiyo wote nendeni mkanunuae vifaa pale, mkauze vifaa vyenu pale kwa kufuata taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu hili la *uniform*, hili wazo la *uniform* namshukuru Mheshimiwa Tambwe, maamuzi yetu sasa tutaleta mapendekezo kwenu na watu wasituletee mambo ya *WTO*. Tukiweza kununua *uniform* kutoka kwenye viwanda vyetu vya nguo, tutaweza kuchochea viwanda vyetu kufanya kazi na kutumia pamba yetu badala ya kununua nguo zisizofaa zinazotoka nje ya nchi. Hiyo italeta kelele tunategemea ninyi Wabunge mtusaidie kutetea viwanda vyenu vya ndani. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 79

**Kuridhia Mkataba wa Marrakesh Treaty
wa Mwaka 2013**

MHE. AMINA S. MOLLEL aliuliza:-

Mkataba wa Kimataifa kuhusu haki za watu wenye ulemavu (*UNCRPD*) wa mwaka 2006 Ibara ya tisa (9) unazungumzia haki za watu wenye ulemavu kupata habari

kwa kuwa kumekuwa na changamoto za kisheria hususani katika nyaraka zenye hati miliki:-

Je, ni lini Serikali itaridhia Mkataba wa Kimataifa wa mwaka 2013 *Marrakesh Treaty* ambao unalenga kuondoa vikwazo mbalimbali vinavyozuia walemavu wasioona waweze kupata habari katika mifumo inayokidhi mahitaji yao?

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Saleh Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkataba wa Marrakesh ni mkataba wenye lengo la kuwawezesha watu wenye matatizo ya kuona, kupata nakala za maandishi yenye hati miliki na vifaa vya kuwasaidia kuweza kupata elimu kwa urahisi kwa kutumia vitabu, magazeti, burudani na shughuli mbalimbali za kijamii, hivyo kuwasaidia katika maisha yao ya kila siku na kuwawezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiuchumi na kuondoa umaskini hatimaye kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kupitia *COSOTA* ilisaini itifaki ya *Marrakesh* tarehe 28 Juni, 2013. Wizara inaandaa mapendekezo ya kuridhia Itifaki ya *Marrakesh* kulingana na taratibu zinavyoelekeza na hivi sasa inakusanya maoni ya wadau kuhusu mkataba huo. Baada ya kukamilika kwa hatua hiyo, waraka wa mapendekezo utawasilishwa Baraza la Mawaziri na hatimae kuletwa Bungeni kwa lengo la kuridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Wizara ni kuleta Itifaki ya *Marrakesh* Bungeni haraka iwezekanavyo mara baada ya kukamilisha taratibu zinazotakiwa kufuatwa ili kuridhia Mkataba wa Kimataifa. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Amina Mollel, swali la nyongeza.

MHE. AMINA S. MOLLEL: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru kwa majibu hayo yanayoonesha jitihada za Serikali katika kusaidia watu wenye ulemavu. Pamoja na hayo nina maswali mawili ya nyongeza. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kujua sasa (*time frame*) ni lini mchakato wa kukusanya maoni ya wadau utakamilika na kwa kuwa ni miaka minne sasa na wenzetu wa Kenya tayari wameshasaini mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kutokusainiwa kwa mkataba huu wa *Marrakesh* kumesababisha watu wenye ulemavu wasioona kushindwa kwenda na wakati na kuendelea kuwa maskini na hasa kutokana na kukosa fursa mbalimbali za kujiongezea kipato, fursa hizo ambazo zinapatikana kwenye maandishi zinazohusu maendeleo ya nchi lakini pia ulimwengu kwa jumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba majibu hayo.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mollel kwa jitihada kubwa anayoifanya lakini pia yeye mwenyewe atakuwa shahidi, Mheshimiwa Rais wetu amekuwa ni mdau mkuu namba moja katika masuala yanayohusu watu wenye ulemavu na ndiyo maana unaona hata kwenye Baraza tayari kuna watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo jambo hili tunalichukua kwa uzito mkubwa na tutahakikisha kwamba mapema iwezekanavyo baada tu ya kumaliza hili zoezi wanaloendelea nalo lipelekwe kwenye vikao vya wataalam na kikao cha Makatibu Wakuu na hatimaye liende kwenye

Baraza la Mawaziri. Mheshimiwa Waziri wangu amekuwa akilifuatilia sana suala hili na najua nadhani umeona hata anakuja kusesitiza kwamba tutafanyia kazi haraka iwezekanavyo ili watu wenye ulemavu wapate haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nikijibu swali la pili ni kwamba, tunatambua watakapoweza kupata machapisho ya aina mbalimbali bila vikwazo itawasaidia pia hata wao kuona namna ya kuweza kuondokana na umaskini. Kwa hiyo, naomba sana ajue kwamba suala hili tumelichukua kwa uzito mkubwa ikizingatiwa kwamba wote sisi ni walemavu watarajiwa. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 80

**Kurejesha Shamba la Malisho kwa
Halmashauri ya Maswa**

MHE. MASHIMBA M. NDAKI aliuliza:-

Shamba la malisho lililopo katika Kata ya Shishiyu Wilayani Maswa linamilikiwa na Serikali lakini halitumiki ipasavyo:-

Je, Serikali Kuu haioni haja ya kulirejesha shamba hilo kwa Halmashauri ya Wilaya ili lipangiwe matumizi mengine?

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo cha kupumzishia mifugo (*holding ground*) cha Shishiyu kina ukubwa wa hekta 4,144 na ni kati ya vituo 28 vilivyotengwa nchi nzima kwa mujibu wa Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 kwa ajili ya kukusanya na kupumzisha mifugo inayotoka minada mbalimbali kwa ajili ya uchunguzi wa magonjwa kabla ya kusafirisha mifugo hiyo kwenda katika viwanda vya kuchinja na kuchakata nyama au kusafirisha kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uwepo wa vituo vya kupumzishia mifugo ni hitaji la Kimataifa katika biashara ya mifugo. Zipo sheria mbalimbali za Kimataifa zinazolazimisha uwepo wa maeneo haya, yanayolenga utoaji huduma unaozingatia viwango ambazo zinasimamiwa na Shirika la Afya ya Wanyama ulimwenguni - OIE na makubaliano ya Kimataifa ya afya ya wanyama na mimea (*Sanitary and Phytosanitary (SPS)*) chini ya Shirika la biashara la Kimataifa (WTO).

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili pia hutumika kama kituo cha karantini kwa ajili ya kuchunguza magonjwa, hususan yale ya milipuko yanapojitokeza hasa kutokana na Kanda ya Ziwa kuwa na mifugo mingi na baadhi ya mikoa katika Kanda hii inapakana na nchi jirani hivyo ni rahisi ka magonjwa ya wanyama ya milipuko kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kuna mwingiliano mkubwa wa wanyama wafugwao na wanyama pori kutoka Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na Pori Tengefu la Maswa kutokana na umuhimu wa kituo hiki kwa ajili ya biashara ya mifugo ndani na nje ya nchi. Hivyo, siyo vema kubadilisha matumizi na madhumuni ya kuanzishwa kwa kituo hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, eneo hili litaendelea kubaki chini ya usimamizi wa Serikali Kuu kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili eneo hili liweze kutumiwa na wadau wote waliopo kwenye mnyororo wa kuongeza thamani (*value chain*) ya mifugo na mazao yake.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mashimba Ndaki, swali la nyongeza.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa shamba hili la Shishiu hakuna mifugo inayokusanywa pale na kwakuwa pia katika *masterplan* ya Waizara ya Mifugo wana lengo la kuzalisha mbegu na malisho kwa ajili ya mifugo ili kuweza kuboresha ufugaji wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuwa lengo la Wilaya ya Maswa sio kubadilisha lakini ni kuitumia kwaajili ya kuzalisha mbegu na malisho. Je, Serikali haioni umuhimu wa kufikiria upya uamuzi wake huu ili kwamba eneo hili lipewe kwa Wilaya sio kumilikisha ili waweze kutumia kwa ajili ya kuzalisha mbegu na malisho kwa ajili ya mifugo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa pia maeneo kama haya yako mengi nchini Mheshimiwa Naibu Waziri ametaja vituo 28 pia ziko Ranchi nyingi ambazo wala hazitumiki ipasavyo; je, Serikali inaonaje ikifanya vituo hivi pamoja na Ranchi kama vituo vya kujenga uwezo wafugaji wetu ili kwamba waweze kuzalisha mbegu na malisho ambayo ni changamoto kubwa kwenye nchi yetu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi kwa swali zuri kabisa la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa maeneo haya kama nilivyoeleza katika jibu la msingi bado unabaki palepale hasa ikizingatiwa ya kwamba tunakwenda katika kipindi cha Tanzania ya viwanda na eneo nyeti kabisa hili la viwanda vya uchakataji na mazao ya mifugo ndio hasa unaoangaliwa. Ninachoweza kumshauri Mheshimiwa

Mashimba Ndaki yeye na wenzake katika Halmashauri ya Maswa wanaweza kuandaa mpango mkakati na wakauwasilisha katika Wizara kwa ajili ya kutazamwa kama itawezekana kuweza kuandaa hati ya maridhiano kwa maana ya *memorandum of understanding* kuweza kufanya haya anayoyasema ya kuboresha bila ya kubadilisha lile lengo la msingi la kutumika kwa maeneo haya kwa ajili ya mifugo na kuongeza thamani ya mifugo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili hili la *Ranch*, naomba nimwambie Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki na Waheshimiwa Wabunge wote, katika *masterplan* yetu ambayo inaendelea kuandaliwa ni kwamba maeneo haya tunawapa umuhimu mkubwa sana na shirika letu la Ranchi za Taifa hivi sasa tuna mpango mkubwa wa kulihuisha na lina mpango mzuri wa kuhakikisha kwamba Ranchi zetu zinakwenda kusaidia kuinua tasnia hii ya huduma za mifugo na hatimaye kuleta kipato kikubwa kwa nchi yetu. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, sasa aulize swali lake.

Na. 81

Fidia kwa Uharibifu Unaofanywa na Tembo

MHE. JOSEPH L. HAULE aliuliza:-

Wanyama hasa Tembo wamekuwa wakiharibu sana mazao ya wananchi kwa fidia ndogo sana ya Sh. 20,000 kwa heka na hii hupunguza ushiriki wa wananchi katika kuzuia ujangili ndani ya Hifadhi:-

Je, Serikali imejipangaje kukaa vizuri na wananchi wa vijiji vinavyopakana na Hifadhi ili kuwa na ushirikiano katika kuzuia ujangili?

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Leonard Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa maisha ya binadamu, mazao na mifugo imeweka utaratibu wa kulipa kifuta jasho na machozi kwa uharibifu unaosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali kupitia halmashauri zake za Wilaya na taasisi zilizo chini ya Wizara ya maliasili na utalii imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kuelimisha jamii kuhusu uhifadhi na sheria zake ikwemo za kufukuza wanyamapori mara inapotokea wameingia katika makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau wa uhifadhi kutoa elimu kwa wananchi juu ya kutumia pilipili na ufugaji wa nyuki kandokando ya mashamba ili kuzuia wanyama hususani tembo kuingia mashambani. Elimu hii ilianza kutolewa katika vijiji vinavyopakana na Hifadhi ya Taifa ya Mikumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ili kufanya zoezi hili kuwa endelevu vikundi 23 vilisaidiwa kuanzisha Mfuko wa Kuweka na Kukopa na fedha wanayopata isaidie kununua baadhi ya vifaa vinavyotumika kuzuia wanyama kuingia mashambani pamoja na kuviwezesha vikundi kiuchumi ili visaidiwe katika kuzuia ujangili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya vikundi vilivyoanzishwa, kumi vimepata usajili toka halmashauri ya wilaya na vingine 13 bado vinaendelea kushughulikia usajili wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imetoa mizinga 180 kwa wananchi wa Kijiji cha Maharaka ikiwa ni kuunga mkono

juhudi zinazofanywa na wananchi katika kutekeleza maazimio ya kutumia pilipili na mizinga ya nyuki kuzuia tembo kuingia katika mashamba yao. Vilevile elimu inaendelea kutolewa katika Vijiji vya Mikumi, Mkata na Ihombwe ili nao kutumia mfumo wa pilipili katika mashamba yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzishauri Halmashauri za Wilaya kuajiri Askari Wanyamapori na kuwapatia vitendea kazi ili waweze kusaidia wananchi pale kunapojitokeza tatizo la uharibifu wa mazao na mifugo kuvamiwa na wanyamapori.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joseph Haule, swali la nyongeza.

MHE. JOSEPH L. HAULE: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nisikitishwe sana na majibu haya ya Serikali ambayo wamekuwa wakiyajibu mara kwa mara, kiukweli yanakatisha sana tamaa. Kwa sasa huu utaratibu wa Serikali wanaosema ni kifuta jasho kwa wananchi ambao wanakuwa wameuliwa na tembo au mazao yameharibiwa kiukweli haina uhalisia na haileti haki kwa wananchi ambao wamekaa kwenye mazingira hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii yote inatokana na sheria ya wanyamapori ambayo imeonekana kuwa na usumbufu na upungufu mkubwa sana. Ni lini Serikali itaileta sheria hii hapa Bungeni ili iweze kubadilishwa ili iweze kwenda na uhalisiana kurudisha fidia na hili neno la kifuta jasho libadilishwe iwe fidia iliyokuwa imetathiminiwa kutokana na matatizo ambayo wamepata wananchi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili juzi kuamkia jana katika Kijiji cha Kikwaraza pale Mikumi ambapo Mbunge wa Mikumi anaishi, simba alivamia zizi la mfugaji anaitwa Agrey Raphael na kuuwa ng'ombe mmoja pamoja na kujeruhi ng'ombe wawili. Sasa hayo matatizo na changamoto kama hizi zimekuwa nyingi sana kule Mikumi kwenye Kata kama Mikumi, Luhembe, Kidodi, Kilangali, pamoja na maeneo ya Mhenda. Je, Naibu Waziri yuko tayari kuambatana na mimi

kuelekea kule mikumi ili akasilize changamoto nyingi za wananchi ambao wamekuwa na kilio cha muda mrefu kutokana na matatizo kama haya ya wanyamapori *kabla hawajaamua kuchukua sheria zao mikononi kwa kutumia silaha za jadi? Ahsante. (Makofi) [Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Haule hayo maneno yako ya mwisho hapo yaondolewe kabisa, habari ya wananchi kujichukulia sheria mkononi haipo. Kwa hiyo, yaondolewe na kwenye *hansard* naagiza katibu. Karibu Naibu Waziri...

Jamani acheni kelele Wabunge hamsomi sheria, siyo wote tuliosoma, kwa hiyo muwe mnatulia tukiwapa haya maneno, muwe mnatulia tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba....

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Matiko, ukitulia kidogo tutakwenda vizuri humu ndani, tafadhali.

Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea.

NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu iko sasa hivi inafanya kuiisha tunapitia upya sera na sheria pamoja na taratibu mbalimbali ambazo zinatumika katika kutoa hiki kifuta jasho na machozi, ni hivi karibuni tu tutaileta hii sheria hapa ndani Bungeni ili Bunge lako Tukufu liweze kushauri na liweze kuipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la kuambatana naye, nataka nimwambie tu niko tayari mara baada ya shughuli za Bunge kukamilika, nitaambatana naye kwenda kuangalia maeneo hayo yote yalioathirika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu, nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo hapa mezani.

Tutaanza na tangazo la wageni kwanza tutaanza na walioko jukwaa la Spika ni hawa ni wageni wangu ambao ni wageni saba viongozi wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Songwe na Mbeya wakiongozwa na Katibu wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mbeya Ndugu William Mkambaku na pia Katibu wa CCM Mkoa wa Songwe Bi. Mercy Mollel. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni mabalimbali wa Waheshimiwa Wabunge tunaanza na wageni 60 wa Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni wanakwaya kutoka Usharika wa KKKT Kijitonyama Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Mkoa wa Dar es Salaam. Naona wamekwisha kusimama hapa.

Hii kwaya ya Uinjilisti watu wengi wanawafamu kwa sababu wameimba nyimbo nyingi sana na taarifa nilizonazo wataimba leo kwenye *chapel* kwenye taarifa ambayo nitaitoa hapa, kuna ibada leo, mnakaribishwa Waheshimiwa Wabunge kwenda, nitawasomea taarifa lakini kwaya hii itaimba kwenye hiyo ibada. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa ambaye ni Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na hawa ni watendaji Wakuu wa Wizara na Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* wakiongozwa na Mhandisi Angelina Madete, ambaye ni Kaimu Katibu Mkuu Mwasiliano. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 105 wa Waheshimiwa Wabunge Wilfred Lwakatare na Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanakwaya wa *Prophetic Singers* kutoka Mkoa wa Dar es Salaam. Sijajua wamekaa upande upi lakini mnakaribishwa sana.

Tunao pia wageni 41 wa Waheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Ritta Kabati ambao ni wanamaombi kutoka Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni nane wa Mheshimiwa Shally Raymond ambao ni Wahadhiri na wanafunzi kutoka Chuo cha St. Johns cha Mkoani Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Frank Mazengo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Klimo, Mifugo na Maji ambao ni watendaji kutoka *Ox Farm* Tanzania wakiongozwa na Ndugu Cassa Bull. Sijui wako upande gani kutoka *Ox Farm, do we have guest from Ox Farm in the House*, nadhani na wao pengine hawakupata nafasi ya kuingia karibuni sana wageni wetu mliokuja kutembelea Bunge siku ya leo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kupitia Kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye ni Waziri wa Nchi, ofisi ya Waziri Mkuu anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka maeneo yanayolima pamba kwamba leo saa tisa na nusu alasiri kutakuwa na kikao cha pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaotoka maeneo yanayolima pamba mnaalikwa katika kikao hicho.

Tangazo lingine Waheshimia Wabunge, ni la ibada na linatoka kwa Mwenyekiti wa ibada *Chapel* ya Bunge na huyu ni Mheshimiwa Anna Lupembe anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo siku ya Jumanne tareha 14 Novemba saa saba mchana mara baaada ya kusitisha shughuli za Bunge kutakuwa na ibada ambayo itafanyika katika *Chapel* iliyoko ukumbi wa Msekwa. Aidha, Mtumishi wa Mungu Mgisa Ntebe kutoka Dar es Salaam atahuduma katika ibada hiyo. Kwa hiyo mnakaribishwa sana kwenye ibada Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo matangazo tuliyonayo. Kwa hiyo, tutaendelea na ratiba yetu.

MWONGOZO WA SPIKA

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Bilago.

MHE. KASUKU S. BILAGO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nasimama kwa kanuni ya 64(7) kuhusu jambo liliotokea mapema leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wangu unahusiana na utaratibu wa maswali; kumekuwa na sintofahamu ya namna ambavyo maswali yanatakiwa kuulizwa hapa Bungeni na aidha, kiti chako kimekuwa kikielekeza ama kufupisha ama kurefusha, sijui iweje ili swali liweze kuonekana ni swali. Sasa tunapata wakati mgumu, Mbunge anasimama kuuliza swali ama linaonekana limerefuka mno sasa tupate utaratibu ni swali linatakiwa liwe fupi kiasi gani au liwe refu kiasi gani ili kiti kiridhike na kitoef nafasi ya kuuliza swali hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kiti hichohicho kiliwahi kupongeza Mbunge Mheshimiwa Mkuchika akiuliza swali, akijenga hoja Spika akasema hivyo ndivyo Wabunge wanavyotakiwa kuuliza maswali ili wananchi wao waweze kuelewa kweli wamewakilishwa vizuri. Sasa humu ndani mtu anauliza swali nimesikitika sana leo kwamba swali la Mheshimiwa Waitara lililokuwa linahoji namna ambavyo wafanyakazi wanahamishwa bila kulipwa na maelekezo ya Rais yametolewa anayehamisha mtumishi awe amemlipa na Wakurugenzi wanaendelea kuwahamisha watu kuwalipa swali hilo limefutwa kwamba sio swali kwa sababu limerefuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kiti chako kituelekeze, utaratibu wa swali ni upi na ni kanuni ipi inayosema hili swali ni refu na hili swali ni fupi? Naomba Mwongozo wako. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan Kiwanga.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami nimesimama kwa kanuni ya 68(7) nikiomba mwongozo wako jambo lililotokea hapa Bungeni mapema na limetokea kwenye kiti chako ukiniambia kwamba jana nilipewa vidonge vyangu na sikuwepo Bungeni.

Ni kweli kabisa, lakini nimefuatilia kwa sababu nilikuwa kwenye mazingira ya Bunge nilikuwa naongea na wapiga kura wa Jimbo la Mlimba mimi wananitambua kama Mbunge wao na aliyekuwa ananipa vidonge vyangu ni Mbunge wa Viti maalum ambaye ni Waziri wa Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wangu wamesikitika sana kwa sababu mpaka leo hii ninavyokwambia nilivyokuwa nachangia mpango nilikuwa nawakilisha wananchi wa Mlimba na Watanzania kwa ujumla wao na mpaka leo ninavyozungumza hakuna hela ya *basket fund* iliyoenda katika halmashauri ya Kilombero ambapo mle wanatoa hela itakayomsaidia mama na mtoto ili kuepusha vifo vya akinamama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninapokuwa natoa maelezo yangu kuhusu mpango ili Serikali ijue ichukue ione namna gani matatizo wanayopata wananchi kwa bajeti ijayo nakuja napewa vidonge. Vidonge sikupewa mimi wamepewa wananchi wa Jimbo la Mlimba, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Mlimba niliopigiwa kura wala sijateuliwa. Sasa tunapokuja hapa tunakuja kama mwakilishi wa mwananchi waliopiga kura sikuteuliwa mimi na mtu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako ni namna gani mimi Mbunge naweza kuchangia mpango halafu Waziri mimi sijamtaja anakuja, halafu ananipa vidonge! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui vidonge gani, *panadol*, *quinine...* (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa umeshaeleweka naomba ukae.

MHE. SUSAN L. KIWANGA: *(Aliendelea kuongea bila kipaza sauti).*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Susan naomba ukae umeshaeleweka. Mheshimiwa Waitara. *(Makofi)*

MHE. MWITA M. WAITARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Natumia Kanuni ya 68(7), naomba mwongozo wako. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali namba 68 alizungumzia fao la kujitoa lakini alipoulizwa akasema mchakato wa fao la kujitoa unaendelea kufanyika na maamuzi yake hayajafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo ninaouomba ni kwamba jambo hili limekuwa na mkanganyiko mkubwa sana. Wako watu waliostaafu kazi hawajapewa mafao yao. Wako watumishi ambao wanafanya kazi kwa mkataba, mkataba ukiisha anaambiwa usubiri miaka 55. Wako watu ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu wangetaka waache kazi wapate mafao yao waanzishe shughuli mbalimbali za maendeleo kulingana na kipato waweze kujikimu. Pia wako watu ambao kimsingi ni wagonjwa na wanahitaji wapate mafao yao, wapate matibabu na wengine wasomeshe watoto wao. Hilo zoezi limeshindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka niombe mwongozo kwa sababu kama Naibu Waziri anasema kwamba jambo hilo lipo kwenye mchakato na Wabunge wanaulizwa na wananchi wao kwamba ni kwa nini hawapewi fedha zao wanaambiwa Serikali imeelekeza mpaka ufikishe miaka 55. Hiyo sheria hatujawahi kuiona, mjadala huo haujawahi kufanyika, jambo hilo halijawahi kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kwa sababu watu hawa waendeleo

kupata haki zao. Kama kuna mchakato; kauli ya Serikali itoke wapate haki zao, mafao yao/wapewe fedha yao wafanye shughuli ambazo wanaweza kujiingizia kipato. Mchakato unapokamilika Watanzania kwa ujumla wao watapata maelezo mengine. Naomba mwongozo wako katika jambo hili muhimu sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba mwongozo kutokana na kanuni ya 68(7) kutokana na swali ambalo ameliuliza kaka yangu Profesa Jay linalohusiana na vijiji vinavyopakana na hifadhi. Asili ya Wilaya ya Ulanga na Malinyi ni milima. Maeneo ambayo ni tambarare yote ni hifadhi ambapo eneo kubwa ni Hifadhi ya Bonde la Mto Kilombero ambapo ndiyo tunalima mchele huu mnaokula.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Serikali hii imeingia madarakani wana vita ya kuwatoa watu kutokana na maeneo haya ambayo yanaitwa hifadhi. Kuna sensa ambayo tunafanya kila baada ya miaka kumi inatambua kuwa raia wetu wa Tanzania na wapiga kura sio matasa, wanazaliana lakini ardhi haiongezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tulikubaliana na Waziri Mkuu, Rais Magufuli aliahidi hawa watu watahalalishiwa haya maeneo, mipaka itawekwa upya ili walime na kufanya vitu vinginevyo. Kinachofanyika sasa hivi ni tofauti, Waziri tangu aingine madarakani yeye ana vita na wapiga kura wetu anawaondoa kwenye haya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukikaa mjini mnatubomolea, mnasema tumejenga kwenye hifadhi ya barabara, tukikaa kwenye vijijiwe mnasema *mission town* mnatukamata mnasema wazururaji. Tukirudi vijijini kulima mnasema tunalima kwenye hifadhi. Sisi hatujapigiwa kura na miti, hatujapigiwa kura na barabara. Tumewaahidi wananchi wetu tutawaletea maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako kuwa Serikali yetu hii imeingia madarakani kupiga vita watu au kuwasaidia watu? *(Makofi/Kicheko)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Nimeombwa miongozo kadhaa na Waheshimiwa Wabunge hapa.

Mwongozo wa kwanza umeombwa na Mheshimiwa Kasuku Bilago ambao ameuliza kuhusu namna ya kuuliza maswali Bungeni na akaeleza kuhusu namna Mheshimiwa Waitara alivyokuwa anajenga hoja yake na kuambiwa na kiti kwamba afupishe, halafu baadaye kuambiwa hawezi tena kuuliza swali. Mwongozo wake anaouliza, pamoja na maelezo marefu aliyoyatoa anataka kujua utaratibu wa kuuliza swali ni upi na unajuaje hili swali ni refu ama fupi?

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu zinatutajia muda wa kuuliza maswali na kwa sababu hiyo mtu anayekaa hapa mbele hutakiwa kuangalia maswali yaliyopangwa na Mheshimiwa Spika yako mangapi na kila swali litatumia muda gani. Ninyi kwa sababu wale ambao wana maswali huwa wanajua, majibu ya kutoka Wizarani ni marefu kiasi gani kuhusu kila swali. Kwa hiyo, kila swali linapangiwa muda wake, mtu aliyekaa hapa mbele huangalia ni kiasi gani cha muda anao kuhusu swali husika.

Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania kwa lengo la kuweka muundo wa kisheria wa uanzishwaji, utawala na uendeshaji wa shirika la umma la mawasiliano litakalojulikana kama Shirika la Mawasiliano Tanzania, kuwezesha shirika la mawasiliano kufanya kazi, pamoja na mambo mengine, kuhusiana na usimamizi wa huduma za mawasiliano na miundombinu ya kimkakati ya mawasiliano kwa lengo la kuwa na shirika bora na salama la mawasiliano lenye kuwezesha uchumi na biashara endelevu.

Muswada huu umegawanyika katika sehemu Sita.

Sehemu ya Kwanza inahusika na masharti ya Awali ambapo vifungu vinavyohusu Jina la Sheria, kuanza kutumika kwa Sheria, matumizi na tafsiri ya maneno yaliyotumika ndani ya Muswada.

Sehemu ya Pili inaainisha masharti kuhusu Uanzishwaji na majukumu ya Shirika, Muundo wa Bodi majukumu na wajibu wake. Sehemu hii vilevile inaweka masharti kuhusu mgogano wa kimaslahi kwa wa wakurugenzi wa Bodi na watumishi wa Shirika. Kwa kuongezea, sehemu hii inatoa mamlaka ya uteuzi wa Kamati za Bodi na ukasimishaji wa majukumu ya Bodi.

Sehemu ya Tatu inaainisha masharti kuhusu uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu ambaye atakua ndiye Afisa Mtendaji Mkuu wa Shirika, Sehemu hii pia inaweka masharti kuhusu vigezo vya upatikanaji wa Mkurugenzi Mkuu na na sababu za kutengua uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu. Sehemu hii pia inatamka mamlaka ya Waziri kwa Bodi ya Wakurugenzi na kwa shirika kwa ujumla.

Kwa kuongezea, Sehemu hii inaainisha majukumu ya Mkurugenzi Mkuu kwa madhumuni ya kutimiza majukumu yake kama Afisa Mtendaji Mkuu.

Sehemu ya Nne inapendekeza kuweka masharti kuhusiana na utaratibu wa usimamizi wa miundombinu ya kimkakati ya mawasiliano na ufikiaji wa miundombinu hiyo kwa waendeshaji wake.

Sehemu ya Tano inaweka masharti ya fedha ya Shirika. Inajumuisha masuala yote yahasuyo vyanzo vya fedha, makadirio ya mwaka, bajeti na masharti mengine kuhusu vitabu vya hesabu.

Sehemu ya Sita inahusu masharti mbalimbali ambamo Sheria ya Shirika la Kampuni ya Simu Tanzania inafutwa. Vilevile, Sehemu hii inampa mamlaka Waziri kutengeneza Kanuni ili kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria. Aidha sehemu hii inahusu masharti ya Mpito na yatokanayo na matokeo ya kuvunjwa kwa Shirika la Kampuni ya Simu Tanzania. Sehemu hii inaelezea uhamishaji wa mali, madeni na watumishi kutoka Shirika la Kampuni ya Simu Tanzania kwenda Shirika la Simu Tanzania linaloundwa na sheria hii.

Dodoma,
..... 2017

MAKAME M. MBARAWA

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. PROF. MAKAME M.
MBARAWA , THE MINISTER FOR WORKS, TRANSPORT AND COMMUNICATIONS
AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE TANZANIA
TELECOMMUNICATIONS CORPORATION ACT, 2017**

Made under S.O. 86(10)(b)

A Bill entitled the "Tanzania Telecommunications Corporation Act, 2017" is amended as follows:

- A:** In Clause 3 by deleting the words "as the Government may, by notice published in the Gazette, proclaim" appearing in the definitions of the term "strategic telecommunications infrastructures".
- B:** In Clause 4(2) by inserting the words "Subject to this Act or any other written law," at the beginning of paragraph (c).
- C:** In Clause 6(1), by-
- (a) deleting paragraph (b) and substituting for it the following:
"(b) in consultation with the Minister, plan, build, operate and maintain the strategic telecommunications infrastructure as determined by the Government;"
 - (b) deleting the abbreviation "ICT" wherever it appears in the subsection and substituting for it the following "Information and Communications Technology (ICT)"
 - (c) adding the word "and" immediately after the "semi colon" appearing in paragraph (k).
- D:** In Clause 7, by-
- (a) deleting the word "or" appearing in subclause (2) and substituting for it the word "of";
 - (b) deleting the reference to subsection (2) (b) appearing in subclause (3) and substituting for it the reference to subsection (2) (a);
 - (c) deleting the words " fees and such" appearing in subclause (5) and substituting for them the words "allowances and".

- E:** In Clause 8-
- (a) by deleting the marginal notes and substituting for them the following:
"Duties of Board"
 - (b) in subclause (1) by deleting the word "undertake" and substituting for it the word "oversee";
 - (c) by deleting subclause (2);
 - (d) by renumbering subclause (3) as subclause (2);
 - (e) in subclause (2) as renumbered, by-
 - (i) deleting the words "subsections (1) and (2)" appearing in the opening words of the subclause and substituting for them the words "subsection (1)";
 - (ii) deleting the word "invest" appearing in paragraph (b).
- F:** By deleting Clause 11.
- G:** In Clause 13-
- (a) by deleting the words "at it may specify, delegate to any committee of the Board or to any employee of the Board some of its functions," appearing in subclause (1) and substituting for them the words "as it may specify, delegate to any Committee of the Board or to the Director General some of the functions of the Corporation, its";
 - (b) in subclause (3) by-
 - (i) adding the words "its powers of" at the end of the opening phrase of the subclause;
 - (ii) deleting the words "its powers of" appearing in paragraph (a);
 - (iii) deleting the words "approve the" appearing in paragraphs (b) and (c) and substituting for them the words "approval of";
 - (iv) deleting paragraph (d) and substituting for it the following:
"(d) exercise of disciplinary authority over the staff of the Corporation."
- H:** In Clause 14 by deleting subclause (3) and substituting for it the following:

"(3) Upon the Corporation becoming aware of any conflict of interest, a determination shall be made by a competent organ of the Corporation as to whether that conflict is likely to interfere with the proper and effective performance of the functions of the Corporation, and the person against whom a conflict of interest is determined shall not vote or partake on the matter for which the conflict of interest relates."

- I:** In Clause 15(3) by deleting the word "of" appearing in paragraph (a).
- J:** In Clause 16(2) by deleting paragraph (c) and substituting for it the following:
- "(c) on behalf of the Corporation, carry out any trade, business or activity and do anything of any nature which can, in the opinion of the Board, be advantageous to the Corporation; and".
- K:** In Clause 18 by deleting the words "of senior officers of the Board his functions conferred or impose" and substituting for them the words "senior officers of the Corporations his duties conferred or imposed".
- L:** In Clause 20 by deleting the words "procedure for" appearing in the marginal notes and substituting for them the word "prudent".
- M:** In Clause 22(1) by adding the word "and" at the end paragraph (f).
- N:** By redesignated the contents of clause 24(1) as contents of clause 24.
- O:** By adding immediately after clause 26 the following new title:
- "PART VII
TRANSITIONAL AND SAVINGS PROVISIONS"
- P:** By deleting clause 27 and substituting for it the following:
- "Savings of instruments and administrative directives"
- 27.** Notwithstanding the repeal of the Tanzania Telecommunications Company Incorporation Act, and the subsequent winding up of the defunct Company, any license, certificate and any other administrative order, circular, instrument, directive and guideline

made, given or issued to or by the defunct Company under or in pursuance of the provisions of respective Acts which are in force on the commencement of this Act, shall be deemed to have been made, given or issued under or in pursuance of the provisions of this Act, and shall remain in force until revoked, replaced or rescinded by subsidiary legislation or another license, certificate or any other administrative order, directives or instructions made under this Act.

- Q:** In Clause 28 by deleting the word "former" appearing in subclause (1).
- R:** By deleting clause 29.
- T:** In Clause 30 by deleting the word "former" appearing in subclause (1).
- Y:** In Clause 31 by deleting the word "Ltd" appearing in subclause (2).
- U:** By renumbering Clauses 12 to 33 as Clauses 11 to 31 respectively.
- V:** In the Schedule-
- (a) in item 1 by adding the words "for another term" at the end of sub item (1);
 - (b) in item 4 by-
 - (i) inserting the word "by" between the words "upon" and "the" appearing in sub item (1);
 - (ii) deleting the word "my" appearing sub item (2) and substituting for the word "by";
 - (c) in item 7(2) by deleting the word "are" and substituting for it the word "as".

NAIBU SPIKA: Tutaendelea na utaratibu wetu. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. Mheshimiwa Profesa Norman Sigala.

MHE. NORMAN A. SIGALLA KING – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza taarifa yangu iingie kama ilivyo kwenye *Hansard*. Yako maeneo ambayo sitayawasilisha kwa sababu sehemu kubwa ya mapendekezo ya Kamati yalizingatiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati Kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania, 2017 (*The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati kwanza inatoa pongezi kwa Serikali kwa kuimarisha sekta ya mawasiliano, hasa kwa kuhakikisha kuwa Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) inabadili jina na kuwa Shirika la Umma la Mawasiliano. Muswada huu ni ishara ya kazi kubwa ambayo inaendelea kufanywa, ili kuimarisha sekta ya mawasiliano nchini na kulinda usalama wa nchi, kukuza uchumi na kutoa huduma bora kwa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya 8(7)(1)(b) cha Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inazipa Kamati za Bunge za kissekta, ikiwemo Kamati ya Miundombinu, jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba iliyo chini ya Wizara inayoisimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu uliwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 24 Oktoba, 2017 na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, ambapo pamoja na maelezo mengine alieleza vizuri manufaa mbalimbali yatakayotokana na kupitishwa kwa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya tano mpaka ya tisa inaelezea historia ya *TTCL*, ambayo naomba iingie kwenye *Hansard* kama ilivyo kwa sababu, historia ni historia huwa haibadiliki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya Kumi; Muswada huu unakusudia kutunga Sheria mpya ya Shirika la Mawasiliano ambalo litajiendesha kibiashara na kuimarisha mawasiliano nchini. Shirika hili la mawasiliano litaendeleza shughuli za kibiashara zilizokuwa zinaendeshwa na Kampuni ya Mawasiliano Tanzania (*TTCL*) na kuongeza wigo wa shughuli zake katika sekta za biashara ya mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu una lengo la Kutunga Sheria ambayo inaweka masharti kuhusu uanzishwaji wa Shirika la Mawasiliano ya Simu, usimamizi wa miundombinu ya mawasiliano na ya kimkakati, uwezekano wa kibiashara na kiuchumi wa huduma za mawasiliano ya simu pamoja na kutunga masharti mengine yanayohusiana na hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya masuala muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni haya yafuatayo:-

Kuweka utaratibu utakaowezesha *TTCL* kutekeleza majukumu yake kama shirika la umma. Kuweka jukumu la ujenzi, usimamizi na uendeshaji wa miundombinu ya kimsingi ya Taifa. Kuweka mazingira ya kinga ya mali(*assets*) na miundombinu muhimu ya mawasiliano ya shirika. Kuanzishwa kwa shirika na kuanisha uongozi wa shirika. Kuainisha vyanzo vya mapato ya mtaji ya washirika na sheria kutumika pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati. Kufuatia uchambuzi uliofanywa na Kamati, marekebisho mbalimbali ya kisarufi na kimantiki yalifanyika ambapo kwa kiasi kikubwa Serikali imezingatia ushauri huo na kufanya marekebisho ya makosa hayo kupitia Jedwali lake la Marekebisho (*Schedule of Amendments*).

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maoni na ushauri wa Kamati:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Kwanza, inaainisha masharti ya awali, jina la sheria, tarehe ya kwanza kutumika kwa sheria na tafsiri ya maneno yaliyotumika. Katika sehemu hii na Kamati haikuwa na marekebisho yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili, naomba niende Aya ya 15(c). Kifungu cha 7(7) pia, ili kumpunguzia Waziri madaraka ya kufanya maamuzi pasipokupata ushauri angalao wa Mwenyekiti wa Bodi; kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza maneno yafuatayo, *upon consultation with the Chairman* katikati ya maneno *Ministerna may*; hivyo, kifungu hicho kisomeke kuwa, *"The Minister upon consultation with the Chairman may by order publish in the gazette..."* halafu itaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 8(1); Kamati inashauri kifungu hiki kidogo kifutwe na kuandikwa kama ifuatavyo:-

"The Board shall oversee and supervise the management in the performance of the functions of the Corporation and shall ensure adherence to the governing laws and procedures.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo hili linatokana na ukweli kwamba, jukumu la Bodi ni kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa kazi za shirika na sio kutekeleza majukumu hayo ya shirika, kama ambavyo Kifungu cha Muswada kilimaanisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu, ambayo kwenye kitabu inaonekana ni 2.3, Sehemu ya Tatu. Kifungu cha 15(3), ili kuepuka uteuzi wa mtu asiye na uwezo wa kufikisha malengo yanayotarajiwa, Kamati inashauri kuongeza kipengele kidogo cha (c) ambacho kitasomeka: *"has a satisfactory performance in relevant field."*

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya 17(f) aidha, kati ya aya ya nne, ili kuepuka matumizi mabaya ya fedha za umma na ili kuweka vigezo vya bodi kuruhusiwa kwenda nje ya nchi, Kamati inashauri kuongeza aya ndogo mpya ya pili ambayo itasomeka kama ifuatavyo:

" Notwithstanding the provisions of the subparagraph (1) the Board shall conduct its ordinary meetings within Tanzania except where the circumstances require otherwise the Board shall pay official visits and business undertakings abroad."

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu aya ya 18, Maoni ya Jumla ya Kamati; pamoja na uchambuzi na marekebisho mbalimbali ya Vifungu vya Sheria hii, Kamati inasisitiza Serikali katika mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Shirika litakaloanzishwa liondokane na mfumo wa utendaji wa urasimu unaofanywa na taasisi zingine za Kiserikali zinazotoa huduma na ambazo si za kibiashara. Katika kulitekeleza hilo uteuzi wa wajumbe ufuatae weledi wa kibiashara; *(Makofi)*

(b) Mtendaji Mkuu wa Mkuu wa shirika pamoja na wasaidizi wake wawe ni watu wenye historia ya kufanya vizuri kwenye taasisi walizopata kuzisimamia.

(c) Ili shirika liweze kufanya vizuri ni vyema Bodi na Mtendaji Mkuu wa Shirika wapewe madaraka kamili ili watumie uwezo wao kuleta maendeleo ya shirika.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii, walioshughulikia Muswada huu, kama ifuatavyo:-

Profesa Norman Adamson Sigalla King Mwenyekiti,
Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso Makamu Mwenyekiti...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa, hao usiwasome, waingize tu kwenye *Hansard* kama ulivyosema, halafu umalize. Ahsante.

MHE. NORMAN A. SIGALLA KING – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante. napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen N. Kagaigai, kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na Mkurugenzi Msaidizi ndugu Dickson A. Bisile; Mkurugenzi Msaidizi Mshauri wa Sheria, ndugu Mossy Lukuvi; Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John na Ndugu Richard Masuke.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inatoa shukrani kwa Washauri wa Sheria, Ndugu Evelyne Shibandiko na Ndugu Mariam Mbaruku pamoja na msaidizi wa Kamati Ndugu Catherine Kitutu kwa kuihudumia Kamati hadi kukamilisha kazi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa; Manaibu Waziri, Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Nditiye na Mheshimiwa Elias Kwandikwa, kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati inamshukuru Katibu Mkuu Dkt. Maria Sasabo akisaidiana na Naibu Katibu Mkuu Mhandisi Angelina Madete pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
MIUNDOMBINU KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA UWAKALA
WA MELI TANZANIA WA MWAKA 2017 (*THE NATIONAL
SHIPPING AGENCIES CORPORATION BILL, 2017*)
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania ya Mwaka 2017 (*The National Shipping Agencies Bill, 2017*).

2. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 30 Oktoba, 2017 Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, (Mb) aliwasilisha Muswada huu mbele ya Kamati, ambapo pamoja na maelezo mengine, alijulisha Kamati manufaa mbalimbali yatakayotokana na kupitishwa kwa Sheria hii.

3. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 84 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ilitoa fursa kwa wadau mbalimbali kushiriki katika kutoa maoni kuhusiana na maudhui ya muswada huu. Wadau walipata mwaliko kupitia matangazo yaliyowekwa katika tovuti ya Bunge, vyombo mbalimbali vya habari na mwaliko wa barua.

4. **Mheshimiwa Spika**, Zoezi la kupokea maoni ya wadau lilifanyika katika ukumbi wa Msekwa siku ya tarehe 31 Oktoba, 2017 ambapo wadau mbalimbali kutoka katika Taasisi za Serikali na binafsi waliwasilisha maoni yao. Kwa namna ya pekee naomba kuwatambua baadhi ya wadau hao kama ifuatavyo:-

i) Tanzania Shipping Agency Association (TASAA);

ii) Tanzania Private Sector Foundation (TPSF);

iii) Tanzania Freight Forwarder Association (TAFFA);iv)

Mamlaka ya udhibiti na usimamamiaji wa usafiri wa nchi kavu na majini (SUMATRA);

- v) Chuo cha mabaharia Tanzania (TMI);
- vi) Chuo cha usafirishaji Tanzania (NIT);
- vii) *Chartered Institute of Logistics Tanzania (CILT);na*
- viii) *SUMATRA Consumer Consultative Council (SUMATRA CCC).*

1.1 Historia ya Uwakala wa Meli Tanzania (*Shipping Agencies Tanzania*)

5. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanzishwa kwa Kampuni ya Taifa ya Wakala wa Meli (*National Shipping Agencies Company Ltd- NASACO*), shughuli za uwakala wa meli zikitekelezwa na Shirika la Biashara la Taifa (*State Trading Corporation - STC*). Mwaka 1973, Serikali ilianzisha NASACO chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212. Lengo kuu lilikuwa ni kuhakikisha kuwa shughuli zote za uwakala wa meli nchini zinafanywa na chombo kimoja ili kusimamia vema wamiliki wa meli wafanyapo shughuli za usafirishaji wa mizigo kwa kutumia meli. NASACO ilipewa mamlaka kutekeleza shughuli zote za uwakala wa meli kwa bandari za Tanzania Bara.

6. **Mheshimiwa Spika**, Kupitia NASACO, Serikali iliweza kusimamia vema shughuli za uwakala wa meli na kudhibiti usahihi wa taarifa kwenye nyaraka na kuhakiki shehena hivyo, kudhibiti magendo, utorohaji wa nyara za Serikali na maliasili ya nchi.

7. **Mheshimiwa Spika**, Kwa sasa wamiliki wa meli wanatumia makampuni binafsi katika bandari za Tanzania Bara kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uwakala wa meli. Utaratibu wa wamiliki wa meli kutumia makampuni binafsi ulianza mwaka 1999 baada ya Serikali kulegeza masharti ya NASACO kuwa ndiyo kampuni pekee ya uwakala wa meli. Masharti hayo yalilegezwa kwa kutoa leseni kwa makampuni binafsi ya uwakala wa meli. Marekebisho hayo yalitoa fursa kwa makampuni binafsi kuingia kwenye biashara ya uwakala ili kuongeza ushindani. Licha ya kwamba hapakuwa na mfumo madhubuti wa kisheria wa kudhibiti na kusimamia biashara hiyo.

1.1.1 Utendaji wa Kampuni ya Taifa ya Wakala wa Meli-NASACO

8. **Mheshimiwa Spika** Kumbukumbu mbalimbali za Serikali zinaonesha kuwa NASACO ilitekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kupata mafanikio makubwa katika kipindi chote cha uhai wake kabla ya kuwekwa kwenye orodha ya kubinafsishwa (*specified*) mwaka 1997 na kufungwa kabisa mwaka 2002. Kabla ya kuwa (*specified*), NASACO ilitoa ajira kwa watazania wasiopungua mia saba (700) na ilikuwa na uwezo wa kulipa kodi serikalini kati ya shilingi milioni mia tano (Tshs. 500,000,000) hadi milioni mia saba (Tshs. 700,000,000) na kutoa gawiwo kwa Msajili wa Hazina kati ya shilingi milioni tisini (Tshs. 90,000,000) hadi milioni mia moja (Tshs, 100,000,000) kwa mwaka.

Jedwali Namba 1: Mwenendo wa Shehena ya Mizigo kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 1991 hadi 1996

	1991/92	1992/93	1993/94	1994/1995	1995/1996
Idadi ya meli	760	857	778	772	753
Mizigo iliyoingia (tani)	3.1	4.2	3.4	3.38	3.28
Mizigo iliyotoka (tani)	2.8	1,7	0.9	0.8	0.92
Jumla	5.9	5.9	4.3	4.18	4.28

Chanzo: *Taarifa ya Mwaka ya NASACO kwa mwaka 1995/1996*

Jedwali Namba 2: Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya NASACO kwa kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka 1991 hadi 1996

	1991/92	1992/93	1993/94	1994/1995	1995/1996
MAPATO(Tsh Bil)	2.22	4.12	4.40	4.70	4.24
MATUMIZI(Tsh Bil)	1.36	2.29	3.40	4.04	4.63
FAIDA(Tsh Bil)	0.86	1.83	1.00	0.66	(0.39)

Chanzo: *Taarifa ya Mwaka ya NASACO kwa mwaka 1995/1996*

9. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa jedwali namba 2, katika kipindi cha kuanzia mwaka 1991 hadi 1996 faida ya

NASACO ilifikia shilingi za kitanzania billion 1.83 mwaka 1992/1993 na kuanza kupungua mfululizo kuanzia mwaka 1993/1994 kutokana na sababu mbali mbali zifuatazo:-

- (a) Kufungwa kwa utoaji wa huduma za meli kupitia Bandari ya Dar es Salaam kwa baadhi ya Makampuni ya meli kama vile *Zambia National Line (ZNL)*, *the Shipping Corporation of India (SCI)*, *Lloyd Triestino (LT)* na *Baltic*;
- (b) Kushuka kwa ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam kutokana na kuwa na vifaa duni vya kazi;
- (c) Kuongezeka kwa gharama za usafirishaji kwa njia ya reli na barabara kwenda nchi jirani kulikofanya nchi hizo kuchagua bandari mbadala za nchi zingine;
- (d) Ukuaji mdogo wa biashara za kimataifa kutokana na sababu mbalimbali;
- (e) Kukosekana kwa utulivi wa kisiasa katika mataifa ya Rwanda na Burudi kuliathiri shehena zilizokuwa zinakwenda na kutoka katika nchi hizo;
- (f) Kuwepo kwa urasimu katika huduma za forodha; na
- (g) Matumizi ya teknolojia duni katika kusimamia na kuendesha shughuli za uwakala.

2.0 UDHIBITI WA SEKTA YA USAFIRI WA MAJINI ULIVYO SASA

10. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na changamoto zilizobainika katika tasnia ya biashara ya uwakala wa meli, Bunge katika nyakati tofauti lilifanya marekebisho ya Sheria mbalimbali na kutunga Sheria zingine. Miongoni mwa Sheria hizo ni:-

- a) Sheria ya Usafiri wa Majini, Namba 21 ya Mwaka 2003 (*The Merchant Shipping Act, 2003*);
- b) Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini Na. 9 ya Mwaka 2003 (*The Surface and Marine Transport Regulatory Act, 2003*); na

c) Sheria ya Uwakala wa Meli Na. 11 ya Mwaka 2002 (*The Shipping Agency Act, 2002*).

3.0 TOFAUTI KATI YA NASACO NA NASAC

11. **Mheshimiwa Spika**, hapo awali shughuli za Uwakala wa meli nchini (Tanzania Bara) zilikuwa zinatekelezwa na Kampuni ya Serikali iliyojulikana kwa jina la NASACO. Kwa sasa, kupitia Muswada huu Serikali inaleta mapendekezo ya kuundwa kwa Shirika jipya la Uwakala wa Meli nchini (NASAC). Kutokana na maelezo hayo, upo umuhimu wa kubainisha tofauti kati ya NASACO ya zamani na NASAC inayopendezwa kuanzishwa. Baadhi ya tofauti hizo ni:-

a) **NASACO ilikuwa Wakala wa Meli nchini wakati NASAC inakuwa Msimamizi wa Mawakala wa meli japokuwa zipo baadhi a shughuli mahsusi ambazo NASAC itazitekeleza kama Wakala wa Meli. Shughuli hizo zinaonekana katika Kifungu Na. 6 cha Muswada;**

b) **NASACO ilitekeleza majukumu yake katika kipindi ambacho hapakuwa na Makampuni binafsi ya Uwakala wa Meli (*monopoly*) wakati NASAC inaundwa ili kufanikisha majukumu ya Uwakala wa Meli kipindi cha soko huria (*libarization*);**

c) NASACO haikujihusisha na masuala ya Usimamizi wa Mazingira ya baharini wakati NASAC itakuwa na jukumu hilo kwa kuzingatia masharti ya Mikataba na Sheria za Kimataifa kuhusu mazingira ya bahari;

d) NASACO haikujihusisha na masuala ya usalama wa meli baharini wakati NASAC itakuwa na jukumu hilo kwa mujibu wa Kifungu Na.11 cha Muswada; na

e) NASACO haikuwa inasajili vyombo vya baharini wakati NASAC itakuwa inashughulikia usajili wa vyombo vya baharini kwa mujibu wa Kifungu Na. 12 cha Muswada.

4.0 MADHUMUNI YA MUSWADA

12. **Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Uwakala wa Meli Nchini wa Mwaka 2017 (*The National Shipping Agencies Bill, 2017*) una madhumuni ya kutunga Sheria ambayo pamoja na mambo mengine, itaanzisha Shirika litakalosimamia shughuli za Uwakala wa Meli na uondoshaji wa shehena (*Clearing and Forwarding*) za madini, makinikia, bidhaa zitokanazo na madini, wanyamahai na nyara za Serikali.

Aidha, Shirika linalopendekezwa kuanzishwa litajulikana kwa jina la Shirika la Taifa la Wakala wa Meli (*The National Shipping Agency Corporation- NASAC*). Majukumu mengine ya Shirika hilo yatakuwa ni kudhibiti huduma za usafiri wa majini, kudhibiti masuala ya mazingira baharini, kuangalia usalama na ulinzi wa vyombo vya majini kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa ambayo nchi imeridhia au itaridhia.

13. **Mheshimiwa Spika**, vilevile dhumuni lingine la kuanzishwa kwa NASAC ni kuanzisha Shirika la Uwakala wa Meli nchini litakalokuwa na majukumu ya uendeshaji wa biashara ya Uwakala wa Meli kwa upande mmoja na majukumu ya udhibiti wa mazingira, usalama na ulinzi wa vyombo vya majini pamoja na udhibiti wa huduma za usafiri wa majini kwa upande mwingine. Aidha, Shirika linalolanzishwa litasimamia utekelezaji wa Sheria ya Usafiri wa Majini, Namba 21 ya mwaka 2003 (*The Merchant Shipping Act, 2003*) ambayo ndiyo sheria ya msingi (*substantive law*) katika sekta hii.

4.1 Umuhimu wa Kuanzishwa kwa Shirika la Taifa la Wakala wa Meli (*National Shipping Agency Corporation-NASAC*)

14. **Mheshimiwa Spika**, kuanzishwa kwa NASAC kuwa Wakala Mkuu atakayesimamia mawakala wa meli binafsi kutaongeza ufanisi katika utendaji wa bandari na kuongeza usahihi wa taarifa zitolewazo na wakala wa meli kuhusu thamani, aina na kiasi cha shehena.

15. **Mheshimiwa Spika**, taarifa zilizopo ni kwamba baadhi ya Mawakala wasio waaminifu hutumia udhaifu wa kiutendaji wa baadhi ya watumishi wa bandari kufanya udanganyifu kiasi cha kuathiri sifa, mapato na ufanisi wa bandari. Hivyo, kuanzishwa Kwa NASAC kutasaidia usimamizi wa karibu wa maslahi ya nchi kwenye sekta ya usafiri majini.

Aidha, uwepo wa NASAC unatarajiwa kuongeza ufanisi katika udhibiti wa usafiri wa majini kwa kuwa na malengo mahsusi ya kuboresha sekta hiyo. Uzoefu unaonesha kuwa nchi nyingi zenye bahari (*Maritime States*) zina vyombo mahasusi vinavyoshughulikia udhibiti wa usafiri majini. Kwa mfano, nchi jirani ya Kenya ina Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Majini (*Kenya Maritime Authority*), Tanzania Visiwani ina Mamlaka inayoitwa *Zanzibar Maritime Authority* (ZMA), Afrika ya kusini wanayo Mamlaka inayoshughulikia masuala yote ya usafiri wa majini inayoitwa *South Africa Maritime Regulatory Authority* (SAMRA).

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

16. **Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina wa Muswada, na kupitia kifungu kwa kifungu, Kamati ilishauriana na Serikali kuhusu marekebisho mbalimbali katika Muswada na kukubaliana. Mapendekezo hayo yalihusu uandishi na madhui kwa kuzingatia madhumuni ya Sheria inayokusudiwa. Mfano wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati kama ifuatavyo:-

a) Jina la Muswada;

17. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu jina la Muswada '***National Shipping Agencies Corporation Bill, 2017 (NASAC)***'; Kamati haikuridhika na jina hilo, hivyo inapendekeza jina la Muswada liwe '***Tanzania Maritime Authority***' ili kuendana na maudhui ya Sheria inayotungwa. Hii ni kutokana na ukweli kuwa chombo hiki kazi yake kubwa itakuwa ni kudhibiti hivyo jina linapaswa kuendana na maudhui makubwa ya Sheria hii. Aidha, uzoefu wa Kimataifa unaonesha kwamba, vyombo kama hivi mara nyingi katika jina vinakuwa na neno

'' **Maritime**'' . Mfano, *Zanzibar Maritime Authority'' Kenya Maritime Authority''*, ''*Mozambique Maritime Authority''*, na ''*South African Maritime Authority''*,

18. **Mheshimiwa Spika**, pendekezo hili bado Serikali haijaliridhia.

b) Eneo ambalo Sheria itatumika;

19. **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 2(2); Kamati inashauri kifutwe ili chombo kinachoanzishwa kifanye kazi Tanzania Bara pekee ili kuondoa mgongano na vyombo vinvavyofanya majukumu haya Zanzibar.

c) Majukumu ya Shirika- NASAC;

20. **Mheshimiwa Spika**, Katika Sheria inayopendekezwa, Kamati ilibaini kuwa NASAC inayopendekezwa itakuwa na jukumu la udhibiti na Kufanya Kazi za Uwakala. Kamati inashauri kuwa ni vema Serikali ikatenganisha masuala ya udhibiti na ufanyaji wa biashara ili kuweza kuondoa mgongano wa kimaslahi kwa mdhibiti kufanya kazi uwakala.

d) Utoaji wa Leseni kwa Mawakala wa Meli;

21. **Mheshimiwa Spika**, Sheria iliyokuwepo ilikuwa inaruhusu Wakala wa Meli kuwa pia Wakala wa Mzigo. Sheria inayopendekezwa yaani NASAC Kifungu cha 38 (2) (a) kinachohusu utoaji wa leseni kwa mawakala wa meli. Kifungu hiki hakiruhusu mwenye meli kupewa leseni ya uondoshaji wa shehena (*clearing and forwarding*).

Kamati inaona kuwa hakuna sababu za msingi za kuzuia hili kwani ni ngumu sana katika Dunia ya sasa kuepuka muingiliano huo. Jambo la msingi ni kuwa na udhibiti na ufuatiliaji wa karibu ili kuepuka ubadhilifu ambao awali ulikuwa unajitokeza.

e) Rufaa

22. **Mheshimiwa Spika**, katika kifungu cha 49, kimempa Mamlaka makubwa Waziri kuwa chombo cha mwisho katika

maamuzi ya rufaa. Kamati inashauri kama ilivyo kwa Mamlaka zingine, Tume ya Ushindani (*Fair Competition Commission*) kiwe chombo cha mwisho kwenye ngazi ya rufaa na sio Waziri.

f) Udhhibiti wa Huduma za Usafiri Majini;

23. **Mheshimiwa Spika**, kama wakala atatofautishwa na mdhibiti yaani vyombo viwili tofauti, Kamati inapendekeza biashara zingine zijumuishwe kwa wakala wa serikali ikiwa ni pamoja na:-

- i. Umiliki wa Meli (*Ship Owners*);
- ii. Uwakala wa Meli (*Shipping Agents*);
- iii. Uwakala wa forodha (*Clearing and Forwarding Agents*);
- iv. Kufunga na kufungua mizigo (*Lashing*);
- v. Uwakala wa Kuhesabu Mizigo (*Tallying*);
- vi. Uhifadhi wa mizigo (*Storage*);
- vii. Kupakia na kupakua mizigo (*Cargo stuffing*); na
- viii. Biashara ya kuuza vifaa na huduma mbalimbali kwenye meli (*Ship Chandling*).

Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ilikubali na kuzingatia.

g) Kifungu cha 30 kinachohusu masuala ya bajeti;

24. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa Sheria hii inaanzisha NASAC ambayo ni shirika la kibiashara, kifungu hiki hakiendani na masharti ya kifungu cha 17 na 22 cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Sheria ya Mashirika ya Umma, Sura ya 257. Kamati inapendekeza kuwa kifungu hicho kiandikwe upya ili kuwiana na masharti ya Sheria ya Bajeti na Sheria ya Mashirika ya Umma.

h) Kifungu cha 55 kinachohusu kufutwa kwa Sura ya 177 na Sura 415 ya Sheria za Tanzania;

25. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Wakala wa Meli inayopendekezwa kufutwa katika kifungu cha 55 cha Sheria hii iliweka masharti yaliyowezesha ufuatiliaji wa karibu wa

Kampuni zinazofanya biashara katika sekta hii. Sheria inayopendekezwa haibainishi masharti hayo. Kamati inapendekeza kuwa:-

- i) Sheria hii iweke utaratibu wa kufuatilia kwa karibu kampuni zinazofanya biashara katika sekta hii;
- ii) Sheria ibainishe kuwa ukiukwaji wa kiwango kitakachoainishwa itakuwa ni kosa la jinai;na
- iii) Sheria ibainishe kuwa Kampuni ambayo mali zake na faida hazifikii kiwango kilichoainishwa na Waziri itazuiwa kutangaza, kuhamisha au kutoa gawio kwa faida inayopatikana kutokana na biashara zake.

26. **Mheshimiwa Spika**, maelezo zaidi kuhusu maoni yaliotolewa na Kamati na kuafikiwa na Serikali kwa kiasi kikubwa yanaweza kurejewa katika kiambatisho cha Taarifa hii.

6.0 MAONI YA JUMLA

a) **Ushiriki wa Watanzania katika Sekta Binafsi ya Uwakala wa Meli;**

Sheria ya Uwakala wa Meli ya mwaka 2002 inayokusudiwa kufutwa na Muswada huu inatoa upendeleo kwa Watanzania na Kampuni za Kitanzania kushiriki katika biashara ya Uwakala wa Meli. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria hiyo kinachobainisha kuwa leseni ya biashara ya Uwakala wa Meli itatolewa kwa raia wa Tanzania au kampuni ambayo imesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 ambayo hisa zake zinamilikiwa na raia wa Tanzania kwa zaidi ya asilimia 50.

Muswada unaopendekezwa haujagusia suala hili. Hivyo, Kamati inapendekeza kwamba, suala la kutoa kipaumbele kwa Watanzania lizingatiwe kwenye Muswada huu ili kutoa fursa pana zaidi kwa Watanzania kushiriki moja kwa moja kwenye shughuli za kiuchumi zinazopatikana hapa nchin

b) **Udhaifu wa Sekta ya Usafiri wa Majini Tanzania;**

Kamati imeona yapo mapungufu yanayoikabili sekta ya bandari hivyo pamoja na kuletwa kwa Sheria hii ni vema

Serikali ikabainisha mapungufu hayo na kuweza kufahamu yanasababishwa na sekta ipi kati ya sekta zinazofanya kazi bandarini zikiwemo Mawakala, Mamlaka ya bandari Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Aidha, Kamati ilibaini yapo mapungufu yaliyopelekea SUMATRA kushindwa kuthibiti shughuli za usafiri wa maji hivyo pamoja na Sheria hii, ipo haja ya Serikali kufanyia kazi mapungufu yaliyokuwepo ili kuweza kuyaondoa na shirika linalotarajiwa kuanzishwa liweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

c) Changamoto zilizobainika katika Udhibiti wa sekta Usafiri wa Njia ya Maji;

Kamati inaishauri mambo yafuatayo ilikuweza kukamiliana na changamoto zilizopo:-

a) Serikali ijikite katika kuweka sheria ambazo zitawavutia wafanyabiashara kutumia bandari ya Dar es salaam, kwani kuna wafanyabiashara waliohamu kutumia bandari yetu kutokana na kuwa na sheria kandamizi.

b) Serikali kuziba mianya ya kisheria inayoruhusu kufanyika kwa udanganyifu katika utoaji wa leseni, ukwepaji kodi, tozo zisizokuwa na uhalisia pamoja na usafirishaji wa bidhaa haramu au bidhaa zilizo chini ya kiwango;

c) Serikali itambue kuwa mapato mengi hupotea kwa sababu ya watumishi wasiowaaminifu na hasa upande wa mapato yaani Mamlaka ya Mapato Tanzania-TRA ambao wanawajibibu kuhakiki mizigo inapotoka na inapoingia bandarini. Hivyo serikali iongeze udhibitiwa kielekitroniki ili kila kinachofanyika na maafisa vionekane na mamlaka zingine. Sheria haiwezi kutibu kila kitu na hasa kwa watumishi wasio waaminifu;na

d) Watumishi kwenye sekta zote wapimwe kwa vigezo vya kitaalamu na uadilifu.

7.0 HITIMISHO

27. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati, sasa naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia Muswada huu kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Prof Norman Adamson Sigalla King, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb "
5. Mhe. James Francis Mbatia, Mb "
6. Mhe. Mansoor Shanif Hirani, Mb "
7. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb "
8. Mhe. Saul Henry Amon, Mb "
9. Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb "
10. Mhe. Quambalo Willy Qulwi, Mb "
11. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb "
12. Mhe. Halima Abdallah Bulembo, Mb "
13. Mhe. Dkt.Chuachua Mohamed Rashid, Mb "
14. Mhe. Mary Deo Muro, Mb "
15. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb "
16. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb "
17. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb "
18. Mhe. Dua William Nkurua, Mb "
19. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb "
20. Mhe. Lathifah Hassan Chande, Mb "
21. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb "
22. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb "
23. Mhe. Emmanuel Mwakasaka, Mb "
24. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb "
25. Mhe. Charles Kitwanga, Mb "
26. Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mb "
27. Mhe. Rukia Kassim, Mb "

28. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen N. Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake. Aidha, napenda kuishukuru sekretarieti ya Kamati ikiongozwa na

Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Dickson M. Mbisile, Makatibu wa Kamati Ndg. Hosiana John na Ndg. Richard Masuke. Vilevile Kamati inamshukuru washauri wa Sheria Ndg. Stephano Seba Mbutu na Ndg. Thomas Shawa kwa kuihudumia Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

29. **Mheshimiwa Spika**, vilevile naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa Mnyaa, Mb. Manaibu Waziri Mhe. Eng Atashasta Justus Ndiye Mb, Mhe. Elias John Kwandikwa Mb. Aidha, Kamati inamshukuru Katibu Mkuu Dkt. Leonard M. Chamuriho akisaidiana na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

30. **Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Prof. Norman A. S. King, Mb
MWENYEKITI
KAMATI YA MIUNDOMBINU
16/11/2017

NAIBU SPIKA: Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Kuhusu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

MHE.DKT. IMMACULATE S. SEMESI – (K.n.y. MSEMAMI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO): Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa James Mbatia, maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania ya Mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ni haki ya msingi ya kila raia wa Tanzania na msingi wa haki hiyo umewekwa kwa Katiba ya Nchi. Ibara ya 18(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba, kila mtu anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya mawasiliano kuwa takwa la Kikatiba katika nchi yetu, lakini hakuna ubishani kwamba, mawasiliano ya aina yoyote ni nyenzo muhimu katika kuchagiza maendeleo. Kutokana na umuhimu wa mawasiliano katika maendeleo baadhi ya Mataifa mengine yamekuwa yakitoa ruzuku katika njia za mawasiliano ili kuwapungumzia mzigo wa gharama za mawasiliano wananchi wao, jambo ambalo limewawezesha kufanya mawasiliano kwa urahisi na hivyo kukuza biashara zao na shughuli zingine za kiuchumi na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi katika Mataifa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; Marekani hutoa ruzuku kwa makampuni ya simu kupitia Mfuko wa Huduma kwa Wote (*Universal Service Fund*) ambao unaratibiwa na Tume ya Mawasiliano ya Muungano wao (*Federal Communications Commission – FCC*). Pamoja na kutambua kuwa hapa Tanzania kuna Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCSAF*) unaotoa ruzuku kwa makampuni ya simu kwa ajili ya kujenga miundombinu ya simu kama vile minara, lakini mawasiliano ya simu hapa nchini kwa maana ya muda wa maongezi (*air time*) yako juu sana hasa simu za nje pale mteja anapofanya *international calls*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tofauti na jitihada hizi za kidunia za kurahisisha mawasiliano kwa kadiri iwezekanavyo, Serikali yetu inaonekana kwenda kinyume na jitihada hizo kwa kuyadhibiti na kuyafanya mawasiliano kuwa magumu. Kutungwa kwa Sheria ya Makosa ya Kimtandao (*Cyber Crimes Act*), Sheria ya Kudumu ya Vyombo vya Habari (*Media Services Act*), kukatishwa kwa matangazo ya *BungeLive*, kupigwa marufuku kwa mikutano ya hadhara ya siasa, kufungiwa kwa magazeti na mengine kunyimwa leseni ni

baadhi ya viashiria vya kunyimwa kwa uhuru wa habari na mawasiliano nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutakubaliana kwamba, mawasiliano ni nyenzo muhimu ya kukuza uchumi, basi hatuna budi kuondoa vikwazo vyote vinavyofanya mawasiliano kuwa magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naenda kuelezea mwelekeo wa dunia katika umiliki wa waendeshaji wa mashirika ya umma. Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi duniani yanayochagizwa na kuenea kwa utandawazi, kulisababisha mabadiliko katika umilikaji na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi. Uchumi ambao hapo awali ulikuwa ukimilikiwa na kudhibitiwa na Serikali (*State Controlled Economy*) ulianza kumilikiwa, kuendeshwa na kudhibitiwa na mahitaji ya soko (*Market Governed Economy*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maneno mengine Serikali za Mataifa mbalimbali zilianza kujiondoa kwenye umiliki wa udhibiti wa uchumi na badala yake kuacha jukumu hilo kwa sekta binafsi chini ya udhibiti wa nguvu ya soko (*market forces*) na sio chini ya udhibiti wa nguvu za dola.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mashirika ya umma, mweleko ulikuwa huo huo, kwa maana ya kuondoa umiliki na udhibiti wa moja kwa moja wa Serikali na kuanza kuishirikisha sekta binafsi katika kumiliki na kuendesha mashirika hayo kupitia mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (*Public Private Partnership*) au ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilikuwa imeshapiga hatua hiyo kupitia sera yake ya ubinafsishaji katika miaka ya 1990. Hata hivyo, ubinafsishaji haukuzaa matunda yaliyokusudiwa kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zilipelekea baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa kushindwa kujiendesha kwa faida, kutokana na mfumo wa kodi uliopo hapa nchini na mitaji ya walionunua kuwa midogo kuweza kukidhi teknolojia ya uzalishaji inayobadilika mara kwa mara na kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, si nia yangu kuelezea historia ya ubinafsishaji nchini; lakini kuna haja kubwa sana ya kuboresha mazingira ya kukuza sekta binafsi nchini. Hii ni kwa sababu hali ya sekta binafsi kwa sasa iko taabani na hali hii ikiendelea itadumaza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba, kwa kuwa tayari *TTCL* ipo na inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100; ingekuwa ni tija zaidi Serikali iuze hisa zake kwenye soko la hisa ili Shirika hilo limilikiwe na kuendeshwa na sekta binafsi. Serikali inaweza kubaki na angalau asilimia 20 ya hisa kwa kuwa imewekeza mtaji wake katika shirika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa pendekezo hili ni kuweka mazingira sawa ya ushindani wa kibiashara baina ya Kampuni ya Serikali na makampuni mengine ya simu, kwa kuipunguzia Serikali idadi ya hisa na mamlaka ya uendeshaji (*managerial power*).

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nakwenda kugusia masharti ya kupitisha sheria inayohusu mambo ya Muungano. Kwa mujibu wa nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mawasiliano ya simu ni miongoni mwa mambo ya Muungano. Kwa kutambua takwa hilo la kikatiba, kifungu cha (2) cha Muswada huu kinaonesha eneo la matumizi ya sheria inayopendekezwa; imeelekeza kwamba, Sheria hii inayopendekezwa itatumika Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ibara ya 98(1)(b) ya Katiba imeweka utaratibu wa kupitisha sheria ambayo matumizi yake ni kwa pande zote za Muungano kuwa itahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Zanzibar. Orodha ya mambo ambayo mabadiliko yake yanahitaji (*special majority*)kilo katika orodha ya pili ya nyongeza ya pili iliyoko mwishoni mwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika orodha hiyo ya masuala yanayohitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Bara na Zanzibar yako mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Sheria inayopendekezwa inahusu mambo ya Muungano na kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka masharti kwamba sheria ya namna hiyo lazima iungwe mkono na idadi isiyopungua theluthi mbili ya Wabunge kutoka pande zote mbili za Muungano. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa Bunge kuzingatia matakwa ya Katiba wakati wa kuipiga kura kupitisha sheria hii ili sheria hii iwe na baraka za pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naenda kugusia Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi. Kifungu cha saba (7) cha Muswada huu, kinaelezea uwepo wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Mawasiliano la Taifa, namna wajumbe wake wanavyopatikana, idadi ya wajumbe, sifa za kuteuliwa kuwa mjumbe na utaratibu wa malipo kwa wajumbe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kwamba Sheria hii iliyopendekezwa ni ya Muungano, ilitarajiwa kwamba Bodi ya Wakurugenzi iwe pia na sura ya Muungano kwa kuwa na uwiano wa wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano. Hata hivyo, ukisoma kifungu cha 7(2)(b) utaona kwamba ni mjumbe mmoja tu wa bodi atatoka Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba uwakilishi huu wa Zanzibar ni mdogo mno kuweza kuleta sura ya Muungano katika Bodi hiyo ya Wakurugenzi. Kwasababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba; angalau wajumbe wawili wa bodi hiyo wawe wanatoka Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitagusia *TTCL PESA Limited* kuhusu kuondolewa kwake katika Muswada huu. kifungu cha

29 cha Muswada huu kinaelezea kuendelea kuwepo kwa *TTCL PESA Limited* katika Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania na kwamba *TTCL PESA* itaendelea kutoa huduma za kutuma na kupokea fedha kwa mfumo wa kidigitali kama ilivyokuwa na kwamba Shirika la Mawasiliano litaendelea kuwa na hisa katika kampuni hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa kifungu cha 29 unaoelezea kuendelea kuwepo kwa *TTCL PESA Limited* hauna maana yoyote kisheria kwa sababu vifungu vya 28, 31, na 33 tayari zimeshaelezea kwamba mali zote, madeni yote, watumishi wote, nyaraka na kumbukumbu zote za iliyokuwa Kampuni ya Simu zitahamishiwa kwenye Shirika jipya la Mawasiliano ya Simu la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, ni kwamba, hata *TTCL PESA Limited* itakuwa imehamishiwa kwenye shirika jipya kwa utaratibu huo huo. Hivyo, hakuna sababu tena ya kuweka kifungu kinachohusu *TTCL PESA* katika Muswada huu vinginevyo italeta taswira ya uandishi mbaya wa sheria (*bad drafting of law*) kwa kurudiarudia masuala ambayo yameshafanyiwa kazi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza kwamba, kifungu hicho cha 29 kifutwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka ya Waziri katika utekelezaji wa sheria inayopendekezwa. Kifungu cha 7(7) cha Muswada huu kinampa Waziri mamlaka ya kubadili, kurekebisha au kuondoa maelekezo ya kifungu chochote au vifungu vyote vya Jedwali lililopo mwishoni mwa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa, vifungu vilivyopo katika jedwali vinahusu muda wa ajira kwa Wajumbe wa Bodi, nafasi za kazi za muda mfupi, kutengua uteuzi wa Mjumbe wa Bodi, vikao vya Bodi, wajumbe waalikwa, akidi na mchakato wa uamuzi wa Bodi, muhtasari wa vikao vya Bodi, uamuzi wa Bodi, kazi za Bodi kuendelea hata kama kuna nafasi za wajumbe zilizo wazi na mamlaka ya Bodi kurekebisha michakato yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mamlaka haya ya Waziri ni makubwa mno na yanaweza kutumika vibaya ikiwa hakutakuwa na jicho la pili. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba ili kutekeleza dhana ya utawala shirikishi, iwe ni lazima Waziri kushauriana na Mwenyekiti wa Bodi, kabla ya kufanya mabadiliko yoyote chini ya Ibara ya 7(7). Hii itasaidia kuleta ufanisi katika Shirika. Ifahamike kwamba mashirika mengi yanashindwa kuwa shindani kutokana na kutegemea uamuzi unaofanywa na mtu mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhali kifungu cha 9(1) kinampa Waziri mamlaka ya kutoa maagizo au maelekezo kwa Bodi juu ya mambo ya jumla au jambo mahususi kuhusu utekelezaji wa kazi za shirika na bodi itatakiwa kutekeleza maagizo hayo kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua umuhimu wa Waziri kutoa maelekezo ya jumla. Tafsiri rahisi ya kifungu hiki ni kwamba lazima Bodi itekeleze maelekezo hayo. Kuibana Bodi kwamba lazima itekeleze maagizo ya Waziri, ni kuinyima uhuru wa kufanya kazi zake. Kwa kuwa mwisho wa siku Bodi ndiyo itakayopimwa juu ya mwenendo wa Kampuni, basi ihukumiwe kwa utendaji wake. Mstari wa mwisho katika kifungu cha 9(1) unainyima kabisa Bodi meno ya maamuzi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitagusia pia sifa za kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano la Taifa. kifungu cha 15(3)(b) cha Muswada huu, mbali na kigezo cha elimu, kinaelekeza kwamba ili mtu awe na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano la Taifa ni lazima mtu huyo awe na uzoefu wa miaka nane katika ngazi ya juu ya utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba huku ni kuwanyima fursa Watanzania wenye weledi na uwezo wa kuongoza taasisi zetu na pia inaleta taswira mbaya kwamba pengine kifungu hiki kimewekwa kwa hila ili kumzuia mtu fulani asipate nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako Watanzania wenye elimu nzuri kama ilivyoielezwa katika kifungu cha 15(3)(a) na wana uwezo mzuri kiutendaji. Kambi Rasmi haipingi umuhimu wa uzoefu, lakini uzoefu huo usiwekwe juu mno kiasi cha kufanya watu wenye taaluma husika na uzoefu wa miaka miwili au mitatu (ambayo kwa mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni unatosha) kwa lengo baya la kuwaengua watu wenye sifa za kuongoza Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumzia uzoefu wa miaka nane; katika ngazi ya juu ya utawala maana yake unazungumzia mtu anayekaribia kustaafu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba badala ya kuweka uzoefu wa miaka nane, basi angalau iwe miaka mitano. Hii ni kwa sababu kinachohitajika ni utendaji uliotukuka na rekodi nzuri ya kazi na sio miaka mingi kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitagusia pia kufutwa kwa Sheria ya Kampuni ya Simu Tanzania, Sura Namba 304 ya Sheria za Tanzania. Ibara ya 26 ya Muswada huu inapendekeza kufutwa kwa Sheria ya Kampuni ya Simu Tanzania, Sura ya 304 ya Sheria za Tanzania na badala yake kutunga Sheria mpya ya Shirika la Mawasiliao ya Simu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya madhumuni na sababu za kuleta Muswada huu, haikuelezwa ni upungufu gani mkubwa uliokuwepo kwenye Sheria ya Kampuni ya Simu, Sura 304 inayofutwa, yaliyopelekea kutungwa kwa Sheria mpya ya Shirika la Mawasiliano ya Simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyofahamika, ikiwa Sheria fulani ina upungufu mdogo mdogo, huwa Serikali inaleta Muswada wa marekebisho ya Sheria hiyo na siyo kufuta sheria hiyo kwa kuleta Muswada wa sheria mpya. Kwa kuwa Serikali imeleta Muswada mpya na kwa kuwa Serikali haijieleza ni upungufu gani mkubwa unaohitaji kutungwa kwa Sheria mpya katika eneo hili la mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni sababu zipi zilizopelekea kutungwa Sheria mpya ambazo zisingeweza kutatuliwa kwa kuleta Muswada wa marekebicho ya Sheria ya Kampuni ya Simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulihakikishia Bunge hili ni kwa namna gani Kampuni ya Simu ya *TTCL* itajijendesha kwa faida katika shirika ikiwa kwa miaka yote Kampuni hii imekuwa na ufanisi mdogo ukilinganisha na makampuni mengine ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kuhitimisha. Sheria bora ni ile inayotungwa kwa maridhiano kati ya Kambi mbili Bungeni yaani Kambi ya Serikali na ile ya Upinzani au Kambi ya Wabunge wa Tanzania Bara na Kambi ya Wabunge wa Tanzania Zanzibar kwa Sheria zile zinazohusu mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Sheria zinazotungwa kwa maridhiano huwa rahisi kuliko zile zinazotungwa kwa ushabiki, ubabe au kwa kiburi cha wingi Wabunge wa Kambi moja dhini ya nyingine. Sheria zinazopitishwa kwa namna hiyo, mara nyingi huwa hazivasaidii wananchi, kwa kuwa zinakuwa zimebeba maslahi ya kambi hizo kuliko maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Nibu Spika, ni matumaini ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwamba Sheria hii inayopendekezwa itapitishwa kwa maridhiano. Aidha, ni mategemeo ya Kambi ya Upinzani kwamba matakwa ya Katiba ya kutumia idadi ya Wabunge isiyopungua theluthi mbili kutoka Bara na theluthi mbili kutoka Zanzibar yatazingatiwa katika kupitisha sheria hii, kwa kuwa Sheria hii ni ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA
MAWASILIANO, MHESHIMIWA JAMES FRANCIS MBATIA
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI YA
UPINZANI, KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA SHIRIKA
LA MAWASILIANO YA SIMU TANZANIA YA MWAKA
2017 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania ya Mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, mawasiliano ni haki ya msingi ya kila raia wa Tanzania, na msingi wa haki hiyo umewekwa na Katiba ya Nchi. Ibara ya 18(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema kwamba: *“ kila mtu anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake”*

Mheshimiwa Spika, licha ya mawasiliano kuwa takwa la kikatiba katika nchi yetu, lakini hakuna ubishani kwamba mawasiliano ya aina yoyote ni nyenzo muhimu katika kuchagiza maendeleo. Kutokana na umuhimu wa mawasiliano katika maendeleo, baadhi ya mataifa mengine yamekuwa yakitoa ruzuku katika njia za mawasiliano ili kuwapunguzia mzigo wa gharama za mawasiliano wananchi wao; jambo ambalo limewawezesha kufanya mawasiliano kwa urahisi na hivyo kukuza biashara zao na shughuli nyingine za kiuchumi na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi katika mataifa yao. Kwa mfano, Marekani hutoa ruzuku kwa makampuni ya simu kupitia Mfuko wa Huduma kwa Wote (Universal Service Fund) ambao unaratibiwa na Tume ya Mawasiliano ya Muungano wao (Federal Communications Commission – FCC). Pamoja na kutambua kuwa hapa Tanzania kuna Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) unaotoa ruzuku kwa makampuni ya simu kwa ajili ya kujenga

miundombinu ya simu kama vile minara lakini mawasiliano ya simu hapa nchini (kwa maana ya muda wa maongezi – ‘*air time*’) yako juu sana hasa simu za nje (International calls).

Mheshimiwa Spika, Tofauti na jitihada hizi za kidunia za kurahisisha mawasiliano kwa kadri iwezekanavyo; Serikali yetu inaonekana kwenda kinyume na jitihada hizo kwa kuyadhibiti na kuyafanya mawasiliano kuwa magumu. Kutungwa kwa sheria za makosa ya kimtandao (Cyber Crimes Act), Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari (Media Services Act), Kukatishwa kwa matangazo ya Bunge live; Kupigwa marafuku kwa mikutano ya hadhara ya siasa; kufungwa kwa magazeti na mengine kunyimwa leseni ni baadhi ya viashiria kwa kuminywa kwa uhuru wa habari na mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Spika, kama tunakubaliana kwamba mawasiliano ni nyenzo muhimu ya kukuza uchumi, basi hatuna budu kuondoa vikwazo vyote vinavyofanya mawasiliano kuwa magumu.

2. MWELEKEO WA DUNIA KATIKA UMILIKI NA UENDESHAJI WA MASHIRIKA YA UMMA

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya kiuchumi duniani yaliyochagizwa na kuenea kwa utandawazi, kulipelekea mabadiliko katika umilikaji na uendeshaji wa shughuli za kiuchumi. Uchumi ambao hapo awali ulikuwa ukimilikiwa na kudhibitiwa na Serikali (state controlled economy) ulianza kumilikiwa, kuendeshwa na kudhibitiwa na mahitaji ya soko (market governed economy). Kwa maneno mengine, Serikali za mataifa mbalimbali zilianza kujiondoa kwenye umiliki na udhibiti wa uchumi na badala yake kuacha jukumu hilo kwa sekta binafsi chini ya udhibiti wa nguvu ya soko (market forces) na sio chini ya udhibiti wa nguvu za dola.

Mheshimiwa Spika, kwa mashirika ya umma, mweleko ulikuwa huo huo – kwa maana ya kuondoa umiliki na udhibiti wa moja kwa moja wa Serikali na kuanza kuishirikisha sekta binafsi katika kumiliki na kuendesha mashirika hayo kupitia mfumo

wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (Public Private Partnership) au ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilikuwa imeshapiga hatua hiyo kupitia sera yake ya ubinafsishaji katika miaka ya 1990. Hata hivyo, ubinafsishaji haukuzaa matunda yaliyokusudiwa kutokana na changamoto mbalimbali ambazo zilipelekea baadhi ya mashirika yaliyobinafsishwa kushindwa kujendesha kwa faida, kutokana na mfumo wa kodi uliopo hapa nchini na mitaji ya walionunua kuwa midogo kuweza kukidhi teknolojia ya uzalishaji inayobadilika mara kwa mara na kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Spika, si nia yangu kuelezea historia ya ubinafsishaji nchini; lakini kuna haja kubwa sana ya kuboresha mazingira ya kukuza sekta binafsi nchini. Hii ni kwa sababu hali ya sekta binafsi kwa sasa iko taabani na hali hii ikiendelea itadumaza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba; kwa kuwa tayari TTCL ipo, na inamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100; ingekuwa ni tija zaidi Serikali iuze hisa zake kwenye soko la hisa; ili Shirika hilo limilikiwe na kuendeshwa na sekta binafsi. Serikali inaweza kubaki na angalau asilimia 20 ya hisa kwa kuwa imewekeza mtaji wake katika shirika hilo.

Mheshimiwa Spika, msingi wa pendekezo hili ni kuweka mazingira sawa ya ushindani wa kibiashara baina ya Kampuni ya Serikali na makampuni mengine ya simu, kwa kuipunguzia Serikali idadi ya hisa na mamlaka ya uendeshaji (managerial power).

3. MASHARTI YA KUPITISHA SHERIA INAYOHUSU MAMBO YA MUUNGANO

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa nyongeza ya kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mawasiliano ya simu ni miongoni mwa Mambo ya Muungano. Kwa kutambua takwa hilo la kikatiba, kifungu cha (2) cha

Muswada huu kinayoonyesha eneo la matumizi ya sheria inayopendekezwa; imeelekeza kwamba, Sheria hii inayopendekezwa itatumika Tanzania Bara na Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 98(1)(b)ya Katiba imeweka utaratibu wa kupitisha sheria ambayo matumizi yake ni kwa pande zote za Muungano kuwa itahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya wabunge wote kutoka Tanzania Bara, na theluthi mbili ya wabunge kutoka Tanzania Zanzibar. Orodha ya mambo ambayo mabadiliko yake yanahitaji “Special Majority” iko katika orodha ya pili ya nyongeza ya pili iliyoko mwishoni mwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika orodha hiyo ya masuala yanayohitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya wabunge wote kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar; yako mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Sheria inayopendekezwa inahusu mambo ya Muungano; na kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka masharti kwamba; sheria ya namna hiyo lazima iungwe mkono na idadi isiyopungua theluthi mbili ya wabunge kutoka pande zote mbili za Muungano; hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa Bunge kuzingatia matakwa ya Katiba wakati wa kuipiga kura kupitisha sheria hii; ili sheria hii iwe na baraka za pande zote mbili za Muungano.

4. WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7 cha Muswada huu, kinaelezea uwepo wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Mawasiliano la Taifa, namna wajumbe wake wanavyopatikana, idadi ya wajumbe, sifa za kuteuliwa kuwa mjumbe na utaratibu wa malipo kwa wajumbe.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba Sheria hii inayopendekezwa ni ya Muungano, ilitarajiwa kwamba Bodi ya Wakurugenzi iwe pia na sura ya Muungano, kwa kuwa na

uwiano wa wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano. Lakini ukisoma kifungu cha 7(2) (b) utaona kwamba ni mjumbe mmoja tu wa bodi atatoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba uwakilishi huu wa Zanzibar ni mdogo mno kuweza kuleta sura ya Muungano katika bodi hiyo ya Wakurugenzi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba; angalau wajumbe wawili wa bodi hiyo wawe wanatoka Zanzibar.

5. TTCL PESA LIMITED IONDOLEWE KATIKA MUSWADA

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 29 cha Muswada huu kinaelezea kuendelea kuwepo kwa TTCL PESA Ltd katika Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania, na kwamba TTCL PESA itaendelea kutoa huduma za kutuma na kupokea fedha kwa mfumo wa kidigitali kama ilivyokuwa, na kwamba Shirika la Mawasiliano litaendelea kuwa na hisa katika kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa kifungu cha 29 unaoelezea kuendelea kuwepo kwa TTCL PESA Ltd hauna maana yoyote kisheria kwa sababu vifungu vya 28, 31, na 33 tayari zimeshaelezea kwamba mali zote, madeni yote, watumishi wote, nyaraka na kumbukumbu zote za iliyokuwa Kampuni ya Simu zitahamishiwa kwenye Shirika jipya la Mawasiliano ya Simu la Taifa. Kwa muktadha huo, ni kwamba, hata TTCL PESA Ltd itakuwa imehamishiwa kwenye shirika jipya kwa utaratibu huo. Hivyo, hakuna sababu tena ya kuweka kifungu kinachohusu TTCL PESA katika muswada huu vinginevyo italeti taswira ya uandishi mbaya wa sheria (bad drafting of law) kwa kurudia rudia masuala ambayo yameshafanyiwa kazi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza kwamba, kifungu hicho cha 29 kifutwe.

6. MAMLAKA YA WAZIRI KATIKA UTEKELEZAJI WA SHERIA INAYOPENDEKEZWA

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7(7) cha Muswada huu kinampa Waziri mamlaka ya kubadili, kurekebisha, au kuondoa maelekezo ya kifungu chochote au vifungu vyote

vya Jedwali lilipo mwishoni mwa Muswada huu. Kwa ajili ya kuweka kumbukumbu sawa, vifungu vilivyopo katika jedwali vinahusu muda wa ajira kwa wajumbe wa bodi, nafasi za kazi za muda mfupi, kutengua uteuzi wa mjumbe wa bodi, vikao vya bodi, wajumbe waalikwa, akidi na mchakato wa uamuzi wa bodi, muhtasari wa vikao vya bodi, Uamuzi wa Bodi, Kazi za Bodi kuendelea hata kama kuna nafasi za wajumbe zilizo wazi (vacancies) na mamlaka ya Bodi kurekebisha michakato yake.

Mheshimiwa Spika, mamlaka haya ya waziri ni makubwa mno, na yanaweza kutumika vibaya ikiwa hakutakuwa na jicho la pili. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba; ili kutekeleza dhana ya utawala shirikishi; iwe ni lazima Waziri kushauriana na Mwenyekiti wa Bodi, kabla ya kufanya mabadiliko yoyote chini ya Ibara ya 7(7). Hii itasaidia kuleta ufanisi katika Shirika. Ifahamike kwamba mashirika mengi yanashindwa kuwa shindani kutokana na kutegemea uamuzi unaofanywa na mtu mmoja.

Mheshimiwa Spika, halikadhali kifungu cha 9(1) kinampa Waziri mamlaka ya kutoa maagizo au maelekezo kwa Bodi juu ya mambo ya jumla au jambo mahususi kuhusu utekelezaji wa kazi za Shirika na Bodi itatakiwa kutekeleza maagizo hayo kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua umuhimu wa Waziri kutoa maelekezo ya jumla. Tafsiri rahisi ya kifungu hiki ni kwamba; lazima Bodi itekeleze maelekezo hayo. Kuibana Bodi kwamba lazima itekeleze maagizo ya Waiziri, ni kunyima uhuru wa kufanya kazi. Kwa kuwa mwisho wa siku Bodi ndiyo itakayopimwa juu ya mwenendo wa Kampuni, basi Bodi ihukumiwe kwa kwa utendaji wake. Mstari wa mwisho katika kifungu cha 9(1) unainyima kabisa Bodi meno ya kufanya maamuzi.

7. SIFA ZA KUWA MKURUGEZI MKUU WA SHIRIKA LA MAWASILIANO LA TAIFA

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 15 (3) (b) cha Muswada huu, mbali na kigezo cha elimu, kinaelekeza kwamba ili mtu awe

na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano la Taifa ni lazima mtu huyo awe na uzoefu wa miaka nane (8) katika ngazi ya juu ya utawala.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba huku ni kuwanyima fursa Watanzania wenye weledi na uwezo wa kuongoza taasisi zetu; na pia inaleta taswira mbaya kwamba; pengine kifungu hiki kimewekwa kwa hila ili kumzuia mtu fulani asipate nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, wako Watanzania wenye elimu nzuri kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 15(3) (a) na wana uwezo mzuri kiutendaji. Kambi Rasmi haipingi umuhimu wa uzoefu, lakini uzoefu huo usiwekwe juu mno kiasi cha kufanya watu wenye taaluma husika na uzoefu wa miaka miwili au mitatu (ambayo kwa mtazamo wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni unatosha) kwa lengo baya la kuwaengua watu wenye sifa za kuongoza Shirika.

Mheshimiwa Spika, ukizungumzia uzoefu wa miaka nane; katika ngazi ya juu ya utawala maana yake unazungumzia mtu anayekaribia kustaafu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba badala ya kuweka uzoefu wa miaka nane, basi angalau iwe miaka mitano. Hii ni kwa sababu kinachohitajika ni utendaji uliotukuka na rekodi nzuri ya kazi na sio miaka mingi kazini.

8. KUFUTWA KWA SHERIA YA KAMPUNI YA SIMU TANZANIA SURA YA 304 YA SHERIA ZA TANZANIA

Mheshimiwa Spika, ibara ya 26 ya Muswada huu inapendekeza kufutwa kwa Sheria ya Kampuni ya Simu Tanzania, Sura ya 304 ya Sheria za Tanzania, na badala yake kutunga Sheria Mpya ya Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya madhumuni na sababu za kuleta muswada huu, haikuelezwa ni mapungufu gani makubwa yaliyokuwepo kwenye Sheria ya Kampuni ya Simu Sura 304 inayofutwa, yaliyopelekea kutungwa kwa Sheria Mpya ya Shirika la Mawasiliano ya Simu.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, ikiwa Sheria fulani ina mapungufu madogo madogo, huwa Serikali inaleta muswada wa marekebisho ya Sheria hiyo, na siyo kufuta sheria hiyo kwa kuleta muswada wa sheria mpya. Kwa kuwa Serikali imeleta Muswada Mpya, na kwa kuwa Serikali haijaeleza ni mapungufu gani makubwa yanayohitaji kutungwa kwa Sheria mpya katika eneo hili la mawasiliano ya simu; Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulleleza Bunge hili ni sababu zipi zilizopelekea kutungwa Sheria mpya ambazo zisingeweza kutatuliwa kwa kuleta muswada wa marekebisho ya sheria ya Kampuni ya Simu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulihakikishia Bunge hili; ni kwa namna gani Kampuni ya Simu ya TTCL itajiendesha kwa faida katika Shirika ikiwa kwa miaka yote Kampuni hii imekuwa na ufanisi mdogo ukilinganisha na makampuni mengine ya simu.

9. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, Sheria bora ni ile inayotungwa kwa maridhiano kati ya Kambi mbili Bungeni – yaani Kambi ya Serikali na ile ya Upinzani au Kambi ya Wabunge wa Tanzania Bara na Kambi ya Wabunge wa Tanzania Zanzibar kwa Sheria zile zinazohusu Mambo ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria zinazotungwa kwa maridhiano huwa rahisi kuliko zile zinazotungwa kwa ushabiki, ubabe na kwa kiburi cha wingi wabunge wa Kambi moja dhini ya nyingine. Sheria zinazopitishwa kwa namna hiyo, mara nyingi huwa hazivasaidii wananchi, kwa kuwa zinakuwa zimebeba maslahi ya Kambi hizo kuliko maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ni matumaini ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kwamba; Sheria hii inayopendekezwa itapitishwa kwa maridhiano. Aidha, ni mategemeo ya Kambi ya Upinzani kwamba; matakwa ya Katiba ya kutumia idadi ya wabunge

isiyopungua theluthi mbili kutoka Bara na theluthi mbili kutoka Zanzibar yatazingatiwa katika kupitisha sheria hii, kwa kuwa Sheria hii ni ya Muungano

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Willy Qambalo (Mb)
**Kny. MSEMAJI MKUU WA
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI,
KATIKA WIZARA YAUJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO.**
14 Novemba, 2017

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumemaliza mawasilisho, tutaanza sasa na michango, lakini kabla hatujaanza kuchangia niwaombe Waheshimiwa Wabunge ambao wana Katiba wasome Ibara ya 98 yote na nyongeza zote ili kuweka vizuri mjadala humu ndani kufuatia haya yaliyozungumzwa kuhusu ibara hii. Ni vizuri isomwe yote ili tusije tukaanza kuambiana hapa ndani tunavunja Katiba.

Nimeletewa majina ya wachangiaji kutoka Kambi zote zilizopo humu Bungeni. Tutaanza na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka atafuatiwa na Mheshimiwa Saed Kubenea ambaye muda wake watagawana na Mheshimiwa Cecilia Pareso, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum ajiandae. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka!

MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niwe mchangiaji wa kwanza wa Muswada huu. Kwa utangulizi kwanza napenda kushukuru na niseme kwamba, ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa hiyo Muswada huu nimeupitia kwa ukamilifu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kuishukuru Serikali kwamba imeona kuleta huu Muswada, lakini kabla sijafikia hatua ya kujadili, nataka tu niiase tu Serikali kwamba

tatizo letu kubwa sio tu utungaji wa sheria. Jukumu hili sisi kama Wabunge huwa tunalifanya kwa ukamilifu na umakini mkubwa sana, lakini tatizo letu kubwa ni namna gani hizi sheria tunaenda kuzitekeleza hasa kwa wale waliopewa dhamana ya utekelezaji wa sheria hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mtazamo huu, ninavyoiona Serikali ya Awamu ya Tano sasa tunataka kwenda kujielekeza kwenye kufanya biashara kwa sababu mtazamo wa huko nyuma, tulikuwa tumebinafsisha haya Mashirika ya Umma kwa maana kwamba Serikali ilikuwa inajitoa kwenye kufanya biashara ili iweze kusimamia namna ya uendeshaji wa nchi yetu. Sasa kwa mtazamo huu inaonekana kabisa moja kwa moja kwamba tunakwenda kuingia kwenye biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, bado kwa mfano kama hili Shirika la *TTCL* hatujaambiwa ni kwa msingi gani, ni kwa nini shirika hili lilibinafsishwa likauzwa na Serikali katika mauzo ya shirika hili tulipata kiwango gani. Vilevile sasa hivi tunakuja tunaambiwa hili shirika sasa sisi ndio tumenunua hisa za iliyokuwa *Zain* ili shirika hili tuweze kulimiliki kwa asilimia 100, lakini bado hatujapata ufafanuzi ni kwa nini tuliliuza na kwa nini leo tunaamua kulinunua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika uundwaji wa *TTCL*, *TTCL* kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani ilivyosema tunalo tatizo la Serikali kutokuwapa mamlaka kamili wale viongozi au wasimamizi wa mashirika haya. Mara nyingi tumekuwa tunaendesha mashirika yetu haya ya umma kwa kauli ama kwa matamko badala ya kuacha ma-*CEO* wa makampuni haya waweze kuyasimamia kwa weledi. Nikitoe mfano hivi majuzi tu, shirika letu hili jipya la *ATCL*, ndege imesimama kwa zaidi ya dakika 45 eti inamsubiri Waziri fulani hajafika *airport*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaharibu kabisa taratibu za uendeshaji wa mashirika haya na sijui Serikali itaepukaje katika hili shirika ambalo tunaenda kuliunda leo lisiendeshe

kwa matamko kama ambavyo ilitokea huko nyuma. Hii ndio sababu kubwa inayopelekea mashirika yetu kushindwa kufanya vizuri kwenye medani za ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunaletewa Muswada wa kuunda shirika la *TTCL*, lakini ninachoomba Serikali ije na majibu ni kwa namna gani *TTCL* itaweza kushiriki kwenye ushindani uliopo ambao huko nyuma tumeshindwa kutekeleza. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, madhumuni makubwa ya kulifufua hili Shirika la *TTCL*, nasema kulifufua kwa sababu nakumbuka kwamba lilikuwepo, ni kulinda maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake ajaribu kutuainishia ni kwa namna gani tunaweza kulinda hayo maslahi ya Taifa, kwa sababu isiwe kama ambavyo sasa hivi inafanywa kufungia magazeti, kuwafanya watu wasiseme ikiwa ndio miongoni mwa mambo ya kulinda Taifa. Hayo yanaweza yakawa ndiyo ambayo Serikali imeona ndio mambo ya kulinda Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili kwa upande wangu naomba Mheshimiwa Waziri atakaporudi kuhitimisha hoja yake, ajaribu kutufafanulia na kuainisha kuweka wazi ni kwa namna gani shirika hili linakwenda kulinda maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika hili la *TTCL* kama mjumbe wa Kamati nilishawahi kutembelea, tuliingia pale kwenye ile sehemu ya *data center*, lakini kwenye Muswada huu wa sheria sijaona mahali ambapo imetajwa ni kwa namna gani kwamba ile *data center* itatumikaje na hasa kwenye taasisi za Serikali kwamba ni kwa namna gani *TTCL* mmeamua kuitangaza ile *data center* ili iweze kutumika kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, kulingana na ushindani wa kibiashara uliopo, Serikali inatakiwa ituambie ni mtaji kiwango gani wanakusudia kuwekeza kwenye hili

shirika ambalo tunakwenda kuliunda leo la *TTCL*. Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani walitoa msisitizo juu ya namna ya uteuzi, kulikuwa na matatizo sana hapa ya uteuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiongozi anaweza akateuliwa kwa ajili ya kuongoza shirika hili, lakini ni kiwango gani amepewa uhuru wa kuweza kutumia ujuzi na weledi wake, kwa sababu hapa inaonekana kama nguvu kubwa amepewa Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kutoa, hasa kwenye maelekezo kwa Bodi na Bodi imekuwa ni lazima kuyafuata haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku shirika hili litakapokosa kufanya yale majukumu yaliyoafikiwa, atakayehukumiwa ni Mwenyekiti wa Bodi na Bodi yake, hatoweza kusema kwamba ameshindwa kuyafikia hayo majukumu kutokana na maagizo ya Waziri. Kwa hiyo, naomba niendeleo kusisitiza maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba ni lazima hii Bodi tuipe uhuru kamili ili mwisho wa siku tuweze kuihukumu kwa namna ya utendaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika hili la *TTCL* kwa ujumla wake linakwenda kufanya mashindano na mashirika mengine yanayotoa huduma kama hizi. Sasa Serikali imejipangaje namna ya kuiwezesha *TTCL* kuingia kwenye ushindani huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, naomba nitoe angalizo kwa Serikali kulingana na matatizo mengi yanayojitokeza ya Serikali kuingilia mashirika yetu. Naomba kwa dhati kabisa kwamba hili ni jambo ambalo Serikali mnatakiwa mlíchukue kwa umakini sana, kuacha kuingilia utendaji wa mashirika yetu ili tusirejee kule ambako tulitoka, mashirika haya yalishindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ulikuwa mchango wangu kwa leo. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kuchauka. Halafu leo hiyo tai imekumpendeza sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, atafuatia Mheshimiwa Cecilia Paresso, Mheshimiwa Saed Kubenea ajiandae; Katibu, hawa wanatumia dakika saba na nusu kila mmoja.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Muswada huu ambao umewasilishwa mbele yetu siku ya leo, na naunga mkono maoni ya Kambi ya Upinzani ambayo yamewasilishwa hapa. Ni vizuri sana Serikali mkatupa majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuongezea mchango wangu, napenda kwanza watuambie ni kwa nini leo wanatuletea mapendekezo haya ya kutoka kuwa Kampuni ya Simu na kwenda kuwa Shirika la Mawasiliano. Mheshimiwa Waziri hapa ameeleza kwamba Muswada huu sasa unaitoa *TTCL* kutoka kampuni kwenda shirika kwa mambo ambayo ameeleza hapo; moja likiwa ni kulinda usalama wa nchi. Tunajiuliza, ilipokuwa kampuni ilikuwa haiwezi kulinda usalama wa nchi? Jambo la pili, amesema kukuza uchumi; ilipokuwa Kampuni ya *TTCL* ilikuwa haikuzi uchumi, leo tunapobadilisha kwenda shirika ndiyo itakuza uchumi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kutoa huduma za mawasiliano kwa jamii; ilipokuwa kampuni ilikuwa haitoi huduma, leo tunapofikiria kuwa na Muswada wa kwenda kuwa shirika, je, ndiyo itaweza kutoa huduma hizo za mawasiliano kwa jamii? Nadhani kinachokosekana sio ubadilishaji wa sheria kutoka kampuni kwenda shirika, kinachokosekana ni Serikali kutokuziwezesha hizi kampuni ambazo zimeanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* imekufa kwa sababu ilikuwa haiwezesawi na Serikali, haipewi ruzuku kwa wakati, haiboreshwi, haiendani na ushindani uliopo. Kwa hiyo,leo wakituletea tu kusema wanabadilisha, kama hawatahakikisha hilo shirika ambalo leo tunataka kulipitisha

hapa litapatiwa ruzuku ya kutosha, maana yake litaendea kuwa kama ambavyo leo liko katika hali mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo hotuba yetu ya Kambi imesema, tunahitaji pia kuhakikisha namna gani Serikali inatoa ruzuku kwa wakati na kuwepo na vyanzo vya uhakika vya kuwezesha hili Shirika la Mawasiliano la Taifa. Kwa hiyo, ni muhimu sana, pamoja na kuwa na sheria nyingi au sheria tu kwenye vitabu, lakini bila uwezeshaji bila shaka hakuna kitu kitakachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tunapofikiria wananchi wetu waweze kupata mawasiliano kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, ni mawasiliano ya namna gani, yanaweza kuwa *affordable* na wananchi wa *level* ipi na kwa kiwango gani. Kwa hiyo, pamoja na kwamba tunaona tunaanzisha shirika, lakini lazima kuwepo na urahisi wa upatikanaji wa mawasiliano kwa wananchi kule vijijini kuhakikisha mawasiliano yanapatikana kwa wakati na yanaweza kuwa *affordable* kwa kila mwananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe mapendekezo katika Muswada kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha saba (7) kimeelezea *Board of Directors*; napendekeza pale kwenye uwakilishi wa *members* wa *Board of Directors* wameleta mapendekezo kwamba upande wa Zanzibar awepo mwakilishi mmoja kati ya *five members* watakaokuwa kwenye bodi. Kama kweli tunaitambua Zanzibar kama sehemu ya nchi hii, kuwapa nafasi moja sio kuwatendea haki, nafikiri kuwatendea haki ni kuwaongezea nafasi, mbili zitoke Zanzibar na nafasi tatu zitoke Tanzania Bara. Kwa hiyo, napendekeza pale katika kifungu cha saba (7) waweze kuongeza idadi ya wajumbe kutoka Zanzibar kwenye hiyo *Board of Directors*; wawe wawili badala ya mmoja kama ambavyo wameweza kuandika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo, katika ibara hiyohiyo ya 7(7), wamesema pale napenda kuongeza

maneno kwamba *The Minister in consultation with the Board* anaweza ku-*publish* mambo yote ambayo yanaweza kufanyiwa marekebisha. Tusimwachie tu Waziri mwenyewe abebe hili jukumu, lakini Waziri afanye mawasiliano na bodi yake. Sasa kutakuwa hakuna maana ya kuwa na bodi kama Waziri anaweza tu akawa anaamua kila kitu. Kwa hiyo, ni vizuri Waziri anapofanya mambo yoyote yale, ni lazima afanye *consultaion* na bodi yake aliyounda ili kuwepo na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika ibara ya tisa (9), wanapendekeza kwamba Waziri anaweza kuzi-*direct bodies*; ni sawa, anaweza kutoa maelekezo, lakini sheria inasema maelekezo yote yatakayotolewa na Waziri ni lazima bodi ifuate na itimize. Nadhani tusiweke kipengele hiki cha kuilazimisha bodi; Waziri ni mtu, ni binadamu, leo anaweza akatoa maelekezo akiwa kwenye hali ya hasira au ana *frustration* au anatoa maelekezo ambayo mwisho wa siku hayawezi kuleta ufanisi wa shirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tuache kipengele kiseme kwamba kama Waziri atatoa mapendekezo kwa bodi, basi iwe ni bodi kuamua kuyafuata, kusiwepo na ulazima wa kisheria au uhitaji wa kisheria kwamba lazima yale ambayo yatatolewa na Waziri yaweze kufuatwa. Kwa hiyo, napendekeza kwamba kifungu cha tisa (9) kuondoa maneno ya mwisho pale baada ya neno *act* kwamba *and the Board shall give effect to any direction given to it*. Kwa hiyo, ibaki tu maneno ambayo yatasomeka hapo haya mengine yaondoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema haya kwa sababu nimepeleka *schedule of amendment*, naambiwa nimechelewa muda hautoshi wakati kuna mambo mengine ambayo tunaweza kuyapendekeza kwa ajili ya Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pia mapendekezo katika kifungu cha 15; uzoefu katika *appointments* hizi za *Director* wa shirika, kama ilivyosema hotuba ya Kambi ya Upinzani, unaposema miaka nane ni mingi sana,

napendekeza iwe *experience* ya miaka mitano. Tunaangalia *experience*, ndiyo ni jambo moja, lakini kuna uadilifu, kuna mambo mengine mengi sana ya kuweza kuona mtu gani anafaa katika nafasi fulani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kusema awe na *experience* ya miaka nane wakati mtu mwenyewe ni mbovu, hana uadilifu wowote ana upungufu mwingi. Kwa hiyo, tusiweke kwamba ni lazima awe na *experience* ya miaka nane, napendekeza kuwe na *experience* ya miaka mitano kwa huyo ambaye atateuliwa kuwa *Director* wa shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie mchango wangu kwa kuendelea kuisisitizia Serikali kwamba, hatuwezi tu kusema tunabadilisha sheria kila kukicha, leo tunabadilisha sheria hii kutoka Kampuni ya *TTCL* kwenda Shirika la *TTCL* halafu bado tunakuja na sheria nyingine nyingi ikiwemo hizo ambazo tumeshapitisha kwenye Bunge hili ya kuzuia mawasiliano, kudhibiti mawasiliano ya watu, kuzuia watu kutoa maoni yao na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Serikali ni vizuri ikawa *consistency* na mambo inayoyafanya katika utungaji wa sheria. Kama tunatunga sheria hiyo tukilenga kumaanisha wananchi wote waweze kupata mawasiliano kwa kadri inavyowezekana, basi tusije na sheria nyingine ambazo zinaweza kuwa zinanyima uhuru wa watu kupata mawasiliano au kutumia mawasiliano kwa kadri ambavyo yataweza kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Saed Kubenea, atafuatiwa na Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mheshimiwa Mbarak Dau ajiandae.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu-Wataala* kwa

kunijalia afya nzuri na kuniwezesha kuwepo hapa Bungeni kushiriki katika kupitisha Muswada huu muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Simu la Taifa linaloundwa ni zao la Kampuni au Shirika la Posta na Simu ambalo lilikuwepo huko nyuma. Serikali hii imeleta Muswada huu bila kufanya utafiti wa wapi tulipoanguka wakati wa Kampuni ya Simu ya Taifa (*TTCL*). Tulikuwa na Shirika la Posta na Simu, lilikuwa shirika moja lenye nguvu nchi nzima, Serikali ikaligawa hilo shirika wakatengeneza Kampuni ya Simu ya Taifa na Shirika la Posta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo tunarudi kuja kuanzisha Shirika la Simu la Umma bila kuangalia kitu gani ambacho Serikali ilikosea katika kubinafsisha Kampuni ya Simu ya Taifa. Kwa mujibu wa aliyekuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi wakati *TTCL* inabinafsishwa, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, alisema yafuatayo, naomba nimnukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwandosya anasema:-

“Pamoja na nia njema ya kuanzisha Mashirika ya Umma, hatimaye yalikuja kuwa mzigo mkubwa kwa Hazina yetu. Asilimia kubwa yalitegemea ruzuku ya Serikali na baadhi yalikuwa mufilisi. Teknolojia ilikuwa imebadilika sana na ili kuyafufua ingegharimu Serikali na umma wa Watanzania kiasi kikubwa sana cha fedha. Uchumi wa nchi wakati ule usingeweza kubeba mzigo huo, ndipo Chama cha Mapinduzi wakati ule kiliporidhia Serikali ibakie na shughuli zake za msingi za utawala, ulinzi na usalama.” Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyokuwa wakati Kampuni ya Simu inabinafsishwa ndivyo hali ilivyo hivi sasa. Kampuni ya Simu inaenda kuanzisha Shirika la Umma mwekezaji kwa mujibu wa taarifa zilizopo aliyepewa kuendesha *TTCL* kwa hisa asilimia 35, aliposhindwa kuendesha alifanya hujuma ya kung’oa mitambo yote iliyokuwepo katika Chuo cha *TTCL* kilichopo eneo la Kijitonyama Jijini Dar es

Salaam. Alikifunga chuo hicho na kung'oa mtambo wa kutoa ankara kwa wateja ambao kwa mujibu wa wahandisi wa kampuni hiyo ulikuwa bado una uwezo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitegemea Serikali ije na majibu ya hujuma iliyofanyiwa *TTCL* kabla ya kuanzisha Kampuni ya Umma ya *TTCL*, majibu hayo hayajaja. Hakuna majibu kwa nini mwekezaji aling'oa mitambo, kwa nini mwekezaji hakuja na mtaji na kwa nini Serikali inanunua hisa kwa fedha ambazo yenyewe iliweka kwenye kampuni ya simu. Ubinafsishaji mzima wa *TTCL* ulitawaliwa na ulaghai, ubinafsi na mchezo mchafu wa kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya watu waliokuwemo wakati wa ubinafsishaji walichafuliwa majina yao kwa mbio za Urais kwa sababu tu walisimamia kitu ambacho kila mtu alikiona *TTCL* inafilisika. Kwa hiyo, hoja ya Waziri kwamba *TTCL* inaanzishwa ili kutoa huduma kwa umma, *TTCL* iliyopo sasa ni kaburi. *TTCL* haina nyenzo na haiwezi kuingia katika ushindani wa biashara wa sasa hivi. Serikali haina uwezo wa kuweka mtaji mkubwa kabisa wa kuifanya *TTCL* iweze kuingia kwenye ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini hizi hatua zinazofanyika bila kufanya utafiti, tutarudi hapa ndani ya miaka mitano au baada ya miaka mitano na historia itatuhukumu, tutarudi kuja kubinafsisha upya Shirika hili la Umma tunalolianzisha leo. Kwa sababu utafiti yakinifu, katika hotuba nzima ya Waziri hajaeleza Serikali imefanya utafiti wapi ilipokosea na kwa nini sasa inarudi kuja kumiliki shirika lake la umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea kwamba Serikali ingekuja na Muswada wa kuuza hisa za *TTCL* kwa wafanyakazi wa Kampuni ya *TTCL* ambao wamelitumikia Taifa hili na shirika lao tokea lilipoanzishwa baada ya kuvunjwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, lakini Serikali inasema inamiliki hisa asilimia 100 bila kuwa na mipango endelevu ya kulikokoa Shirika hili la Simu la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo matatizo yaliyokuwepo kwenye uwekezaji, Waziri, kampuni ya *MCI* ambayo ndiyo ilikuwa wamiliki wa hisa asilimia 35 za *TTCL* waliuziwa hisa hizo kinyemela, mchakato haukufuata utaratibu na waliahidi kujenga njia za simu 800,100 pamoja na kulipa dola za Marekani milioni 120. Fedha hizo hawakulipa na njia za simu hawakujenga na Serikali ikatoa fedha nyingine kununua hisa zenye za *TTCL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji alitakiwa kuonesha waziwazi zabuni ya kununulia asilimia 35 za hisa za *TTCL*, pamoja na kueleza njia watakazofunga katika kipindi cha miaka minne hadi mwaka 2003. Kampuni inayoshinda zabuni haikuweza kufanya yote ambayo walikubaliana katika mkataba, lakini Serikali iliendelea kumbeba, kumkumbatia na kumpakata mwekezaji wakati ameshindwa kulinda masharti yote ya mkataba wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Serikali inatoa fedha za umma ambazo zilipaswa kwenda katika vijiji vyetu kulipia umeme, kulipia maji, kuhudumia wananchi wetu, lakini zinatumika kununua hisa ambazo ni mali ya Serikali. Jambo hili sisi hatulungi mkono, pamoja na nia njema iliyopo lakini tunafikiri kwamba ni lazima tungeanzia pale ambapo Serikali iliishia, ilishindwa kuliendesha shirika hili.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kubenea, muda wako umekwisha.

MHE. SAED A. KUBENEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na naunga mkono hoja ya Kambi ya Upinzani.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Kubenea, hapa hoja huwa ni moja tu, kwa hiyo, umeunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, haya mengine huwa ni maoni. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji; Mheshimiwa Saada

Mkuya Salum, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Dau na Mheshimiwa Deo Ngalawa ajiandae.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata fursa hii ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano. Kwanza kabisa, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai pamoja na afya na kuweza kufika hapa kuendelea na majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii, hasa kwa sababu Serikali inaji-*tune* katika mabadiliko haya ya kiutendaji kazi. Maana yake tulipokuwa Bungeni kipindi kilichopita mara nyingi tulikuwa tunapata maelezo ni jinsi gani Serikali inataka kujitoa katika ule ubia pamoja na *Bharti Airtel* na kuwa shirika hili liwe *owned a hundred percent by the Government* na maoni mengine hatayalitoka upande wa pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nadhani sasa Serikali imekuja na majibu na naipongeza sana kazi iliyokuwa imefanywa na Serikali ya Awamu ya Nne kuhakikisha kwamba tunatoka kwenye ule ubia na sasa shirika letu linakuwa *owned by the Government a hundred percent.* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunampongeza vilevile *CEO* wa *TTCL*, ndugu Waziri Kindamba ambaye anafanya kazi nzuri *as occurence* na nadhani huwa anakuja na *ideas* nyingi sana katika mazingira haya ya kidijitali pamoja na kimawasiliano. Tunampongeza na tunamwomba sana aendelee na jitihada zake za kutaka kubadilisha utendaji mzima wa *TTCL.* (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia hasa upande wa *operations* kwa sababu tumeulizia, kwa sasa hivi hatuwezi tena kuleta *amendments*, kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Waziri ayachukue haya ambayo nitayasema ili ayafanye kazi katika *operations* zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza hili ni shirika la Muungano, *application* yake ni Tanzania *Mainland as well as to* Tanzania Zanzibar, kwa hiyo, tunaomba katika sura ya uongozi, shirika hili liwe katika sura ya Muungano. Tunaomba sana shirika hili upande wa Zanzibar kuwa na *may be Resident Director* au mtu mkubwa ambaye atakuwa ana-*coordinate* upande wa Zanzibar na awe ni Mzanzibari kwa ajili ya *ku-create ownership* lakini vilevile kwa ajili ya kupata *support* kubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu *TTCL* kwa upande wa Zanzibar ina-*serve* taasisi za Serikali lakini vilevile kuna Balozi ambazo zinafanya kazi zake Zanzibar na Mashirika ya Kimataifa na asilimia kubwa inategemea sana *TTCL*. Kwa hiyo, tunaomba sura ile ya kiuongozi iwe ni sura ya Muungano kwa vitendo siyo kwa maneno. Tunaomba kuwe na Mtendaji Mkuu ambaye atakuwa Zanzibar, awe ni Mzanzibari lakini vilevile labda tunaweza tukagawa kwa *zone* baina ya Unguja na Pemba. Hiyo ita-*create ownership* lakini vilevile ita-*create* utendaji mzuri wa *TTCL* kwa upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili hata suala la ajira, kuna vijana wengi Zanzibar ambao wanamaliza *technical colleges* na ni weledi lakini *when it comes to* ajira hata ukitaka ku-*apply TTCL* lazima waje *headquarters*. Tunaomba sana kwa upande wa Zanzibar shirika hili lipewe *mandate* ya kuweza kuajiri vijana ili waweze kufanya kazi katika shirika lao ambalo lipo upande ule wa pili wa Jamhuri. Hatuwezi kuyaingiza hapa haya lakini katika masuala yote ya kiutendaji Mheshimiwa Waziri tunaomba sana alisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar, watendaji ni wazuri mno, mimi nyumbani natumia *TTCL*, *once* ikiwa kuna *any fault* ukiwapigia simu tu kwamba kuna tatizo, wale watendaji wanaharaka kuja kuangalia tatizo liko wapi lakini wanatumia vifaa duni mno. Katika barabara za ndani za Zanzibar ukiona *TTCL* wanakuja na ile, *what they call it*, bajaji, ngazi, wakati sasa hivi tuna *revamp operation* za *TTCL*, tunaomba kwa upande wa Zanzibar tufikirie vilevile na vifaa.

Wana vifaa duni vya kufanyia kazi wao wenyewe ni weledi, ni mahodari, wanajituma kwa nguvu zote lakini *when it comes to* vifaa bado vifaa vya kufanyia kazi ni duni, tunaomba hili Mheshimiwa Waziri aliangalie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL operation* zake mara nyingi sisi ambao tuna *-rely on TTCL with data* na vilevile *voice* kuna *-breakdown* ya mara kwa mara na ya muda mrefu. Unaweza ukakaa siku nne au tano usipate *data* na wala huwezi kupata hata *voice*. Sasa unaulizia unaambiwa labda mtambo uliharibika, sasa saa nyingine wanakuwa hawana uwezo nalo kwa sababu siyo jambo ambalo limeharibika *local*, mara nyingi inakuwa ni *network* nzima. Kwa hiyo, tunaomba sana katika marekebisho haya ya kiutendaji lazima tuangalie hili suala la *breakdown* ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye *service delivery*, kama nilivyosema, tunaomba *TTCL Zanzibar* iwe *treated* kwa *major areas* kama inavyokuwa Dar es Salaam na Dodoma kwa sababu Zanzibar ile *TTCL* ina-*serve* taasisi za Serikali lakini vilevile Mashirika ya Kimataifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kuna jambo moja amelisahau, hii ni *Bill* ambayo ita-*apply* kote lakini tumesahau ku-*define government*. *Application* ya *government* hapa ni muhimu kwa sababu kuna *infrastructure ownership* kama ambavyo imetafsiriwa kwenye ukurasa wa sita ile ya *support core network* yaani ni *ownership* ya *infrastructure* yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke kwa upande wa Zanzibar kuna *fiber optic which is not part of this*. Kwa hiyo, naona kama inaweza ikaleta mkanganyiko. Kwa hivyo, hebu atakapokuja kujibu hizi hoja tunaomba a-*define, fiber optic* ya Zanzibar *is not part of this infrastructure* ieleweke hivyo na kwamba hii sheria isije ikakanganya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusiana na *Board composition*, kuna mtu amezungumza kwamba hili ni Shirika la Muungano lakini nadhani kuna hii *tendency*

ya kufikiria kwamba Shirika la Muungano kwenye *Board of Directors* una-*qualify at least one member representative from Zanzibar*. Hivi huwa najjuliza, *why at least one member?* Hili ni Shirika la Muungano *why should not be two?* Kwa nini wasiwe wawili? Yaani mtu mmoja ndiyo atakuwa ana-*represent Zanzibar*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani huu mwelekeo tuangalie zaidi inaleta sura ambayo siyo nzuri sana katika mustakabali mzima wa Muungano. Mheshimiwa Waziri aliangalie hili, siwezi kuleta marekebisho lakini naamini hii *at least one member should be at least two members, why one?* Tunaomba suala hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile limesahauliwa jambo moja muhimu, *the way* ilivyokuwa *qualified* hakuna *gender consideration*. Tunaomba kwenye mambo ya teknolojia kama haya, wanawake sisi ndiyo tuko mbele kweli kweli. Lazima liangaliwe kwenye masuala ya *management*, teknolojia tuko mbele, tunaweza kweli kweli. Tunaomba sana *gender equality* iwe-*considered* katika hii *Board composition*. Suala la Zanzibar, suala la *gender* tuangalie kwa makini kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo limeonekana vilevile kuhusiana na hizo *directions* ambazo *Minister may give to the Board* naona tuache *Board* iwe inafanya kazi yake *rather than to accept directions from the Minister*. Kama tukiiacha *Board* ikawa inajiendesha itaweza ku-*compete* katika mazingira haya magumu, *very complex* ya kiteknolojia, lakini mara kwa mara Mheshimiwa Waziri akiwa anaingilia na anaweka *directions to the Board* *how to operate* hii *cooperation* nadhani halitakuwa ni jambo la buasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi maneno yangu yalikuwa ni machache lakini naomba sana Mheshimiwa Waziri ayazingatie katika *positive outlook* kwa sababu tunaweza sana tukajichanganya kwenye *operation* zetu. Tunaomba sana, *TTCL* kwa upande wa Zanzibar inafanya kazi

nzuri lakini ipo katika mazingira magumu kiutendaji. Ajira zifikiriwe, *TTCL* Zanzibar iajiri wenyewe Wazanzibari ambao wana sifa kuingia kwenye *TTCL* kwa sababu ita-*create ownership* na vilevile itaweza kufanya kazi nzuri kwa sababu itakuwa ina-*serve* Serikali lakini ina-*serve* mashirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaona sana jitihada za *TTCL* kwenda kwenye *underserved areas*. Sehemu ambapo kampuni binafsi hazipo ni lazima Serikali iingine huko *through TTCL*. Kuna sehemu nyingi Tanzania ambazo hazina mawasiliano ya simu, ni *challenge* lakini kwa *TTCL* ichukue kama ni *opportunity* ya kwenda kuwekeza huko kwa sababu ya kibiashara lakini vilevile kwa sababu hii ni *social service*, wananchi wanapenda kuona Serikali inafanya kazi. *TTCL* nadhani ina *composition* kubwa ya *fixed landline* na hii ni *advantage*, tunaomba sana tutafute *new subscribers* wa *landlines* kwa sababu *TTCL is almost monopoly* kwenye suala hili la *landline*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile kwa sababu ya *growing demand*, tunataka tubadilishe huu mwelekeo wa *TTCL*. Katika *business plan* yetu ambayo tutaitengeneza ama imeshatengenezwa tunaomba tufikirie suala la sisi viongozi kui-*support TTCL*. Kwa mfano, kama tunataka *TTCL* i-*grow* kama ni kampuni ya nchi ni lazima na sisi tuwe tuna-*stake* maana yake inawezeka katika *business plan* tukaangalia tu unakuta watu wana simu mbili, tatu, nne pengine hakuna hata moja ya *TTCL*. Tungefikiria *at least* simu moja katika simu tano ambazo unazo mojawapo iwe ya *TTCL* ili kuweza kuliweka shirika letu katika hali nzuri kimapato na liweze kuwa *competent* katika mazingira haya ya kiteknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Saada Mkuya Salum. Sasa kwa sababu mengi umetoa ushauri wa kiutendaji labda utusaidie kufafanua jambo moja kidogo kwa ajili ya kuweka mambo sawa.

Umependekeza kwamba huko Zanzibar kama kutakuwa na *Resident Director* awe Zanzibar na pia umependekeza kwamba watakaojiriwa kwenye hilo shirika ambalo ni la Muungano kwa upande wa Zanzibar wawe Wazanzibari. Sasa hili shirika kama ni la Muungano, ofisi zake upande wa Bara, yule atakayekuwa Mkurugenzi hatakiwi kutoka Zanzibar ama waajiriwa wengine pia watakaokuwa upande wa hii Jamhuri nyingine hawatakiwa pia kutoka Zanzibar, kwa sababu upande wa Zanzibar utakuwa na Wazanzibari peke yao, upande huu wa Bara utakaaje?

Naomba maelezo ili likae vizuri na hawa waangalie namna ya kwenda kulifanyia kazi huko wakati wa kufanya hizo *operations* ulizopendekeza.

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nilichokuwa nimependekeza, kwa sababu sasa hivi tunaona haya mashirika ya Muungano hata yule aliyekuwepo Zanzibar mara nyingi anakuwa hatoki Zanzibar *most of the time. I have a very good example* wa TCRA yupo na anafanya kazi lakini kwa sababu ya *ku-create ownership* katika *competition* kama ya Zanzibar tunaomba awe Mzanzibari ili aweze kufanya kazi katika mazingira yale pale *rather than* mtu mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemshauri Mheshimiwa Waziri hata wakati wa *ku-create* ajira, ziwe zinafanyika Zanzibar kwa sababu mara nyingi wanapokuja upande mwingine wale ambao hawana uwezo wa kusafiri lakini wana-*qualifications* hawawezi kupata nafasi hii. Vyovyote atakavyofanya Mheshimiwa Waziri lakini hilo na lenyewe alizingatie siyo lazima iwe *100%* lakini *at least* kuwe kuna *component* ya Wazanzibari katika suala zima la *corporate structure* kwa upande wa Zanzibar.

NAIBU SPIKA: Haya Serikali nadhani kazi kwenu. Hili kwa kweli ni kazi kwenu, sijui mtapanga vipi hiyo *structure* lakini ndiyo ushauri huo mmepewa. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na uchangiaji, Mheshimiwa Mbaraka dau atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mheshimiwa Richard Mbogo kama muda utakuwa bado unatoshia utafuata.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushuru kwa kunipa fursa hii ili na mimi nichangie Muswada huu muhimu uliopo mbele yetu.

Mhshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana mtoa hoja Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwa kutuletea Muswada huu ambao kwangu mimi nauona kama umekuwa ndiyo *overdue*, tulikuwa tukiusubiri kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Profesa hapa amesema tunalirudisha shirika hili kwenye miliki ya umma kwa sababu kubwa tatu kama zilivyoelezwa hapa; sababu za kiuchumi, kiusalama na kijamii. Napenda nianze mjadala wangu kwa ku-*combine* yote matatu kwa pamoja. Ni kweli na nianze kwa kusema mapema tu kwamba naunga mkono hoja hii kwa umuhimu wake na kutokana na hizi nukta tatu muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usalama, uchumi na kijamii kwa Shirika kama la *TTCL* ambalo mwanzo lilikuwa ndani ya Serikali baadaye likatiwa katika mipango ya kubinafsishwa na sasa linarudi Serikalini ni muhimu sana. Hata hivyo, nina *some reservations* kwenye mpango huu. Kwangu mimi hili ni shirika la kimkakati lakini naona kama mazingira ambayo tunaanza nayo pengine yanaweza yakawa ni mazingira ya kulifanya hili shirika lisifanikiwe kama lilivyoshindwa huko mwanzo. Sasa ni muhimu haya mambo tukayangalia kama nilivyosema nitayazungumza yote kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *brand* kubwa za *TTCL* ni Mkongo wa Taifa, *Data Center* pamoja na huduma hizi za mawasiliano. Kwa masikitiko makubwa sana Serikali tuliwekeza pesa nyingi sana kwenye Mkongo ule wa Taifa na

ukasambaa karibu nchi nzima lakini kwa bahati mbaya sana tukaruhusu tena na watu binafsi nao wakajenga mikongo yao *parallel* na Mkongo wa Taifa. *Halotel* wana *network* kubwa sana ya mkongo. Haya mashirika mengine wanajiita *consortium; Vodacom, Tigo* pamoja na *Airtel* na wenyewe nao pia wana mikongo yao ambayo ni kama *missing link* inajazia kwenye ule Mkongo wa Taifa. Sasa wasiwasi wangu ni kwamba hizi *infrastructures* na hili suala la usalama hapa ndipo linapokuja mahali pake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani na naomba Mheshimiwa Waziri achukue ushauri huu kwamba hizi *infrastructures* hususani huu Mkongo wa Taifa lazima wote urudi Serikalini, hatusemi kwamba tunabinafsisha mashirika, tunabinafsisha zile *infrastructures*. Ukisharudi Serikalini, *TTCL* atakuwa na miguu ya kufanya kazi lakini tumewekeza kwenye mkongo na kwa bahati mbaya sana tukaruhusu na watu binafsi nao wamewekeza kwenye mkono, huu mkongo wa *TTCL* unakuwa *redundant*, matumizi yake ni madogo na mapato kutokana na matumizi ya huu mkongo yatazidi kushuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kama itawezekana tuangalie namna gani Kampuni kama za *Halotel* na ile mikongo ya ule ushirika wa *Tigo, Vodacom* pamoja na *Airtel* na yenyewe nayo pia tufanye utaratibu irudishwe Serikalini. Kwa kufanya hivyo tutaanza vizuri na *TTCL*. Kwa sababu katika hali ya kawaida, mkongo ni *product* kama vile unavyoona viwanja vya ndege, huwezi ukawa na kiwanja cha ndege cha *private sector*. Ni vizuri sana mikongo yote pamoja na *extension* zake zitakazofanyika zije kwenye umiliki wa Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu *Data Center*, hii ni *another product* ya *TTCL*. Nakumbuka kulikuwa na agizo la Mheshimiwa Rais hapa kwamba makampuni yote ya simu yaanze kutumia ile *International Data Center* yetu ambayo inamilikiwa na *TTCL*...

MBUNGE FULANI: Tarehe 1 Juni...

MHE. MBARAKA K. DAU: Ilikuwa tarehe 1 Juni, nakumbushwa, lakini mpaka leo sijui labda Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuja kujibu hapo atuambie ni makampuni mangapi yame-*comply* na hii kitu sambamba na hilo na mabenki nayo pia wanatumia hii *data center* kwa sababu tumewekeza pesa nyingi sana pale. Haiwezekani ikawa tunaruhusu tena na watu wengine wanajenga na vi-*data center*vyao vingine *parallel* na ile *data center* ambayo Serikali tumejenga kwa gharama kubwa sana na lilikuwa ni agizo la Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nitoe tu ushauri wa ziada wa namna ya kuifanya *TTCL* isimame kwa miguu yake. Ni muhimu sana kama ambavyo tulivyojadili katika Bunge la bajeti hapa, *TTCL* iongezewe mtaji. Nina wasiwasi mkubwa sana isije ikawa unamchukua mtu ambaye hajui kuogelea ukampeleka katika kina kikubwa cha maji ukamtosa, halafu ukamwambia tukutane juu anaweza akafia njiani. *TTCL* ni mtoto wa Mheshimiwa Waziri, wahakikisheni kwamba ile *commitment* ya Serikali ya kuongeza mtaji pale ili aweze kushindana na makampuni mengine ni muhimu sana sambamba na lile ambalo walilolisema wenzangu la kuuza hisa katika soko la hisa ili kuitunisha mtaji wa *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hili ambalo wazungumzaji wengi wamelizungumza la *composition* ya *Board ya Directors* pale. Hata mimi pia naunga mkono ile *part* ya Zanzibar kama ile *Board* itakuwa na watu watano basi wawili watoke Zanzibar na watatu watoke Tanzania Bara ili kuleta sura nzuri ya Muungano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni uendeshaji wa shirika kwa maana ya Mkurugenzi Mkuu pamoja na Bodi yake tuwape uhuru. Mengi yamesemwa hapa sina haja ya kuyarudia, kama tunataka kulifufua hili shirika tuwaachie Mkurugenzi Mkuu na bahati nzuri tuna Mkurugenzi Mkuu mzuri sana, apewe mamlaka pamoja na Bodi yake waweze kufanya kazi bila ya kuingiliwa ili kuhakikisha kwamba Shirika letu hili linasonga mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo nimalizie kwa kusema naunga mkono hoja na nashukuru sana kwa fursa hii, ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Ngalawa kama muda utabaki tutamsikia Mheshimiwa Richard Mbogo.

MHE. DEOGRATIUS F. NGALAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuchangia Muswada huu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania. Kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Mawaziri na timu zao kwa namna nzuri ambavyo wameuwasilisha Muswada huu. Muswada huu ni muhimu sana kwa namna ambavyo umeelezwa, kwanza kwa ajili ya usalama na ulinzi, pili kukuza uchumi na tatu kwa ajili ya masuala ya kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* ilikuwa tayari imeshazama, kwa hiyo mpango ambao Serikali imeuleta ni mzuri. Pamoja na Waheshimiwa wenzangu wote kuchangia lakini mimi kubwa najikita katika masuala matatu. Suala la kwanza liwe ni suala la mtaji, la pili miundombinu na pia wakati mwingine lazima tuziangalie hizi sheria zetu hasa tunapoyapeleka mashirika ya umma kwenda ku-*compete* na mashirika mengine. *TTCL* inatakiwa kupewa mtaji, ikishapewa mtaji naamini kabisa ni shirika ambalo linaweza likafanya kazi yake vizuri na likapeleka gawio Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mtaji siyo lazima utoke *direct* kwenye Serikali lakini bado Serikali ina uwezo wa kutoa *guarantees* na kulifanya hili shirika liweze kusimama na kujiendesha kibiashara. Kipindi kile *TTCL* ilikuwa haiwezi sana ku-*move*, inawezekana ni kwa sababu tu ya mwingiliano wa maslahi ya kibiashara, kwa sababu kuna *component* ambapo *Airtel*/naye alikuwa tayari ni *shareholder* pale wakati wanafanya *the same business*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hali kama hiyo shirika lisingeweza kwenda kwa sababu kuna mdau mwingine

ambaye alikuwa ndani ya *TTCL* yenyewe na yeye anafanya biashara ambazo zinafanana lakini sasa hivi huyo mdau hayupo. Kwa hiyo naamini kwa sababu ya shirika kuwa ni asilimia 100% *government ownership* lina uwezo wa kwenda na ku-*compete* kama ambavyo yanafanya mashirika mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, limezungumziwa suala la Mkongo wa Taifa. Mkongo wa Taifa ni mali ya Serikali kwa hiyo katika hali ya kawaida huu Mkongo wa Taifa kwa sasa kwa namna tunavyokwenda apewe *TTCL* moja kwa moja ili aweze kuimarisha hiyo miundombinu na aingie kwenye soko akiwa tayari ana nguvu za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo ilo eneo la *Data Center* kwa sababu ni mali ya Serikali hatuna sababu *TTCL* isipewe umiliki wa moja kwa moja *Data Center* hizo. Vilevile tuangalie hizi *Data Center* ambazo zinaanzishwa nje ya ule mfumo wa *Data Center* ya Kitaifa, naamini kwamba Serikali ina nguvu na uwezo wa kutosha kuhakikisha ina-*control* hiyo na wote ambao wanatumia *data* wakatamia *data* hizi za *TTCL* ili mwisho wa siku ziweze kwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hii Sheria ya *Procurement*, *TTCL* sasa hivi anaenda kwenye ushindani, hawa wenzake hawana viziwi katika kufanya *business* na katika kuagiza baadhi vifaa ambavyo vinaweza vikafanya waweze ku-*dominate* soko la biashara. Kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia kwa maana ya kutoa *exemption* fulani fulani katika hii Sheria ya *Procurement* ili kuifanya hii *TTCL* iweze kufanya biashara yake *smoothly*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la sivyo wakati wengine wana uwezo wa kuagiza vifaa na *components* zozote bila kizuizi chochote sisi wakati tunaiwekea kizuizi kampuni yetu ya *TTCL*, naamini kabisa uwezekano wa kuingia kwenye *competition* na kudumu kwenye soko utakuwa ni mdogo. Hatukatai kwamba hii sheria ipo, ni kweli ipo lakini kwenye baadhi ya maeneo ambayo tunaona kwamba inaweza ikawa ni kipingamizi au kizuizi cha kufanya biashara yake

vizuri basi *TTCL* apewe hizo *exemptions* ili aweze kufanya hiyo biashara ili mwisho wa siku ijiendeshe kwa faida na Serikali ipate gawio lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo upungufu ambao *TTCL* ya sasa inayo na naamini upungufu huo ndiyo uliopelekea kubadilishwa kwa sheria. Upungufu wa kwanza ni kwamba mdau aliyekuwepo ndani alikuwa na yeye ni mshindani kwenye biashara. Kwa hiyo, kutoweka kwake ndiyo maana sasa tunaita ile sheria ya kwamba kwa nini tunatoka sasa kwenye kampuni kuja kwenye shirika? Tunatoka kwenye kampuni kuja kwenye shirika kwa sababu ni 100% *government ownership*, ni jibu rahisi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine tunapokuwa tunazungumzia biashara, biashara inafika kipindi inakuwa na kikomo, biashara inategemea mazingira, jibu linakuja kwamba mazingira ya sasa hairuhusu *TTCL* kujiendesha kama inavyojiendesha na ndiyo maana Serikali inaleta Muswada huo. Kwenye *business life cycle*, *business* inapitia *challenges* nyingi, sasa hatuwezi kubaki *stagnant* eti kwa sababu tu kwa nini ulianzisha vile, kwa nini ulianzisha vile, teknolojia imebadilika, mazingira ya ufanyaji biashara yamebadilika na ndiyo maana na sisi sasa tunapaswa kubadilika ili tuweze ku-move. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilikuwa haiwezi kutoa mchango wake kwa sababu kulikuwa na *percentage* kwenye *share*, hilo nalo limepelekea Serikali kuleta Muswada huu kwa sababu huwezi kupeleka tu kama unavyotaka wakati huo kuna mwingine mnaye pale mnapaswa mjadiliane. Kwa hiyo, inategemea wakati mwingine mnaweza mkawa na *convincement power* ya namna gani ili kuweza kumshawishi mbia muweze kwenda sawa. Sasa hivi ni 100% *government ownership*, kwa hiyo inaweza ikatengeneza bila kuhujumiwa na mtu mwingine yeyote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna mamlaka au madaraka au uhuru usiokuwa mipaka. Nakubali *CEO* na Bodi

yake ifanye kazi kwa uhuru, lakini lazima kuwepo na *scenario* ambayo Serikali kama mwenye kampuni aweze kuona nini kinachoendelea. Mimi siamini kwamba Waziri atakuwa kazi yake kuleta *directions* tu kwa Bodi au *CEO* na atakuwa anafanya hivyo kwa sababu ya kupewa ushauri fulani fulani. Kwa hiyo, naamini ile *component* pale ya Waziri iendelee kuwepo kwa maana Waziri ndiyo aliyepewa mamlaka na Serikali katika kuhakikisha kwamba anahakikisha ile taasisi inakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna uhuru usiokuwa na mipaka ila ijaribu tu kuangaliwa kwamba ule uhuru au ile dhamana ambayo Waziri anayo ifanyiwe marekebisho kiasi ambacho haitaifanya kampuni iweze kutetereka au kurudi nyuma katika kufanya biashara zake za kila wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niishie hapo, lakini niendelee kusesitiza tu taasisi hii inayokuja ni lazima ipewe mtaji, taasisi inayokuja ule Mkongo wa Taifa uumiliki kwa 100%, *Data Center* imilikiwe na *TTCL* na taasisi zote za kiserikali zitumie *data* za *TTCL* kwa sababu *TTCL* ni baba na mama wa hivyo vitu. Kwa hiyo, inapokuwa kwamba wewe mwenyewe unayo taasisi ambayo inafanya kazi hiyohiyo halafu wewe ni mmoja unatoka unaenda kufanya kazi kwenye taasisi nyingine nadhani haiwi nzuri sana. Nipende kushauri kwamba taasisi zote za kiserikali, taasisi za umma zitumie *TTCL* katika matumizi yake ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda uliobaki hazitatimia dakika 15 za kuchangia kwa Mheshimiwa Richard Mbogo, kwa hivyo tutaanza naye tutakaporejea jioni na kutakuwa na wachangiaji wengine watatu.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijawasoma majina nieleze kidogo kuhusu ushauri uliotolewa na Mheshimiwa Saada Mkuya. Pamoja na mambo mengine, Katiba yetu inaweka utaratibu wa namna ya kufanya mambo na sisi

kama Bunge lazima tufuate utaratibu huo. Kwa hivyo, michango yetu lazima izingatie Katiba na sheria zinasemaje. Nasema haya kwa sababu Wizara imeshauriwa namna ya kwenda kufanya kitu ambacho hatutapata fursa ya kujadili hapa ndani, humu ndani huwa hatujadili utendaji wa Wizara mojamoja, kazi yetu ni kutunga sheria na kuwashauri hapa na pale.

Shirika hili la Mawasiliano linaloundwa na huu Muswada ambao tutapitisha leo kuwa sheria kama tukiamua kupitisha ama kama tutakaa hilo litakuwa suala lingine, lakini kama tutaupitisha Wizara lazima iangalie kwamba ushauri uliotolewa humu ndani na Waheshimiwa Wabunge hili si shirika pekee ambalo ni la Muungano. Kwa hivyo, lazima muangalie sheria nyingine zinasemaje kuhusu mashirika mengine ili shirika hili lisije likajikuta lipo katika mazingira ambayo limeanzisha utaratibu ambao haupo kwenye maeneo mengine.

Waheshimiwa Wabunge, nasema hivi kwa sababu sheria nyingi tu za mapato zimeeleza tutagawana vipi na kuna nyingine ambazo zimeweka mgawanyo wa hivi vyeo. Kwa hiyo, lazima mziangalie na hizo si kuangalia hili shirika kana kwamba ndiyo tunaanza kullitengeneza ni la kwanza na kana kwamba litakuwa la mwisho.

Haya mambo yote tuyaangalie maana wengi wetu pengine tunaweza kuwa mengine hatufuatilia, lakini wale Wabunge wa zamani humu ndani na wengine ambao tulipata fursa ya kuwepo mambo mengi sana yalitokeza wakati wa kutengeneza Katiba mpya na wote nadhani ni mashahidi na mnayakumbuka.

Kwa hiyo, tusifike mahali ambapo Bunge hili litakuwa likifanya mambo ambayo wenyewe tumeyapitisha lakini tunataka kwenda tofauti nayo. Kwa hiyo, Waziri utakapokuja kujibu hoja na wachangiaji wengine watakaomendelea tutahitaji jambo hili liwekwe vizuri, hatutataka Bunge lijikute katika mazingira ambayo tutakuwa sisi wenyewe ni wa kwanza kuvunja yale ambayo tumeyaweka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, ninalo tangazo hapa kutoka kwa Mheshimiwa Spika, kuhusu mabadiliko madogo ya ratiba ya Mkutano wa Tisa wa Bunge na mabadiliko haya baadaye mtaletewa karatasi lakini kwa wale wanaotaka kuandika wanaweza kuandika.

Mheshimiwa Spika ameagiza niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba amefanya mabadiliko madogo kwenye ratiba ya Mkutano huu wa Tisa wa Bunge kama ifuatavyo:-

(i) Kesho Jumatano tarehe 15 Novemba, 2017, kutakuwa na Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 4 wa Mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments No. 4) Bill, 2017*), badala ya Muswada ya Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania wa Mwaka 2017 (*The National Shipping Agencies, Bill 2017*)

(ii) Siku ya Alhamisi tarehe 16 Novemba, 2017 kutakuwa na Muswada wa Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania wa Mwaka 2017 (*The National Shipping Agencies Bill, 2017*) badala ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevywa ya Mwaka 2017 (*The Drugs Control and Enforcement (Amendment Bill), 2017*)

(iii) Siku ya Ijumaaa tarehe 17 Novemba, 2017 kutakuwa na Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevywa wa Mwaka 2017 (*The Drugs Control and Enforcement (Amendment) Bill, 2017*) badala ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na.4 wa Mwaka 2017 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) No.4 Bill, 2017*)

Waheshimiwa Wabunge, lengo la marekebisho haya ni kutoa nafasi kwa Kamati ya Miundombinu kuweza kukamilisha kazi ya kuchambua Muswada wa Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania wa Mwaka 2017. Kwa hiyo, marekebisho ni haya yaliyofanyika kwa maana ya kubadilisha tarehe za Miswada hii ya siku itakayoingizwa hapa Bungeni.

Kwa hiyo mtaletewa hayo mabadiliko ili Waheshimiwa Wabunge muweze kujiandaa ipasavyo mkijua ni Muswada gani unafuata.

Wachangiaji wetu wa mchana tutaanza na Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Hussein Bashe na Mheshimiwa Peter Serukamba.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 12.55 Mchana Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitudia)

NAIBU SPIKA: Tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na uchangiaji. Tutaanza na Mheshimiwa Richard Mbogo, atafuatiwa na Mheshimiwa Salome Makamba na Mheshimiwa Hussein Bashe ajiandae.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na pia namshukuru Mungu kwa namna ya pekee ambavyo tumeweza kufika siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono mabadiliko ya kuleta hii sheria na kuifuta kampuni ya *TTCL* na kuanzisha Shirika kwa sababu hii imelenga changamoto zilizokuwepo kwa ufanyaji kazi wa kampuni na imelenga changamoto zilizokuwepo katika ubinafsishaji kwa ujumla. Kwa hiyo, niipongeze sana Serikali kwa namna ya pekee ambavyo imeona sasa ni wakati muafaka kurudisha hili shirika na kutokana na umuhimu wake wa kuwa na shirika letu la mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna baadhi ya nchi bado zina mashirika ya mawasiliano kwa mfano China, mpaka sasa hawaruhusu *code share* yaani muungano na kampuni nyingine za simu nje ya nchi ya China. Yote hii imelenga

kuimarisha usalama wa nchi yao, kukuza uchumi kama ambavyo kazi zimeainishwa za kampuni za hili shirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, China kwa sasa hivi hata *social media* wanaangalia jinsi gani ya kuzidhibiti na hata mitandao kwa mfano kama *whatsapp*. Sasa yote hii inalenga kwenye mambo mazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na michango hiyo, naomba niendeleo na maeneo mengine, kuhusiana na *composition* ya Bodi, napendekeza angalau aongezeke mtu mmoja na kwa upande wa Zanzibar wawe wanatoka watu wawili. Vilevile katika uteuzi sifa za hawa *Board Members* ziweze kuangaliwa kiufasaha zaidi na angalau hata kwenye kanuni ambazo zitatumwa na Waziri mhusika basi sifa za *members* ziboreshwe angalau sasa kwa sababu shirika letu liko nchi nzima na tumeshakuwa na changamoto kule nyuma katika utendaji wake, mpaka ikasababisha hatua zilizochukuliwa na Mheshimiwa Rais katika kulifufua, basi tuwe na Bodi ambayo itakuwa ni nzuri na inafanya kazi vizuri, *recruitment* ya hawa *Board Members* kama kutakuwa na uwezekano tuweke taasisi ya tofauti (*independent organ*) iweze kufanya *interview* na ku-*recruit* bodi ambayo itakuwa ni nzuri kuliko kuwa chini ya Waziri. Kama itawapendeza Serikali, nitaomba ikae namna hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 22(1)(a) katika masurufu ya vyanzo vya mapato vya hili Shirika la Mawasiliano, kifungu cha (1) kinazungumzia kwamba Bunge linaweza likatenga fedha kwa ajili ya kazi za shirika hili. Kwa sababu tunajua mawasiliano ni moja ya sehemu ambazo kwenye mwaka wa fedha uliopita kwa mfano 2016/2017 zilichangia karibuni asilimia 17 kwenye kukuza uchumi na hata pato la Taifa hizi kampuni za simu tunaona ni maeneo ambayo mapato yapo kama tutakuwa na mkakati mzuri na uongozi na bodi zitafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama itapendeza tu-*delete* Kifungu cha 22(1)(a) shirika likajitegee asilimia 100 bila kupata ruzuku yoyote kutoka Serikalini ili waweze kufanya

kazi kwa ufanisi na kwa sababu vifungu vinavyofuata vinaruhusu kukopa basi wakawe kibiashara zaidi waweze kukopa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mojawapo ya sheria zilizopitishwa na Bunge lako Tukufu ni makampuni ya simu kujisajili kwenye soko la hisa. Kwa hiyo, tungeomba kutokana na mchakato ambao unaendelea na *performance* ya *TTCL*, najua sasa itahamishwa kwenda kwenye shirika, basi na mchakato wa kwenda kwenye soko la hisa uweze kufanywa na tuingie huko ili kuendelea kuweka uwazi. Kwa sababu sasa mahesabu, utendaji vitakuwa wazi kwenye *public* kwa hiyo hii itasaidia sana kulenga kwenye ufanisi wa Shirika letu hili la Mawasiliano. Kwa hiyo, nitaomba Serikali walichukue hilo na muweze kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 28 kwenye suala la kuhamisha mali na madeni kutoka kwenye kampuni inayofutwa na sasa tunakwenda kwenye shirika tungepata kwa sasa hivi hii *TTCL* ambayo sasa inaenda kufutwa kama kampuni hali yake ya ufanyaji biashara ikoje, wana-*operate* kwenye *loss*, wana *operate* kwenye faida na *status* za madeni zikoje maana ukienda kuangalia kwenye *balance sheet* utaweza kujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana katika kuhamisha mali hizi, uthamani na kuthamini madeni pamoja na mali zinazohamishwa ufanyike kiufasaha na najua tulipitisha Sheria ya mambo ya *Valuers* na *Valuation* mwaka jana, basi tuzingatie sana tupate *valuers* wazuri ili tunavyohamisha hizi mali na madeni, kwa mfano kama madeni haya *third party confirmation* ifanyike. Lazima tuthibitische kwa wale wanaotudai kwamba kweli kiwango hiki ndicho tunachodaiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu tumeshakuwa na changamoto nyingi kwenye kampuni ambayo ilikuwa ina *nature* ya shirika ya kuwa kwamba huenda kuna madeni hewa au wadaiwa hewa, kwa hiyo, ni suala la kuthibitisha. Kwa hiyo, tuhamishe vitu ambavyo

vimebeba *value* ile halisi kwa ajili ya kwenda kwenye shirika letu ili lisije likabeba mizigo ambayo siyo ya kwake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kuona pia katika kifungu mmezingatia kwamba mtabeba masuala ya waajiriwa wote, kwenye kifungu hiki cha 31, *terms* zao zilivyo sasa hivi, masurufu yote ya watumishi yanabebwa yanaenda kwenye shirika na hapo ndiyo huwa msingi mzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ningependekeza kama wanaweza kuongeza kipengele, sasa hivi najua watumishi wengi ni wa mkataba wa muda mrefu, wale *permanent employees* basi tuone kama wanaweza wakaruhusu na kama kuna mikataba ya hiari kwa hii kampuni sasa hivi kwa wale ambao wangependa kustaafu wakaanze maisha yao waruhusiwe lakini ni lazima waangalie pia na *potential* ya mtu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtu mwingine anaweza akawa anaomba kustaafu lakini ni *potential* kwa mfano Idara ya Ufundi, Idara ya Mitambo ndiyo sehemu ya *operation* ndiyo *production area*, huko lazima tuangalie, lakini maeneo mengine katika kupunguza mizigo kwenda kwenye shirika, sasa hivi kampuni iangalie watu wenye hiari ya kustaafu iwaruhusu wastaafu, walipwe masurufu yao, basi tunavyoingia kwenye upande wa shirika na kama tunaleta ajira mpya tulete ajira pia za kudumu na hata zile za mkataba ili tuwe na soko huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwa upande wa watumishi tuna changamoto kidogo, makampuni mengine ya simu kwa mfano *Vodacom*, *Tigo*, ulipaji wa wale *key personnel's* na hasa upande wa *operation* masurufu yao wanalipwa vizuri zaidi kuliko watu walioko ndani ya *TTCL*. Kwa hiyo, unaweza kukuta kwenye hili shirika tunalolanzisha tutakuwa tunaajiri watu baada ya mwaka mmoja, miezi sita wanaacha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuangalie tuje kuwa na mishahara ambayo inaendana vizuri na soko ili

wataalam wetu ambao tutakuwa nao wakiingia na ndiyo wataalam wetu wasiondoke haraka. Kwa hiyo, ile *labour turnover* iwe ndogo kuliko kwa sasa hivi sidhani kama wana-*maintain* sana kutokana na malipo yao hayalingani na kampuni zingine za ushindani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu hii *TTCL Pesa Limited*, kwa sababu tuna-*adapt* kila kitu na katika vyanzo vya mapato vikubwa vya makampuni ni mambo ya miamala ya kipesa. Kwa hiyo, tuzingatie sana, hii *TTCL Pesa Limited* iendelee lakini usimamizi wake uwe wa hali ya juu kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kwa faida na hakuna *frauds*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine nimeona kwamba Bodi itaandaa *Annual Report* baada ya kufunga mahesabu miezi sita, lakini litakuwa ni shirika ambalo litakaguliwa. Sasa hii miezi sita sidhani kama inatoshia, kuna miezi mitatu kama tunavyo-*adapt* katika Taasisi za Serikali ya kuandaa mahesabu, miezi mitatu Mkaguzi afanye kazi, kwa hiyo miezi sita hii haitoshi kwamba ripoti tayari amepewa Waziri. Kwa hiyo, angalau ingesema kwamba baada ya miezi sita Bodi inaweza ikawasilisha ripoti za ukaguzi kwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kwamba, tayari sisi nchi yetu tuna Mkonga wa Taifa na nina matumaini kwamba utakuwa chini ya shirika hili. Kwa hiyo, tuone matumizi mazuri na katika kuongeza vipato Halmashauri zote ziwe *connected* na huo Mkonga wa Taifa na unaendelea kusambazwa nchi nzima. Basi ufanisi wa kuuza *data* wa shirika hili la mawasiliano tuharakishe pia na Mkonga wa Taifa kuweza kutumika. Sasa hivi mawasiliano nasikia tunaenda kwenye 5G, tulikuwa 3G, tumeenda 4G, 5G inakuja, sasa tuangalie jinsi gani pia ambavyo tunaweza kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, tubadilisha tabia (*attitude*), ule ufanyaji kazi wa kimazoea kama ilivyokuwa shirika, imekuwa kampuni, tukibadilisha *attitude* ya watumishi na utendaji wa shirika kiujumla iwe na kimtazamo sasa wako kwenye ushindani, ufanisi wao na ufanyaji kazi wao utakuwa

ni mzuri sana na mantiki ya kuvunja kampuni na kwenda kwenye shirika sasa tunatarajia italeja tija katika nchi yetu na tunatarajia *Treasury Registrar* ataweza kupata mgao wake wa faida kwa Shirika letu hili la Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nashukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono mabadiliko ya sheria hii. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba atafuatiwa na Hussein Mohamed Bashe.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kipekee na mimi niweze kuchangia Muswada huu wa Shirika la Simu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kwa makini sana maelezo ya Mheshimiwa Waziri, Profesa Makame Mbarawa aliyoyotoa akiomba tupitische Muswada wake wa kumpatia shirika hili na katika maelezo yake anasema moja kati ya madhumuni yake eti anataka kulipatia Shirika la Mawasiliano ya Simu jukumu la kusimamia miundombinu ya kimkakati ya mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika hili lilianza shirika, ikaja kampuni sasa tunarudi kwenye shirika, lina miaka zaidi ya 40. Bahati nzuri ndugu yangu Profesa Makame Mbarawa amekuwa kwenye *system* hii ya mawasiliano kwa muda mrefu, alikuwa huko na mpaka sasa amekuwa Waziri. Juzi alikuja hapa wakatulisha ubwabwa, wakasema kwamba wanazindua *TTCL*, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwepo kama mgeni rasmi, mpaka leo sijaona ushindani kati ya *TTCL* na makampuni mengine ya simu yaliyoko Tanzania. Sijauona ushindani wa aina yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunaongea habari ya *3G, 4G, 2G* peke yake *line* ya *TTCL* ukiweka kwenye simu hizi ndogo ndogo za tochi haifanyi kazi. *Line* ya *TTCL* ukitoka *three kilometers radius* kutoka maeneo ya mjini au kwenye *highway* haishiki. Leo tunataka kumpatia Profesa na Wizara yake

jukumu la kwenda kusimamia *TTCL* ambayo kimsingi ameshindwa kui-*manage* asimamie hiyo pamoja na makampuni mengine ambayo kimsingi kwake ni *giants* kwenye masuala ya mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda namna hii inabidi tuwe makini sana kwa sababu wakati mwingine inawezekana tunafanya hivi ili kujifurahisha lakini kweli leo tunarudi kwenye shirika kuipa ruzuku, kui-*breast feed TTCL* yenye miaka zaidi ya 40. Ina miaka zaidi ya 40 inataka *breast feeding* ili iweze kukua iende ikashindane na makampuni mengine maana tunasema sijui *database* na kadhalika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inabidi Waheshimiwa Wabunge tulifikirie mara mbili suala la *TTCL* na suala la kwenda kwenye shirika la simu. Mimi ninachokiona hapa tunarudi kwenye ujamaa. Tunarudi kwenye Sera ya Ujamaa ya kutaka kwa vile *TTCL* yetu imeshindwa kushindana na makampuni mengine ya simu sasa tunataka kuyadhibiti ili angalau twende pamoja wakati tunazidi kuchelewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge tujaribu kusajili *line* ya *TTCL* leo. Ukisajili *line* ya *Tigo*, *Vodacom* dakika tano unakuwa uko hewani, *TTCL* ukienda kusajili kwa wakala itakuchukua saa moja mpaka masaa mawili ili uweze kuwa hewani. Sasa mimi najjuliza Mheshimiwa Makame Mbarawa amekaa siku zote hizi, hebu kwanza atupe *update* tangu tumekula ubwabwa wa uzinduzi wa hili suala amefikia wapi? Au ndiyo leo anakuja na *gear* hii kesho unabadilisha unaingia na *gear* hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu Mheshimiwa Waziri atueleze amefikia wapi miaka miwili na nusu akiwa kama Waziri katika Sekta hii ya Mawasiliano kuhuisha kampuni ya Kitanzania ya mawasiliano kushindana na makampuni mengine na ndiyo maana unaona hata Wabunge wakisimama humu ndani leo hawaombi upeleke mnara wa *TTCL* wanasema leta *Halotel*, wanasema leta *Voda*, hamna mtu anataka habari ya *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tumeshindwa kushindana kiuchumi kwa kufuata *fair competition* tusitumie mwanya kwa sababu sisi ni Serikali eti tuseme tunaenda kukandamiza *private sector*. Tusitumie mwanya huo kwa sababu mwisho wa siku tutakosa hata hao wawekezaji. Tunawakaribisha kwa mbwembwe na vigelegele na nini karibuni mazingira yako *conducive*, mwisho wa siku mbele ya safari tunaanza kubadilisha magoli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye Muswada huu wameweka mazingira ya kuwa-*favour* wao. Wanasema ili mtu aweze kuwa Mwenyekiti wa Bodi anatakiwa angalau awe na uzoefu wa miaka nane. Kama hiyo haitoshi kufanya kazi miaka mitano, hivi kweli, hawawezi kuiga mfano kwa wenzenu?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo makampuni ya simu yaliyowekeza hapa Tanzania wanatumia wasanii tu kijitangaza na mambo yanakwenda, utasikia mara leo haliishi *bundle*, mara leo halichachi, mara nini, kampuni inasonga mbele, lakini sisi tulichokalia ni kutengeneza yale mazingira ya *bureaucracy* na urasimu mle ndani ili kusudi tu ionekane kwamba hii ni kampuni ya Serikali, kiukweli sioni sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Makame Mbarawa ampime mtu utendaji kazi wake kwa jinsi ambavyo alivyo *creative*, ampime kwa *competency* yake, ampime kwa jinsi gani anamletea matunda na siyo kukimbia mara anataka shirika, mara leo *corporation*, mwisho atasema iwe *NGO*. Tafadhali sana, tunamwomba awapime kwa *competence*. Leo mtu anayeweza kukaa kwenye Bodi akamletea mabadiliko akimchukua kwenye makampuni mengine ya simu hampati mtu wa miaka 56 au 57 anayemtaka yeye, hampati!

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo vijana wadogo wanafanya kazi, afungue boksi Mheshimiwa Waziri apate watu ambao watamsaidia kusukuma kazi siyo kila siku

anacheza na makaratasi, anabadilisha sheria hii, anaweka urasimu huu, haitamsaidia wala haitaisaidia Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Simu (MTN) South Africa, leo mimi nikisikia habari ya MTN cha kwanza ninachokifikiria ni South Africa, wamei-brand ile kampuni ya simu ya nchi yao ili popote itakapokuwa inapita ionekane kwamba ni nchi yao. Tunao vijana wazuri wanaocheza mpira, wanaigiza sanaa wako kimataifa, yuko Mbwana Samatta, amtumie, anatumika kwenye matangazo mengine huko, atamsaidia hata bure kwenye Instagram yake ata-post TTCL. Kwa nini tusitumie marketing strategy na tuwe business oriented ku-push hii TTCL.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naiona a hidden agenda ya kurudisha hii mambo ya shirika, sijui corporate, sioni nia njema ya dhati ya Serikali kutaka kusukuma maendeleo. Tumesh invest vya kutosha, tumeweka pesa nyingi kwenye mashirika ya umma lakini sijaona mafanikio makubwa kama nguvu inayoingia, sijayaona.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka nimuulize Mheshimiwa Makame Mbarawa hili suala la upigaji kura, aje atueleze hapa, tukija kupiga kura kwa sababu hili suala kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 98(b) ukisoma pamoja na Orodha ya Pili ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Nyongeza ya Kwanza inasema jambo la simu ni jambo la Muungano. Sasa Mheshimiwa Waziri aje atueleze hapa wakati tunapiga kura tutatafuta ile theluthi mbili ya Zanzibar na theluthi mbili ya Tanzania Bara au upigaji kura utakwendaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani kufahamu kwa sababu ninavyofahamu Wazanzibari hawajanufaika kwa namna yoyote na uwepo wa kampuni hii ya simu. Leo tukisema tunarudi kwenye suala la shirika tunarudi kulekule ambako wanasema jiwe wallilolikataa waashi, ndiyo tunarudi kulekule, sasa tuone kama kweli tukipiga kura watarudi kuchagua hili suala la shirika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko kwenye dunia ya ubepari siyo dunia ya ujamaa kwamba leo tukiona tumezidiwa mchezo tunabadilisha magoli, hatuko huko. Tunahitaji kuona Kampuni ya Tanzania, mimi leo utaniita siyo mzalendo natumia makampuni mengine ya simu kwa sababu hivi kweli nitasikia raha gani niko mbali na familia yangu nikishika simu yangu kutwa inaniambia hakuna *network*? Nitasikia faraja ya namna gani? Natamani nikishika simu nasafiri kwenda kwangu Kahama kule Shinyanga mtandao uwepo, lakini leo *TTCL* mikoani haipatikani na zaidi ya yote ni simu ya watu ambao ni matajiri, wanaoweza kumiliki *smart phone* kwa sababu inashika *3G* na *4G* peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, *of course* inaleta *assurance* kwamba ukiwalazimisha Ofisi zote za Serikali na Idara zake watumie *TTCL* utapata wateja zaidi ya milioni saba au milioni nane, lakini hivi kweli wanaturudisha kule ukienda kukata leseni unaambiwa mtandao umebuma, wanataka waturudishe kule ukienda bandarini kulipia unaambiwa mtandao uko *down*. Huwezi kuwalazimisha watu watumie huduma mbovu unayoitoa eti kwa sababu wewe ni Serikali na wala hatuwezi kukubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme leo Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atueleze tangu amepewa dhamana ya kuwa Waziri wa Mawasiliano amefanya nini kuhuisha *TTCL* ili iweze kutumika na kushindana na makampuni mengine ya simu Tanzania. Siyo tu hivyo, aje atueleze hapa nini mkakati wake atakapopewa huu uwakala wa kusimamia makampuni mengine ya simu ilhali tulishaingia kwenye mikataba tukakubaliana na wawekezaji waliokuja kuwekeza kwenye *industry* ya mawasiliano kwamba mchezo utakuwa *fair*. Nini *strategy* ya Serikali juu ya hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli tunasema Tanzania ni kisiwa cha amani, ni eneo ambalo unaweza kuwekeza, lakini kwa mazingira ninayoyaona, tunawatisha wawekezaji kwamba Tanzania utawekeza leo, miaka mitatu au minne mbele hali lazima itabadilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekaa nafikiria kuhusu suala la *Data Centre* kwamba iwe *managed* na *TTCL*. Mheshimiwa ananicheka, labda kama tunaliongea hili kisiasa lakini tukiliongea kibiashara kwamba tunatafuta biashara Tanzania *TTCL* ifanikiwe tupate hela halafu leo unasema lazima iwe *managed* na *one centre source*, mimi hainingii kichwani. Tushindane kwa hoja, tushindane kibiashara, tusitumie rungu la Serikali kwamba kwa sababu sisi ni Serikali tuna uwezo basi kila siku sisi tunaibuka na matamko, kila siku sisi tunaibuka na malekezo, mara tumebadilisha sheria, hapana. Tanzania ni nchi *conducive for investment*, hatuwezi kufikia hatua ya Mataifa mengine ambayo watu wanakimbia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wangu hii hoja aliyoleta Mheshimiwa Makame Mbarawa sijaelewa yaani naona anazidi kuturudisha ambako hata sisi hatukuwepo maana hiyo miaka hata sikuwepo, ndiyo anatupeleka huko. Tulisoma kwenye vitabu vya historia darasani ndiyo anaturudisha huko halafu tena anatuchanganya. Twende kibiashara, aendeshe *TTCL* kama kampuni ya kibiashara, watu wale wawe *answerable*. Huwezi kuniambia ili ufanye kazi kwenye kampuni ya simu, Joti amesomea mambo ya simu?

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi ukaniambia ili ufanye kazi kwenye kampuni ya simu lazima uwe na uzoefu wa miaka nane, mimi hicho kitu sikubaliani nacho, Joti amesomea mambo ya simu? Wako vijana machachari tufanye *marketing, advertisements, investment*, tutumie *resources* tulizonazo tupambane na mashirika mengine duniani. Hata ukiweka Mlima Kilimanjaro kwenye *TTCL* watu watanunua *line* ya *TTCL* lakini usiniambie leo unaenda kushindana na watu kwa kuwaambia eti unataka kutengeneza mkakati, wewe mkakati wa kwako mwenyewe umeshindwa kutengeneza, utaweza kutengeneza mkakati wa mashirika mengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata darasani anayechaguliwa kuwa *monitor* ni yule anayefaulu, huwezi kuwa *monitor* darasani wakati unafeli. Sisi tumeshafeli kwenye

TTCL, sasa tumeona hapa tutafute ukiranja ili mwisho wa siku mtu akiongea unamwambia kaa chini, wakiibuka hawa kaa chini, kama ambavyo inafanyika kwenye mashirika mengine mengine sitaki kuyataja nitachangia siku ikifika. Tushindane kwa hoja, tushindane kibiashara, mambo ya kuleta usanii wa...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ajiandae.

MHE. HUSSEIN M. BASHE: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Labda nianze kwa kusema kwamba Serikali imetuletea Muswada huu wa kuihamisha *TTCL from a Limited Company* kwenda kuwa *Corporation*. Kwenye biashara maana yake tumeitoa kwenye uwanja wa mapambano tunaenda kuifungia chumbani ili tui-*spoon feed*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini najjuliza tu swali, *why corporation and not limited liability company?* Naelewa, *strategically* ni Serikali haitaki kuipeleka kwenye *DSE*, kwenye soko la hisa, ndio mkakati. Ili tuiweke miongoni mwa mashirika ambayo kwa muda mrefu yameendelea kuwa *liability* kwa Serikali lakini tatizo la msingi la *TTCL* ni sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni swali ambalo lazima tuweze kujijibu sisi. Tatizo la msingi la *TTCL* sio sheria, tatizo la msingi la *TTCL* ni *business model* ya *TTCL*. Kwenye sheria kuna *subsidiary company* inaitwa *TTCL Pesa*, *money transfer* kwenye *mobile business* ni *one of the product*. Kama kweli tunataka

kuifanya *TTCL* kuwa *strong and effective* kwa nini tunaiacha hii *subsidiary* peke yake? Nani atai-*finance*? Itabebwa na nani? Sheria haijasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri kama tumeamua kula nguruwe tule aliyenona. Tumhamishe na huyu *TTCL Pesa* kama tunavyochukua mali zote, *assets and liabilities* kuziingiza chini ya *corporation* tuiweke kwa sababu ni moja ya *line* ambayo italipatia pesa shirika hili. Hilo ni jambo la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, sheria hii inampa mamlaka Waziri kuisimamia Bodi na kutoa maelekezo. Siyo nia mbaya lakini nataka niulize Serikali tuna mtu anaitwa *Treasury Registrar*, huyu ndiye msimamizi mkuu wa mashirika yote ya Serikali. Humu kwenye sheria Bodi haiambiwi kwamba itawajibika kwake, itapewa maelekezo na Waziri na siyo Hazina, kwa nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tuna nia kweli ya ku-*transform* na *model* zipo. Ukiangalia *Far East Malaysia*, *Singapore*, *the powers* za *Treasury Registrar* zilizopo kwenye mashirika ya umma ndiyo maana yame-*perform*, hata hiyo China mnayojadili. *These are the people* wanaisimamia, *Treasury Registrar* ana *right* ya ku-*hire* na ku-*fire*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwapeni swali Waheshimiwa Wabunge, tujiulize anayesimamia mashirika ya umma ni Msajili wa Hazina, lakini Msajili huyu wa Hazina hana mamlaka ya kumfukuza kazi Mkurugenzi wa Shirika, hana mamlaka ya ku-*appoint Board of Directors*, tumezipeleka hizi *powers* kwa *political figures* halafu tunategemea *results*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri, hapa sina *platform* ya kuleta *ammendments*, nashauri kwa Mheshimiwa Waziri, *I agree* dhamira ya Serikali kwamba tunataka ku-*maintain security*, *communication is very important* lakini lazima wajue tunatengeneza *monopoly rights* kwa *TTCL*. Inawezekana kuna

sababu zipo za kiulinzi na kadhalika, *we can agree, but* wajenge mazingira ya kulifanya shirika hili liweze kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mazingira haya ili tufanikiwe, ili tuweze kufika tunakotaka, Msajili wa Hazina angepewa hizi *mandate* anazopewa Waziri. Msajili wa Hazina angepewa *mandate* ya ku-*appoint Board of Directors*, hata Mwenyekiti, angepewa haki ya kuweza ku-*hire* na ku-*fire* Mkurugenzi ili aweze kusimamia vizuri haya mashirika, aweze kuwa na *powers* huyu Msajili. Bila ya hivi tutaendelea kuongeza mzigo, tuna mashirika zaidi ya 50 au 60 ni mangapi yanafanya kazi kwa faida? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatengeneza hili, najua tuna sheria keshokutwa tutaleta ya *NASAC* ambayo na yenyewe tunaipa mamlaka ya kufanya biashara *indirect* na yenyewe itataka kupata fedha kutoka Bunge, itataka kupata msaada wa Bunge na yenyewe kuwa shirika. *Are we creating environment* ya biashara? Kwa nini Waziri anachukua *mandate* hizi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa kaka yangu Mheshimiwa Profesa Mbarawa ni kwamba, wakati ana-*wind up* hapa, akubali tu hizi *powers* alizochukua za kusimamia Bodi hii wamwachie *Treasury Registrar*. Tuangalie uwezekano wa *AG* kuleta ka-*ammendment* hapa ili *Treasury Registrar* tumpe jukumu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni *recruitment process*, ukiangalia zote ni *appointment*. Hivi jamani kwa nini tusiseme kwamba *Directors* wote wa Bodi wata-*apply* na wata-*compete* kama ambavyo *private sector* inafanya lakini wote tunawa-*appoint* na hili shirika tunatarajia liende likafanye biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba sioni kama tatizo la *TTCL* ni sheria, sioni tatizo la *TTCL to be called corporation or limited company*, aah, aah, hili sio tatizo. Tatizo la msingi la *TTCL* tunatoka kwenye tatizo

tunaenda kwenye tatizo lingine kwamba tunampa Waziri mamlaka lakini Waziri siyo msimamiaji wa mashirika haya ya umma. Mwenye mamlaka ya kusimamia mashirika haya ya umma hana *powers* kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine dogo tu ambalo nataka niliseme, kulifanya kuwa *corporation* tusilifungie mlango wa kulipeleka kwenye soko la hisa. Tuna *window* ya makampuni yanayopata hasara, tulipeleke kule, tuliache liende kule ili Watanzania waweze kushiriki. Kuwe kuna *transparency* ili tuweze kuona *books of accounts* za haya mashirika ya umma kwa sababu yakienda kwenye soko la hisa tutayaona lakini tusipofanya namna hiyo hili ni tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* haiwezi kufanya kila kitu, ni lazima ikubali ku-*define*, tunali-*empower* hili shirika ili likajibu tatizo gani? Likajibu tatizo la kuwa na simu za mkononi, likajibu tatizo la *data* kwa sababu *the future of this business* ni *data*. Lazima tujue tunataka kwenda wapi na ili tuweze kufanikiwa ni lazima tuondoe mfumo wa mashirika ya umma Wakurugenzi, *Board of Directors* kuwa *appointed* na Mawaziri, iwe ni *competitive mechanism*. Yanatangazwa, wana-*apply*, wanaingia kwenye *interview* ili waweze kupata nafasi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, kupokea taarifa kwa miezi sita Mheshimiwa Waziri *according to this law is too long*. Apate taarifa za shirika hili *quarterly*, tuisubiri miezi sita. Akipata taarifa hizi *quarterly* atakuwa na nafasi ya kuweza ku-*take corrective measures* kwenye shirika hilo kwa muda mfupi kabla ya hasara au matatizo ku-*grow*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme kwamba tulipo ni *point of no return* na mwelekeo ni kwenda kuanzisha *corporation*, Waziri akubali kifungu hiki kinachompa mamlaka makubwa ayapunguze, amuachie *TR* ili awe na haki ya kuisimamia hii bodi *direct*. *TR* apate *powers* za ku-*appoint directors* ili aweze kuwa *answerable* siku ya mwisho kwa Waziri wa Fedha kwa sababu shirika hili likilegalega

watarudi kwa Waziri wa Fedha kuomba hela kutoka Hazina na watakuja hapa tutawapitishia lakini jicho la Wizara ya Fedha kwenye mashirika ya umma ni *TR* ambaye hana *powers* katika haya maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie tu kwa kusema kwamba inawezekana dhamira ni njema sana lakini *strategy is very wrong* kwa mwelekeo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah atafuatiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ajiandae.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia Muswada uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue fursa hii kuwapongeza sana Mawaziri wangu wa Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri waliyoifanya jana. Mawaziri hawa jana wameonesha kabisa kwamba wao wanaendana na kasi ya Mheshimiwa John Pombe Magufuli. Wamejibu vizuri sana, tunawapongeza tunawaomba waendelee kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kuleta Muswada huu wa *TTCL* kuwa shirika la umma kwa asilimia 100. Kwa nini nasema hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* ndiyo mawasiliano yote ya nchi yako pale. Unapoichukua *TTCL* unaiunganisha na *CelTel* ni kwamba unaweza ukauza siri za nchi yetu bila wewe mwenyewe kujijua. Kwa hiyo, niipongeze sana Serikali, wamefanya jambo zuri ambalo kwa kweli tutaendelea kuwapongeza siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tatizo lolote lingetokea tungeshindwa kujilaumu kwa sababu mawasiliano yetu yanaweza yakaingiliwa wakati wowote na wabia ambao wamekuja kuwekeza kwetu. Kwa hiyo, nawapongeza sana wamefanya jambo jema na nawaomba Wabunge wote tuupitithe Muswada huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile huko vijijini ukiwasha *Vodacom* unapanda kwenye mti, hawaendi sehemu ambazo hazina wateja wengi. Kwa hiyo, Serikali yangu naomba sasa *TTCL* muipe nguvu na mtaji mzuri ili waweze ku-*compete* kwenye biashara na mashirika ya mawasiliano yaliyopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimefurahi. Sisi tunatoka huko vijijini utakuta mtu akiwasha *Vodacom* mpaka aende juu ya mti au porini lakini naamini kwa kuwapa asilimia 100 *TTCL* tutaweza kupata mawasiliano nchi nzima kwa kupitia shirika letu la umma la *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niunge Serikali yangu mkono kwa kuwapa *TTCL* Mkongo wa Taifa pamoja na *Data Centre* ili waweze ku-*compete* vizuri na mashirika mengine kama *Vodacom*, *Airtel* na *Zantel*. Hata hivyo, hili lisiwe sababu ya kuwanyima masafa wenzetu wa *Vodacom*, *Airtel* na wengine wowote wanaofanya biashara hizi. Wakiomba masafa na wenyewe wapewe ili waweze ku-*compete* kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napata tabu kwenye kitu kimoja, naona watu wana mawazo sana kwamba labda haitaweza kujiendesha, sijui tumerudi kwenye ujamaa, hivi vitu vimetoka wapi? Mbona China wamedhibiti mawasiliano yao yote na wanajiendesha na wana maendeleo makubwa? Pia Korea na nchi nyingine tofauti tofauti wamefanya hivyo, kwa nini sisi leo tunakuja hapa badala ya kuipongeza Serikali kwa kudhibiti mawasiliano, tunasema tena tuache mawasiliano yaendeleo kuendeshwa na wawekezaji? Kwa kweli jambo hili siwezi kulikubali kabisa na tunaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuache kutishana kwamba kila kitakachofanyika ni ujamaa, hata kudhibiti mawasiliano yetu ni ujamaa, hii itakuwa shida na tutashindwa kufanya kazi. Halafu pia ujamaa siyo dhambi hivyo kama tunavyoiongelea au tunavyoifikiria, ni mambo ya kawaida tu ya kupanga ni kuchagua, kama Serikali yetu imepanga kufanya nini, basi mambo yanakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe pia Serikali yangu kuweka mtaji mzuri kwenye shirika hili la umma la *TTCL* lakini pia kupata *management* yenye uwezo mkubwa. Niiombe Serikali katika hili ndiyo tuangalie sana kuweka *Managing Director* ambaye ana uwezo na watu wake wa kumsaidia ili shirika letu liweze kwenda vizuri. Kwa mfano, Shirika la *National Housing* limekaa vizuri linajiendesha kibiashara, tunaamini *TTCL* litakuwa shirika la kibiashara ili liweze ku-*compete* na wenzie na siyo lijibweteke lingojee kila siku kupata ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona *ATCL* juzi Mheshimiwa Rais amefufua shirika hili na tunaona jinsi linavyoenda vizuri. Ukisoma taarifa yao ya karibuni utaona kwa muda mfupi wamepata faida ya karibia shilingi bilioni tisa. Kwa hiyo, naamini pia *TTCL* ikisimamiwa kwa Serikali ya Awamu ya Tano inavyofanya kazi hatutajuta na tutakuwa tumejiwekea kitu kizuri, siri zetu zitakuwa bado zimo ndani kwetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na naipongeza sana Serikali. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Mwanasheria Mkuu wa Serikali atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Mheshimiwa Waziri mtoa hoja ajiandae.

MWANASHERIA MKUU A SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru ka kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha na mimi nipate fursa ya kushiriki nanyi nikishauri mambo kadhaa ambayo yamejitokeza humu ndani na hasa masuala ya katiba na sheria. Nianze kwa kusema tu kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Serikali imechelewa sana kuleta Muswada huu. Sababu za kuwa na shirika linalosimamia mawasiliano yake nchini ni muhimu sana. Ngoja Waheshimiwa Wabunge niwaambie, yule mtu anayemiliki miundombinu ya mawasiliano anakutawala. Anayemiliki miundombinu ya uzalishaji wa umeme anakutawala. Kwa hiyo haishangazi mifano inayotolewa kuhusu China unaona wanamiliki miundombinu ya mawasiliano na mnaona ni *the giant, one of the super powers*, hata wakubwa wanalazimika kusafiri kutoka huko kwenda China. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Tambwe; labda niseme tu hivi unajua sisi tunaosoma ujamaa kila wakati, ujamaa ndio unaotawala sasa hivi. Kwa sababu hata katika hii *corporate world* kuna *corporate social responsibility* kwamba wewe ulienacho hakikisha kwamba unashirikiana na wengine. Kuna suala la kulipa kodi, kuna suala la *floating shares* kwenye *stock exchanges* watu wananunua *shares*. Kwa hiyo, unakuta mwananchi au mtu yeyote na miliki ile. Kwa hiyo tusiseme ujamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilifikiri niliseme hili wazi kabla hatujaenda kusema. Kwa hiyo mimi nasema naunga mkono hoja muswada huu kama walivyoshauri Waheshimiwa Wabunge na kama ulivyoletwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ambalo ningeanza kulisemea ni suala kutunga sheria zinazotumika pande mbili za Muungano. Utaratibu umewekwa kwenye Katiba, Ibara ya 98(1) (b) imeeleza vizuri sana, sidhani kama

nahitaji kuisoma kwa sababu nina muda mfupi sana. Lakini hayo mambo yanayohitaji theluthi mbili ya Wabunge kutoka Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Zanzibar ni yale mambo ambayo yameongezwa katika nyongeza ya pili, jedwali la pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yenyewe ukiyasoma; na ni lazima niyaseme sasa hapa; *essentially* ni mambo ya Katiba. Yaani katiba haijiandiki yenyewe inaletwa na Muswada. Kwa mfano kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni suala la katiba hilo, ukishakwenda kwenye Katiba lazima uwe na theluthi mbili kutoka Bara na theluthi mbili kutoka Zanzibar. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kuwepo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano na madaraka ya Serikali ya Zanzibar ni masuala ya katiba yapo kwenye Katiba hii. Mahakama Kuu ya Zanzibar, orodha ya mambo ya Muungano na idadi ya Wabunge kutoka Zanzibar ni suala la Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukitaka kubadilisha haya unaleta Muswada wa Mabadiliko ya Katiba, ni lazima sasa hizi nchi mbili zinarudi katika *position* zake, wakubaliane. Kwa hiyo, Waheshimiwa na hii si sheria ya kwanza ambayo tumetunga kwa njia hii, tumetunga sheria nyingi tu hapa ambazo zinaenda kutumika Zanzibar kwa sababu hapa hatubadilishi katiba. Kwa hiyo ni suala tu la uelewa wa katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nilifafanue hili lakini nadhani Waheshimiwa watanielewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni hili ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Bashe. Unajua ibara ya 36 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, imeweka utaratibu wa namna ya kupata watendaji wakuu wa vyombo hivi. Kabla sijasema pale niseme hivi, Msajili wa Hazina (*Treasury Registrar*) ana sheria yake mahususi na chini ya sheria ile ndiye

anayesimamia utendaji wa haya mashirika kwenye level ya utendaji. Kwamba wanafanya kwa kadri inavyotakiwa...

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Lakini Waziri yeye msingi wake anahangaika na masuala ya kiseru na msingi wake anahangaika na masuala ya kiseru na msingi wake...

T A A R I F A

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuna taarifa, Mheshimiwa Salome Makamba!

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninapenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, *unless* kama sijaelewa. Ie orodha ya pili anayoisoma ambayo ipo nyuma ya katika; moja mpaka saba inasema orodha ya mambo ya Muungano. Ukinipeleka kwenye orodha ya mambo ya Muungano kwenye Katiba ya Kiswahili ukurasa wa 128, namba 11 inasema katika mambo ya Muungano kuna bandari, mambo yanayohusika na usafiri wa anga, posta na simu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mwanasheria Mkuu wa Serikali afahamu kwamba kwenye orodha ya mambo ya Muungano na ndiyo maana nimehoji kwamba kama tutaenda tutaangalia ibara ya 98 basi kwenye orodha ya mambo ya Muungano posta na simu ambao ndio mjadala uliopo mezani iko *included*. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unapokea taarifa hiyo?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei, unajua sio wote wataalam wa *Constitutional Law*, hili nimelishalitafsiri. Nasema haya masuala yamewekwa mahususi tena mbele pale

wamesema kwamba haya ndiyo yanayohusika na ibara ya 98(1)(b) ya kupigia kura. Waliokuwa ndani ya Bunge hili mwaka 2015 ilikuja hoja kama hii, Waziri Mkuya alikuwa na Miswada mitatu, Saada Mkuya akiwa Waziri yuko hapa; wakasema ni lazima twende Zanzibar tukatoa ufafanuzi hapa tukaelewana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kama tusingekuwa tumeliamua hapa, 2015 mbona hiki kifungu kinajieleza? Unasemaje haya yaliyopo pale, sheria za Utumishi, *Immigration* ambazo ndilo hasa Taifa lenyewe hilo kwa nini hazipigiwi kura mara mbili? Kwa hiyo, naomba kusema hivi kwenye masuala haya *technical* muachie *Attorney General* awasaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniongezee muda ili niyamalize haya. Hoja ya kusema kwamba mashirika haya ndiyo yaachwe kwa *Treasury Registrar*; ukweli ni kwamba *Treasury Registrar* ana mamlaka yake chini ya Sheria ya *Treasury Registrar Act*. Yeye ana mamlaka sasa ya kusimamia utendaji wa mashirika haya. Mamlaka haya ya Waziri yanayozungumzwa humu ni ya usimamizi wa masuala ya kisera na mamlaka hayo anapewa tangu kwenye kifungu cha sita (6) cha Sheria ya Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo masuala ya kisera, someni sheria mama ya mashirika ya umma kifungu cha sita (6) pale. Kwenye mambo ya utendaji sasa kuhakikisha kwamba yanafanya kazi kwa mujibu uliokusudiwa na yanajiendesha kibiashara, hakuna ufasadi, hakuna vitu gani hiyo ni kazi ya *Treasury Registrar* iko kwenye sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo pia, huyu Msajili wa Hazina hawezi kuteua viongozi hawa na yeye mwenyewe anateuliwa na Rais atateua nani? Kwa hiyo ibara ya 36, ibara ndogo ya Katiba inasema hivi:-

“Rais atakuwa na madaraka ya kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka ya viongozi wanaowajibika kuweka sera za idara na taasisi za Serikali, na watendaji wakuu

wanaowajibika kusimamia utekelezaji wa sera za idara na taasisi hizo katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, nafasi ambazo zitatajwa katika Katiba hii au katika sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge kwamba zitatajwa kwa uteuzi unaofanywa na Rais."

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, hawa lazima moja wateuliwe na Rais, kwamba Mtendaji Mkuu ateuliwe na Rais kama ambavyo Muswada unavyosema. Hawezi huyu akaachiwa akateuliwa na Waziri wala na *Treasury Registrar*. *Treasury Registrar* madaraka yake ni madogo sana, ni kwenye kusimamia utendaji bora wa mashirika haya ya umma ambayo Serikali ina hisa na ambayo Serikali haina hisa. Kwa mfano kuna mashirika mengine Serikali ina hisa kidogo sana, sasa unafanyaje, kule nako atateua *Treasury Registrar*? Kwa hiyo nilifikiri haya mawili ya kikatiba niyafafanue.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kushauri ni hili ambalo amelisema Mheshimiwa Saada Mkuya. Unajua ukija na *scheme* ya aina ile mnaanzisha ubaguzi usiokuwa na sababu, si tu kwamba ni kuvunja Katiba ibara ya 13(2), (4) na (5) pia sio utaratibu mzuri na hata ibara ya 17 (1) ya Katiba. Mimi nawafahamu Watanzania wenye asili ya Zanzibar ambao wengi wanaishi na kufanya kazi Bara. Kupata ajira katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au taasisi yoyote ya umma wala haiangalii Uzanzibari wala Utanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sifa tu ni kwamba ukishakuwa raia wa Tanzania una nafasi ya kufanya kazi kila sehemu. Kwa hiyo kwa utaratibu huu unaopendekezwa kwamba kama ni Mkurugenzi tu sijui Zanzibar anakaa pale pale wengine Wapemba wanakaa pale pale mnataka kulivunja Taifa hili. Ni utaratibu ambao Wabunge msiuruhusu, ni kinyume cha Katiba na naomba kuwashauri muachane na mapendekezo ya aina hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine linazungumzwa...

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

T A A R I F A

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaku.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Alichokizungumza Mwanasheria Mkuu na alichokizungumza Mheshimiwa Saada alitoa ushauri tu. Sasa Mwanasheria Mkuu ana haki ya kuchagua kutoka Bara au Zanzibar maana yake ni nafasi nyingi kama *IGP*, *CDF* na Kamishna wa *TRA* hawajawahi kutoka Zanzibar, na haya ni mambo ya Muungano. Sasa ni ushauri tu ulikuwa ule, kama ameipokea sawa, kama hakuipokea ajue na yeye ni mshauri wa Rais anaweza kumshauri. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali unaipokea taarifa hiyo?

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo siipokei na naomba uniruhusu niendelee. Ushauri huo ndio tunaoujibu sasa hadharani kama ulivyotolewa hadharani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nimeombwa nichangie ni hili ambalo limezungumzwa na Mheshimiwa Richard Mbogo ambaye pamoja na kuunga mkono ameona kwamba kile kifungu cha 22(1) (a) kwenye Muswada kiondolewe ili shirika liweze kujiendesha. Pia nimesikia michango mingi ya Waheshimiwa Wabunge ambao wanataka sasa shirika hili liwezeshwe kimtaji ili liweze kwenda kufika sehemu ambazo huduma hizi hazifikiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hiki kimewekwa hapo makusudi ili kulisaidia sasa shirika hili liwe na mtaji wa kutosha kuja kutekeleza majukumu ambayo sasa linapewa ikiwa ni pamoja na kupeleka huduma za miundombinu katika sehemu mbalimbali ambako huduma hizi hazipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri kwamba kuna umuhimu sana kifungu hiki kikabaki, kisipobaki na wengine wamesema hapa sehemu nyingine hakuna, sasa watapata wapi pesa za kujiendeshea lazima waendeshwe pale. Ila kazi ya Wabunge sasa itakuwa ni kuishauri Serikali mbona hamjatenga fedha za kuwezesha miundombinu ili Shirika hili la simu lifike huko tunakokwenda?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu kwamba Serikali kwa kweli ilisikiliza sana Kamati ya Miundombinu ikafanya jedwali la marekebisho. Kwa hiyo, yale ambaye umeyazungumza tulishawasilisha ndani ya Bunge lako Tukufu jedwali la marekebisho ambalo limeyafikiria yote haya. Yale ambayo pia mmechangia asubuhi tayari tumeshaweka kwenye jedwali la marekebisho na tumewagawia Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE - NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama kwa mara nyingine mbele yenu kwa ajili ya kuchangia hoja yetu hii ya Shirika la Mawasiliano Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nianze kwa kuwashauri Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hakuna mahali hata sehemu moja ambako Serikali imezuia au inawatisha wawekezaji kutoka sekta binafsi kuja kuwekeza katika sekta hii maalum kabisa ya mawasiliano. Kumekuwa na maelezo mengi sana kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na hasa wa upande wa pili kwamba kitendo kinachofanywa na Serikali kinakusudia kuwatisha wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo mashirika, tunazo hizi sekta binafsi, kampuni ambazo zinaendesha huduma za mawasiliano kama *Tigo*, *Vodacom* na *Halotel*, tunafanya nazo kazi vizuri kabisa na tunazipatia ushirikiano wa kutosha na bado tunaendelea kuwashawishi na kuwakaribisha sana wawekezaji wengine waje kuwekeza kwenye sekta hii ya mawasiliano kwa sababu nafasi zipo na uwanja mpana upo kwa ajili ya kuwekeza. Hatuwezi kumtisha mtu na hatuna nia hiyo wala hatutakuja kuwa na nia hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri hawa wenzetu wanapokuwa wanasifia Mataifa mengine wajue kwamba nchi kama Marekani wana shirika imara kabisa la simu linaitwa *AT&T*. Hilo ni mali ya Serikali asilimia 100 na linaendeshwa na Serikali na ndilo linalofanya kazi nzuri sana kwenye soko la mawasiliano katika nchi ya Marekani. Hiyo ni nchi ambayo mara zote wanafanya mfano wake; lakini vile vile tuna *British Telecommunication* inamilikiwa kwa asilimia 100 na inafanya kazi nzuri sana katika sekta ya mawasiliano ya simu kwenye nchi ya Uingereza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Serikali tutaendelea kuhakikisha kwamba tunaliwezesha shirika letu hili jipya la simu kwa kila hatua kuhakikisha kwamba linakamata soko na hao wengine waje washindane wala sisi hatuwezi kuwazuia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge kadhaa ambao walizungumzia kuhusu gharama za mitandao ya simu na hasa za kwenda nje. Nieleze tu ukweli Waheshimiwa Wabunge lazima wafikirie na wakubaliane na sisi, kwamba miaka 10 iliyopita gharama za simu hazikuwa hivyo. Nashukuru Mungu kwamba kuna Mbunge mmojawapo ameeleza kabisa kwamba Shirika la Simu lilivyokuwepo kipindi hicho yeye hakuwepo, kwa hiyo hajui lolote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimfahamishe tu na nimpe faida kidogo, kwamba wakati hizi huduma za simu zinaanza tulianza na shirika linaitwa *Tritel*, wakati ule ukipiga

unachajiwa na ukipigiwa unachajiwa; na kwa kuwa haukuwepo siwezi kukulaumu. Naomba akamuulize hata kaka yake, baba yake mdogo na vitu kama hivyo atamweleza kwamba hizo huduma zilikuwa ghali sana tofauti na sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tutahakikisha kwamba huduma zinaendelea kuwa nafuu kwa sababu kutokana na *competition* iliyopo, mashirika yenyewe na hizi kampuni binafsi zina-*regulate* bei zao kuvutia watumiaji. Vile vile kuwepo kwa mkongo wa Taifa kutalisaidia Shirika letu la *TTCL* kuhakikisha kwamba linakuwa na gharama nafuu sana kwenye ushindani uliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu waliuliza sana kwamba kwa nini Kampuni ya *TTCL* tumeifuta na kwa nini tunaleta hii mpya. Naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wezangu; miaka ya mwanzoni ya 1990 wakati tunafanya ubinafsishaji, wakati wa wimbi la ubinafsishaji tulibinafsisha mashirika mengi sana na moja kati ya vitu tulivyofanya kosa tukabinafsisha ni Benki yetu ya *NBC*. Ninyi ni mashahidi, wachache mlikuwepo, wengine najua hamkuwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ile benki yetu ambayo ilikuwa imara kabisa tulilazimishwa kwa ulaghai ambao ninyi wengine mnauunga mkono, kwamba tuigawe kwenye taasisi tatu na matokeo yake tumeendelea kuyumba sana. Kwa sababu hiyo, sasa hivi Serikali imejipanga kutokurudia makosa hayo. Ni lazima wanaotaka kuja kushindana kwenye sekta mbalimbali waje wakiwa wamejipanga, wakute kwamba sisi tuko imara na tunaendesha shughuli zetu bila kuwategemea wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hili Shirika la Mawasiliano (*TTCL*), tumelianzisha kwa sababu lililokuwepo lilikuwa limeanza kufanya vibaya baada ya kuamini kwamba tukichanganya na sekta binafsi mambo yanaweza yakaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaeleze tu Waheshimiwa Wabunge; ni lazima wakubaliane na Muswada wetu kwa sababu hatimaye Shirika letu hili la Mawasiliano litawatumikia wananchi wa Tanzania na ni mali ya wananchi wa Tanzania. Linafanya kazi kwa ajili ya wananchi wa Tanzania wote. Pia ni shirika ambalo linatulinda kiusalama na mwisho wa siku faida itakayopatikana itaingizwa katika Hazina Kuu ya Serikali kwa ajili ya kugawiwa tujengewe barabara, hospitali na zahanati ambazo Waheshimiwa Wabunge wote tunahitaji kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliomba sana *TTCL* ijiorodheshe kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam *(The Dar es Salaam Stock Exchange Market)*. Kama nilivyozungumza hapo awali, hili shirika ni mali ya Serikali, Shirika hili la Mawasiliano Tanzania lipo kwa ajili ya Watanzania, ni kwa maslahi mapana ya nchi, hatutegemei kulipeleka kwenye soko la hisa kwa muda huu kwa sababu tunategemea lilinde maslahi mazima ya nchi kiuchumi, kiusalama na kijamii. Kwa hiyo tunategemea kuendelea kulilinda kwa hali yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema hapo awali, tutaendelea kuliwezesha na tutaendelea kuhakikisha kwamba linapata *management* stahiki bila kujali mapendekezo mengi ambayo yanakuja kinyume na Muswada tuliouleta. Kwa sababu shirika hili likiyumba ni sisi Waheshimiwa Wabunge tutaingia huku tena kuanza kulaumu. Sisi tumepanga majukumu ya watendaji wa shirika hili, tumepanga kwa kuangalia maslahi ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kabisa kwamba kuna suala zima la *experience* ya atakayeliongoza shirika. Hili suala limejikita zaidi kwenye kanuni za mashirika ya umma. Kwenye taratibu za ajira kwa mashirika ya umma kuna vigezo ambavyo vinazingatiwa, na kigezo kimojawapo cha kuwa mtendaji mkuu wa shirika ni lazima uwe na *experience* ya kutosha kwenye tasnia hiyo au zinazofanana na hiyo. Naisi

tumezingatia hilo katika kuhakikisha kwamba shirika letu linapata uongozi ulio imara, uongozi bora ambao utatusogeza mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

NAIBU SPIKA: Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, mtoa hoja.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujalia kukutana hapa tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza nikushukuru wewe mwenyewe binafsi na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uwezo na umahiri mkubwa mnaonesha katika kuliendesha Bunge letu Tukufu. Aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia hoja yangu niliyowasilisha hapa Bungeni leo asubuhi na wametoa michango mizuri sana ambayo tumeichukua na tumeifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge 14 waliochangia katika Muswada huu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania wa Mwaka 2017 *(The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017)*. Michango ya Waheshimiwa Wabunge wote ilikuwa ni mizuri sana na ilisheheni mapendekezo, ushauri na hasa namna bora ya kuendeleza Shirika la Mawasiliano Tanzania ili liweze kuchangia zaidi katika maendeleo ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri na maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu yamezingatiwa. Vilevile maoni na ushauri kutoka Kambi Rasmi ya Upinzani utazingatiwa. Hata hivyo, ningependa nitumie muda wangu mfupi sana kujibu baadhi ya hoja zilizowasilishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nia ya Serikali yetu ni kuweka mikakati mizuri ya kuliimarisha Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*) ili nalo liweze kuleta ushindani mkubwa kwenye soko la mawasiliano. Kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamelalamika sana kwa nini tunafanya *corporation* au ushirika, hili sio jambo geni, kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyosema, nchi mbalimbali duniani zina utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ambao nyote mnauona ni wa *Viettel* ya Vietnam. Hii ni kampuni ya Serikali, na si tu kampuni ya Serikali, ni kampuni ya jeshi na inafanya kazi kubwa na hapa Tanzania kwa muda mfupi tumeona wana takribani *subscribers* au wateja milioni 3.5. Ukienda China, *China Telecom* ni kampuni ya Serikali na ni kampuni ambayo inakuwa kwa kasi kubwa duniani, *China Mobile* ni kampuni ya Serikali ambayo inafanya kazi vizuri sana. Ukienda Singapore kuna *Singtel*, ni kampuni ya Serikali inafanya vizuri sana. Naweza kutaja kampuni nyingi za mawasiliano za simu za Serikali ambazo zinafanya vizuri; jambo muhimu ni usimamizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu, Serikali yetu na Serikali ya Awamu ya Tano, Awamu ya Nne, tumefanya kazi kubwa sana kuimarisha Shirika la Simu la Tanzania. Kuanzia mwaka 2009 Serikali ilikabidhi Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa Shirika la Simu la *TTCL*. Mkongo ule unagharimu takribani Dola za Kimarekani milioni mia mbili na wamekabidhiwa *TTCL* na *TTCL* inautumia na inauza huduma hizo za mkongo kwa kampuni zote Tanzania. Kwa ufupi, kampuni zote za Tanzania zinazonunua huduma ya mkongo kutoka Kampuni ya *TTCL* zimeridhika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2014, Serikali iliipa Kampuni ya *TTCL* masafa ya *megahertz* 1,800 kwa ajili ya kupeleka huduma ya simu za mkononi na *TTCL* sasa hivi imeanza kufanya kazi hiyo. Mwaka 2014 kampuni ya Serikali iliipa Kampuni ya *TTCL bandwidth* ya Serikali kwa ajili ya taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2015, Serikali ilifuta deni la *TTCL* takribani bilioni 25 ambazo ilikuwa ikidaiwa na *TCRA*. Mwaka 2015 tena Serikali ilifuta deni la *TTCL* takribani bilioni 76, hii yote tunaifanya *TTCL* iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha Kampuni ya *TTCL* mwaka 2016, Serikali iliipa *TTCL data center* ambayo leo hii ina wateja 28. Kati ya wateja hao, wateja 19 ni taasisi za Serikali na tisa ni kutoka Sekta Binafsi. Mwaka 2016, katika kuiimarisha *TTCL* Serikali ilinunua *shares za Bharti Airtel* kwa shilingi takribani bilioni 14.7 ili kuifanya *TTCL* kuwa kampuni ya Serikali kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2017, ili *TTCL* iweze kuendelea na huduma ya *4G*, Serikali tumeipa Kampuni ya *TTCL* masafa ya *megahertz 800*; ni kampuni pekee sasa hivi tuliyoipa masafa hayo ambayo inaweza kutoa huduma bora za *4G*. Mwaka 2017, *TTCL* ilianzisha Kampuni ya *TTCL Pesa* ambayo iko chini ya *TTCL* wenyewe na leo hii tunatayarisha sheria hii ili kuiwezesha zaidi Kampuni yetu ya *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufupi, katika huduma za *data* hapa Tanzania, kampuni bora ya huduma hizo ni *TTCL*. Huwezi ukailinganisha na *Vodacom*, *Airtel*, *Tigo* wala *Halotel* kwenye huduma ya *data*. Kwa hiyo kama tutaipitisha sheria hii na kuiwezesha *TTCL* tunaamini kwamba itakuwa kampuni kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto nne muhimu ambazo zimetufanya tuweze kutengeneza sheria hii. Changamoto ya kwanza kabisa ni ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano. Sekta hii inakua kila siku na ni muhimu kuiwezesha kampuni yako ili iweze kushindana. Kwa hiyo, tumeona tuitengeneze sheria hii ili kampuni ya *TTCL* iweze kushindana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya pili ya msingi, miundombinu ya *TTCL* sasa hivi imezeeka, kwa hiyo iko haja ya kuwezesha *TTCL* ili iweze kuendana na huduma za mawasiliano na ushindani kwa kuwekeza kwenye mitambo

mipya. Sababu ya tatu ya msingi, Watanzania wengi wako vijijini na kwenye vijiji vyetu kuna changamoto kubwa ya mawasiliano. Kwa kuiwezesha Kampuni yetu ya Mawasiliano tunaamini sasa vijiji vingi vya Tanzania vitapata huduma ya mawasiliano ambayo ni bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waheshimiwa Wabunge wengi walivyosema, suala la usalama halina mjadala. *TTCL* kiusalama ni kampuni moja nzuri. Kwa kuwafahamisha tu; wakati Rais wa Marekani alipotembelea Tanzania, kampuni ambayo alitumia kwenye huduma za mawasiliano ni *TTCL*, hakwenda kutumia *Vodacom*, *Airtel* wala nini, mawasiliano yote yaliunganishwa kwenye mtandao wa *TTCL* kwa vile *TTCL* ni kampuni muhimu na ipo haja ya kuiimarisha kwenye mambo ya kiusalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na Mbunge mmoja, Mheshimiwa Saada, alizungumzia kuhusu utaratibu wa utendaji kazi wa *TTCL*. Naomba nimfahamisha tu; *TTCL* inafanya kazi kiutaratibu wa ukanda. Kuna kanda ya kwanza tunaita Kanda ya Dar es Salaam, kuna Kanda ya Pwani ambayo yenyewe inachukua Zanzibar, Pemba, Mtwara na Lindi; kuna Kanda ya Kaskazini, kuna Kanda ya Ziwa na kuna Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Kanda ya Pwani inachukua Zanzibar, Pemba, Mtwara na Lindi na utaratibu wa ajira wa *TTCL* Mtanzania yeyote anafanya kazi kwenye *TTCL*. Tunachoangalia sisi muhimu ni uwezo wa mtu na sifa za mtu. Ni jambo ambalo limenishtua sana na sikutegemea Mheshimiwa Saada angesema vile, kwamba anataka *TTCL* Zanzibar ifanywe na Wazanzibari wenyewe tu, hicho kitu sikutegemea, hasa kutoka kwa kiongozi kama Mheshimiwa Saada ambaye amekuwepo Serikalini; hasa kutoka kwa kiongozi kama Mheshimiwa Saada ambaye ana uzoefu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea Mheshimiwa Saada asilete mawazo na maoni kama hayo...

MHE. SAADA MKUYA SALUM: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Saada Mkuya, naomba ukae, hakuna taarifa akiwa amesimama Waziri hapa mbele; hakuna taarifa kikanuni.

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea mawazo au maoni kama yale wazungumze watu wa kijijini kule Pemba, nilitegemea mawazo kama yale wazungumze watu wa vijiwani pale Darajani, sikutegemea kabisa. Nilitegemea yeye kama kiongozi na sisi kama Watanzania katika kujenga umoja wetu tuseme kila Mtanzania aweze kufanya mahali popote pa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi tunavyoongea leo Meneja wa *TTCL* Zanzibar ni Mzanzibari anaitwa Mohamed Mohamed, Meneja wa *TTCL* Pemba ni Mzanzibari, anaitwa Ngwali Hamis. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Saada, hazijui kiutendaji; Mtendaji Mkuu wa *TTCL* mwaka 2010 mpaka 2012 alikuwa *Engineer* Said Ameir ambaye mimi ni mwalimu wangu, ni Mzanzibari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sikutegemea; nasema tena, ni kitu ambacho kimeniama sana, hasa kwa mimi kwa sababu haya mambo siyajui; nilitegemea kama Mtanzania unatoka Lindi kama kuna fursa Zanzibar kwenye *TTCL* uende, kama Mzanzibari unatoka Zanzibar kuna fursa Kibondo ama wapi, *anywhere*, aende; hii ndiyo Tanzania tunayoitaka, hii ndiyo Tanzania Watanzania kule nje wanayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikienda zaidi; tuna *TTCL Pesa*, ina watendaji watano, *senior management positions* kuna Watanzania watano, watatu ni Wazanzibari. Mkuu wa *Head of Compliance* anaitwa ndugu Lulu, ni kutoka Zanzibar, bwana Hamis Rashid unatoka Zanzibar, ni mkuu pale, ndugu Nasra Mulher, pengine ni ndugu yetu, unatoka Zanzibar. Sasa leo tunapeleka *message* kwamba hawa wote tuwatoe tuwapeleke Zanzibar ama Pemba, sio sahihi, hatuwatendei

haki Watanzania. Sisi viongozi tuoneshe mfano, hasa sisi tuliopo Serikalini na wengine waliokaa Serikalini, wanajua utaratibu; Watanzania wote ni wamoja, lazima tujenge umoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Saada, Serikali ya SMZ itam-*support* kiongozi yeyote ambaye anafanya kazi *TTCL* Zanzibar au Tanzania nzima, haitambagua Mtanzania yeyote; naomba alifahamu hilo na Waheshimiwa Wabunge wote naomba mlijue hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi walizungumzia suala la kuchagua Wajumbe wa Bodi kutoka mmoja kuwa wawili; mwezi wa Tisa sisi tulikwenda Zanzibar, kama kawaida yetu ikiwa jambo la Muungano tunashauriana na wenzetu wa Zanzibar na wenzetu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ikasema kwamba tuongeze Mjumbe mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujua umuhimu wetu na kwa kujua ushirikiano baina ya Serikali hizo mbili, tulilipokea na tumeleta mabadiliko kwenye Muswada huu, Wajumbe kutoka Zanzibar sasa watakuwa wawili. Naomba niwahakikishie Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar maoni mtakayotupatia wakati wowote tutayachukua, si kwa Muswada huu tu lakini Miswada yote inayohusu mambo ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na *issue* ya uzoefu wa Mtendaji Mkuu. Sisi tumependekeza kwenye Muswada tuweke miaka minane na miaka minane ni sahihi kwa Mtendaji Mkuu wa shirika kama lile. Huwezi kumchukua mtu wa mwaka mmoja ukaenda kumjaribu. Ntawapa mifano; Mtendaji Mkuu wa Vodacom, Ian Forare, ana umri wa miaka 34 lakini ana *experience* ya miaka zaidi ya 12 ya *senior management*. Mtendaji Mkuu wa *Airtel* ni kijana mdogo, ana miaka 40, lakini ana zaidi ya miaka kumi ya *experience* kwenye *senior management*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi tu kufanya mtu wa miaka miwili au mwaka mmoja tumpeleke, si sahihi, lazima tuweke utaratibu wa kisheria ambao tunaweka muda wa kutosha (*experience*). Tusichanganye hapa baina ya *CEO* na *entrepreneur*, ni vitu tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, *entrepreneurs* au mjasiriamali anaweza kuvumbua pengine akatengeneza *software* yeye ni mvumbuaji anaweza kutengeneza pesa nyingi lakini kiutendaji kama Kampuni hawezi kufanya. Lazima kwenye suala la Kampuni tuheshimu uzoefu kwa vile sisi Serikali tumeona hili ni jambo sahihi na tutaendelea nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine ambao nyote mnajua, mtendaji mkuu wa *National housing*, Mchechu yeye ni *CEO* mzuri sana na ana uzoefu mkubwa wa zaidi ya miaka 10 ya *senior management position*. Mwaka 2002 alikuwa ni *director* kwenye Benki ya *Standard Bank*, ana uzoefu mkubwa. Sasa hatuwezi kujaribu kuchukua tu mtu wa mwaka mmoja, miaka miwili tukampeleka kwenye *position* ile. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba hii nafasi ni kubwa tusicheze na makampuni yetu. Kama tunataka makampuni haya yasimame lazima tuweke watu wenye uzoefu. Tunaweza kupata kijana tofauti ambaye ana uzoefu mdogo tukamweka lakini tuweke utaratibu. Nakutolea mfano mzuri wa *Ian*, *Ian* miaka 34 ana uzoefu wa miaka 12, *CEO* wa *Vodacom*. Si kwamba mtu akiwa kijana mdogo hana uzoefu mnakosea, kwa hiyo naomba muelewe pale sisi tumeweka huo umri kwa sababu tunaamini tukiweka mtu mwenye umri huo atasimamia Shirika letu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la mkongo, kuna mkongo wa Zanzibar na mkongo wa Taifa. *TTCL* wanasimamia mkono wa Taifa ambao wenyewe una kilometa 7,560, umeunganisha mikoa yote ya Tanzania, tumewapa *TTCL* ndio wanaosimamia hili. *TTCL* tumewapa vile vile kuendesha *data center*, lakini mkongo za Zanzibar unasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wenyewe ni kilometa nafikiri

400 tu kwa vile iko huko Zanzibar na inafanya kazi Zanzibar na hatuna mpango wa kwenda kuuchukua, kwa hiyo naomba mlijue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mkongo tena unazungumzwa, mkongo wa *Halotel*; *Halotel* imejenga mkongo takribani kilometa 18,000. Kila unapopita Mkongo ule zimeweka *pair* sita kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Mkongo wa *Halotel* haushindani na mkongo wa Taifa. wamekwenda kwenye Wilaya, na *condition* ama sharti ambalo tuliwapa *Halotel* katika kuweka mkongo lazima wasishindane na mkongo wa Taifa, na ndivyo hivyo tulivyo. Kwa hiyo, naomba tu niwahakikishie Watanzania na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwamba Serikali inasimamia miundombinu yote ya mawasiliano hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa njikite kwenye hoja kwa haraka haraka. Kwanza kuna hoja ya Kamati ambapo Kamati inasema Shirika linaloanzishwa liondokane na mfumo wa utendaji wa urasimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania nataka niwahakikishie kwamba Shirika hili tunalolanzisha sasa litakuwa ni Shirika la mfano. Tutalisimamia kwa nguvu zetu zote ili kuhakikisha kwamba linafanya kazi ile ambayo ilikusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la Mtendaji Mkuu nimeshalizungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja, ili Shirika liweze kufanya vizuri, Bodi na Mtendaji Mkuu wa Shirika wapewe madaraka kamili. Taasisi zote za Serikali, Bodi pamoja na watendaji tunawapa mamlaka kamili na wasipoteteleza mamlaka hayo tuwafukuza. Kwa hiyo, naomba waelewe Watanzania ama watendaji wenyewe waelewe, tunawapa madaraka kamili na wanafanya hivyo na pale wanapoharibu tunawaambia *the door is open bye bye*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeendelea na kusema kuna kipengele namba 7(7) kuhusu Waziri ku-*consult* Mwenyekiti. Hili tumelichukua na tumelifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwa haraka haraka kwenye hoja za Mbunge mmoja mmoja. Kuna hoja ya Mheshimiwa Zuberi, anauliza kwa nini Serikali ilibinafsisha Kampuni na sasa tumeamua kuirejesha? Ni kweli Serikali iliamua kuibinafsisha kampuni kwa kuzingatia sera zilizokuwepo wakati huo na tumeona sasa sera hizo haziwezi kuleta tija kwa Shirika, kwa sababu hii tumeamua kubadilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hija nyingine ya Mheshimiwa Zuberi anasema, namna gani Serikali imejipanga ili Shirika liweze kushiriki katika ushindani kwa maslahi ya Taifa? Majibu ya hoja hiyo ni kama ifuatavyo. Serikali imejipanga kwa kutayarisha Mpango wa Biashara wa miaka mitano wenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Shirika la Simu la *TTCL* ili iweze kushindana. Baada ya mpango huo tutakuwa tunafuatilia kila baada ya muda ili kuona kwamba mpango huo unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja nyingine ya Mheshimiwa Zuberi, anasema namna gani *data center* itatumika kikamilifu. Kama nilivyosema kwenye majibu yangu, Serikali inaendelea kuhamasisha matumizi ya *data center* ambapo sasa kuna taasisi 28 ambapo taasisi 19 ni za Serikali na taasisi tisa ni za watu binafsi. Tunaendelea kuhamasisha watu wengi waweze kuitumia *data center* hiyo na nchi za jirani kwa mfano Burundi, Rwanda zote tunataka wahifadhie *data* zao hapa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna hoja kwamba, je, Serikali imepanga kuwekeza mtaji kiasi gani katika shirika. Kama nilivyosema, Serikali imeandaa Mpango Mkakati wa Biashara wa miaka mitano ambao huanzia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi mwaka 2021/2022, ambao tunaamini baada ya makadirio haya yatakapoletwa ndipo tutaweza kutenga mtaji kwa ajili ya Shirika letu la *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya Mheshimiwa Cecilia Pareso, kwamba kwa nini tunatoka kuwa kampuni na kuwa shirika? Hiyo ndiyo hoja yake na majibu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika lililopo kwa sasa, kampuni ya TTCL inatoa fursa kwa kampuni kubinafsishwa ilhali nia ya Serikali kwa sasa ni kulifanya shirika liwe madhubuti. Kwa hivyo iko haja ya kubadilisha sheria hii iliyopo. Pia sheria iliyopo haijaainisha masuala ya usimamizi wa miundombinu ya kimkakati, hivyo Muswada huu unapendekeza kuainisha miundombinu ya kimkakati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, anaendelea kuuliza, je, shirika linaweza kulinda usalama? Muswada unaopendekezwa unaainisha ulinzi wa usalama wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia amezungumza kuhusu suala la bodi ambalo tayari tumeshalizingumza, kwamba tumeweka wajumbe wawili kwenye Bodi yetu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine Mheshimiwa Said Kubenea aliuliza je, Serikali ilikosea wakati wa ubinafsishaji wa TTCL? Mazingira ya wakati huo yalilazimu Serikali kuchukua hatua hizo ambapo kwa sasa mazingira yamebadilika na ndiyo tumeamua kuleta Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ameuliza tena, kwa nini muwekezaji ameng'oa mitambo, hakuja na mtaji na Serikali ikanunua hisa? Katika kuiandaa TTCL kuingia ubia na mwekezaji mitambo yote ambayo haikuwa na uhusiano na masuala ya utoaji wa huduma za simu ilichukuliwa na Serikali, lakini si kwamba mwekezaji aling'oa mitambo hiyo. Katika makubaliano na mwekezaji kuingia ubia na Serikali, mwekezaji alipaswa kununua hisa asilimia 35 kama sehemu yake ya uwekezaji ndani ya Kampuni. Serikali ilinunua hisa hizo za mwekezaji asilimia 35 kwa shilingi bilioni 14.7 kwa ajili ya kuifanya kampuni ya simu iwe asilimia 100 ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya Mheshimiwa Saada Mkuya nilishayajibu sipendi nirejee tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbaraka dau kulikuwa na hoja Shirika hili ni la kimkakati. Ni kweli Sheria inayopendekeza imezingatia suala hili kwamba Shirika hili ni la mkakati. Kuna suala je, ni kampuni ngapi na benki ngapi zinatumia *data center* tangu ilipoanzishwa? Kama nilivyosema, mpaka sasa hivi kuna Taasisi 28 zinatumia *data center*. Taasisi 19 ni za Serikali na Taasisi tisa ni za sekta binafsi. Nia yetu ni kuhakikisha kwamba taasisi zote za Serikali zinatumia *data center*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, iko hoja tena inasema Serikali iongeze mtaji kwa *TTCL* na iuze hisa kwenye soko la hisa ili kutunisha mtaji wa *TTCL*. Mpango Mkakati wa Kibiashara wa *TTCL* utainisha mahitaji ya mtaji na hivyo Serikali tutajipanga kutokana na mpango mkakati huo. Aidha, kwa sasa Serikali imejikita zaidi katika kumiliki Kampuni ya *TTCL* kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, anaendelea Mheshimiwa Dau kuuliza Serikali impe mamlaka Bodi na *CEO* kufanyakazi bila kuingiliwa. Siku zote Serikali inaipa Bodi mamlaka na Mtendaji Mkuu wakati wote ili kuhakikisha wanaweza kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Deo ambaye katika hoja yake ya kwanza anasema kwamba *TTCL* ipatiwe mtaji wa kutosha ili iweze kujiendesha kwa faida na kupeleka gawio Serikalini. Ushauri huo umepokelewa

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* ipewe Mkongo wa Taifa ili iweze kujiimarisha. Kwa sasa Serikali imeipa mkongo wa Taifa na *data center TTCL* ili iweze kujiendesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, anaendelea na hoja yake kuhusu Sheria ya *PPRA* kwa *TTCL* iangaliwe kwa baadhi ya maeneo ili iweze kujiendesha kibiashara. Sheria ya Manunuzi

iliyopo kwa sasa inajitosheleza na inatoa mwanya kwa kila aina ya manunuzi yanayohitajika kulingana na mazingira ya manunuzi husika

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, tutaendelea na utaratibu ulio mbele yetu. Waheshimiwa Wabunge naomba mkae.

Kabla hatujaendelea na hatua inayofuata, tunao wageni ambao wamekuja Bungeni jioni hii na hawa ni wanafunzi 105 wa kidato cha nne na Walimu watano kutoka shule ya sekondari Msalato iliyopo hapa Mkoani Dodoma. Karibuni sana watoto wetu, tunaamini mnajifunza kuhusu Bunge na pengine wengine mtakuja kuungana nasi huko mbele, karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

NDG. THEONES RUHILABARKE – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa Mwaka 2017 (*The Tanzania Telecommunications Corporation Bill, 2017*)

Ibara ya 1

Ibara ya 2

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 3

Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

Ibara ya 7

Ibara ya 8

Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 10

Ibara Mpya ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 12

Ibara Mpya ya 13

Ibara Mpya ya 14

Ibara Mpya ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 21

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 23

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara Mpya ya 25

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

**Hapa kiliongezwa Kichwa cha habari kipya kati ya
Ibara ya 25 na 26 (kwa maana ya Sehemu ya
Saba ya Muswada)**

Ongezeko la kichwa cha habari

*(Kichwa cha habari kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na
Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya Mpya 26
Ibara Mpya ya 27
Ibara Mpya ya 28

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara Mpya ya 29
Ibara Mpya ya 30
Ibara Mpya ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali

NAIBU SPIKA: Jedwali pamoja na marekebisho kwa sababu yako katika vifungu vitatu vya jedwali hilo tutaenda kifungu kimoja baada ya kingine.

Ibara ya 1 ya Jedwali

*(Ibara ya Jedwali iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 2 ya Jedwali
Ibara ya 3 ya Jedwali

*(Ibara za Jedwali zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na
Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 4 ya Jedwali

(Ibara ya Jedwali iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 5 ya Jedwali

Ibara ya 6 ya Jedwali

(Ibara za Jedwali zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibara ya 7 ya Jedwali

(Ibara ya Jedwali iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)

Ibara ya 8 ya Jedwali

Ibara ya 9 ya Jedwali

Ibara ya 10 ya Jedwali

(Ibara za Jedwali zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH- KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti kamati ya Bunge zima imemaliza kazi yake.

NAIBU SPIKA: Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada ibara kwa ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Shirika la Mawasiliano Tanzania wa 2017 sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makofi)

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA
MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

NAIBU SPIKA: Hoja imeungwa mkono. Kwa hivyo tutaendelea na utaratibu wetu, Katibu.

NDG. THEONEST RUHILABAKE- KATIBU MEZANI:

Muswada wa Sheria kwa ajili ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Tanzania, kuweka muundo wa utawala na uendeshaji wa Shirika, Kuainisha majukumu ya Shirika ikiwemo kusimamia huduma za Mawasiliano na Miundombinu ya kimkakati ya mawasiliano na kuwa na Shirika bora na salama la mawasiliano lenye kuwezesha uchumi na biashara endelevu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo *(A Bill for an Act to make Provisions for Establishment of Tanzania Telecommunication Corporation, Management of Strategic Telecommunication Infrastructure, Commercial and Economic viability of Telecommunication Services, and to provide for the other related matters.*

(Kusomwa Mara ya Tatu)

(Muswada wa Sheria wa Serikali Ulipitishwa na Bunge)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumemaliza utaratibu wetu kwahiyi sisi kama Bunge tumeshamaliza kazi. Tuwapongeze sana Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Manaibu wake kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wameyatoa kwenye hatua mbalimbali za kutengeneza ama kutunga sheria hii na baadaye kuleta mapendekezo ya mabadiliko ambayo leo jioni hii Wabunge wamekubaliana nayo. Kwa hiyo niwapongeze sana Waziri na timu yako ya

wataalam kwa kuleta Muswada huu ambao Bunge sasa limeshaupitisha. Niwatakie kheri naamini kwamba Mheshimiwa Rais atakapousaini kwa mujibu wa matakwa ya Katiba yetu na ninyi mtaweza kuanza kuutekeleza kwa kadri ambavyo sheria imepitishwa na Bunge hili. Kwa hiyo, niwatakie heri katika utekelezaji wa sheria hii pale ambapo Mheshimiwa Rais atakuwa ameshaweka saini yake.

Waheshimiwa Wabunge na ninyi niwashukuru sana kwa ushiriki mkubwa sana; kwanza nianze na Kamati kwa niaba yetu sisi sote kwa kazi kubwa sana ambayo wameifanya ya kupitia Muswada huu na kuweza kutusaidia kutuonesha maeneo ambayo wao wameshashauri na mpaka Serikali imekubaliana na hayo. Kwa hiyo, ahsanteni kwa kazi nzuri; lakini pia na Wabunge wengine ambao si sehemu ya hiyo Kamati ila wamesoma Muswada huu na wameweza kutoa maoni yao. Kwa hiyo, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo moja, linatoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Shuguli za Bunge. Waheshimiwa Wabunge mnatangaziwa kwamba mnatakiwa kujaza fomu za tamko la viongozi wa umma kuhusu rasilimali na madeni kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma namba 13 ya mwaka 1995, na namba tano ya mwaka 2001, kifungu cha tisa (9) na 11.

Fomu hizo zinapatikana katika Ofisi ya Spika, chumba namba 120, ghorofa ya kwanza, jengo la utawala. Hivyo Mbunge yeyote ambaye bado hajachukua fomu hizo, apite hapo na kuchukua ili aweze kuzijaza na pia aweze kuziwasilisha ofisini kwa Mheshimiwa Spika tarehe 20 Disemba, 2017; kabla ya kuziwasilisha kwa Kamishna wa Maadili tarehe 31 Disemba, 2017.

Waheshimiwa Wabunge, aidha wote mnakumbushwa kwamba ujazaji na urejeshaji wa fomu hizo ni hitaji la kisheria, hivyo mnaombwa sana kuzingatia muda uliowekwa. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka mwaka jana kuna watu ambao mpaka ikabidi waandike barua za

kujeleza kwa nini hawakupeleka kwa wakati. Kwa hiyo, sasa mmetangaziwa mapema kabisa. Fomu hizi ukishachukua ujaze na ziifike Ofisi ya Spika tarehe 20 Disemba halafu tarehe 31 zitafikia Ofisi ya Maadili kwa mujibu wa taratibu tulizonazo.

Waheshimiwa Wabunge kabla sijaahirisha shughuli za Bunge niwakumbushe jambo moja tu, matumizi ya kanuni ya 147. Tumetunga kanuni humu ndani kuhusu matumizi ya lugha; tunazo lugha rasmi za Bunge; sasa umekuwa ni utaratibu lakini pia tunakumbushana kila wakati.

Tunafahamu wazi hakuna mtu ambaye aliwahi kwenda nchi ambayo inazungumza lugha yao akawasikia wale watu wakizungumza wanachanganya na maneno ya Kiswahili labda nitamsubiri huyo mtu aje anioneshe mfano kwamba alishawahi kuona chombo rasmi kama cha Bunge huko kwingine watu wakichangia wanachanganya tu maneno kana kwamba ni kawaida. Tusichukulie kwamba ni kawaida hili jengo hili lina kanuni za uendeshaji ambazo tumejitungia wenyewe.

Kwa hiyo tuchukue muda sisi kama viongozi unapotaka kuzungumza fikiria kwanza neno la ile lugha unayotumia ili utumie lugha ile kwa ufasaha; lakini tusichukulie kwamba ni jambo la kawaida tunapochanganyachanganya lugha wakati wa kuchangia. Kwa sababu tumejitungia wenyewe kanuni na kuweka utaratibu, basi tufuate utaratibu huo na hapa huwa tunakuwa na watu ambao wanakuja kujifunza na wao wanaweza kuona ni kawaida kwamba mawasiliano mahususi kama haya unaweza ukawa unachanganya lugha zote. Si jambo ambalo tunatakiwa kulilea sisi kama viongozi lazima tufuate utaratibu tuliojiwekea.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mapaka siku ya kesho, siku ya Jumatano tarehe 15 Novemba, 2017, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 11.00 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya
Jumatano, Tarehe 15 Novemba, 2017, Saa Tatu Asubuhi)*